

# **IMAM ALI (A.S.) NDUGU YAKE MTUME MUHAMMAD (S.A.W.)**

**Usahihishaji Upya wa Historia na  
Utafiti wa Kina wa Madhehebu ya Shia**

## **JUZUU YA PILI**

Kimeandikwa na:  
**Sheikh Muhammad Jawad Chirri**

Kimetarjumiwa na:  
**Salman Shou**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 9987 - 427 - 512 - 89 - 8**

Kimeandikwa na:  
**Sheikh Muhammad Jawad Chirri**

Kimetarjumiwa na:  
**Salman Shou**

Kimepangwa katika Kompyuta na:  
**Hajat Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Oktoba,2011  
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:  
Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania


Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info



## YALIYOMO

### Sura ya Kumi na Sita

Imam wakati wa enzi ya makhalifa watatu.....	4
Khutba ya Abu Bakar .....	5
Kongamano la Kisiasa.....	6
Umar alizungumza kuhusu kongamano .....	7
Maswali ya kisharia na kihistoria.....	8
Aisha alisimulia kinyume.....	10
Chuki ya dhahiri bila sababu.....	12
Hadith ya Maghafir.....	13
Umar aliuona uchaguzi kama ni vurugu.....	15
Tamko la mwisho la Umar.....	16
Je! Kuchaguliwa kwa Abu Bakr kulikuwa ni halali?.....	21
Mteule wa Mtukufu Mtume (s.a.w.).....	24
Maquraishi na Ukhilifa.....	26
Maquraishi na uchaguzi havipatani.....	33

### Sura ya Kumi na Saba

Ali anautaamani huo Urithi.....	35
---------------------------------	----

### Sura ya Kumi na Nane


Abu Bakr amtaja mrith wake.....	41
---------------------------------	----

## Sura ya Kumi na Tisa

Umar anarithi.....	45
Umar na Elimu ya Ali.....	48
Majadiliano yahusuyo ukhalifa.....	52
Ukubwa wa Sera ya Umar.....	55
Alianda Mapema kabla juu ya Mustakabali wa Waislamu.....	57
Watu wachochezi kwenye mfumo wa utawala wa khalifa.....	61
Ukoo wa Bani umayyah uliingia kwenye Uongozi.....	62
Utawala wa Bani Umayyah ulikuwa si wa kuepukika.....	65
Kilichomaanishwa na ubashiri wa kinabii.....	65

## Sura ya Ishirini

Jopo la mkutano wa uchaguzi maelezo ya utaratibu.....	71
Je, Mtu asiyе Quraishi angeweza kuwa Khalifa.....	78
Hivi, Uislamu unakataza upinzani?.....	82
Onyo lisilotiliwa maanani.....	84
Uhalalisho kwa kutumia Hadithi .....	89
Kujitolea kwa kipekee kwa Ali.....	93
Utabiri	wa
kweli.....	94
Nia na matokeo.....	97
Tabaka Jipyा.....	99
Fursa iliyopotea.....	99



## Sura ya Ishirini na moja

Utawala wa Uthman.....	102
Mtu kiiunganishi.....	104
Upinzani ulianza mapema.....	105
Utekelezaji wa mpango wa bani Umayyah.....	109
Muawiya na Syria.....	110
Ibnabu Sarha akiwa Misri.....	111
Basrah.....	114
Sera legelege ya hazina ya Umma.....	117
Umar na Abu Hurairah.....	121
Misaada mingine kwa watu wengine.....	122
Sera ya magavana ni majimbo.....	122
Kuongezeka kwa upinzani.....	125
Wajumbe wengine wawili wa jopo la uchaguzi.....	127
Upinzani kutoka kwa masahaba wasiokuwa maquraishi.....	131
Abu Dharr uhamishoni.....	132
Uhamisho wa kudumu.....	133
Abdullah Ibn Mas'ud.....	136
Upinzani kutoka nje ya Madina.....	138
Imam anapatanisha.....	148
Makazi ya Khalifa yazingirwa.....	150
Kutubia na kujirudi.....	151
Muawiyah alitukatisha tamaa Khalifa.....	155
Watu wa Madina ya walimkatisha Tamaa Khalifa.....	156



## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili



### NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kitiwacho, *The Brother of the Prophet*. Sisi tumekiita, *Imam Ali (as) Ndugu wa Mtume Muhammad (saw)*. Kitabu hiki kilitungwa na aliyekuwa mubalighi mashuhuri wa dini ya Kiislamu ya Ushia nchini Marekani, Marehemu Sheikh Muhammad Jawad Chirri.

Kitabu hiki ni wasifu wa mtu mkubwa ambaye alikuwa mwanamume wa kwanza kuamini Utume wa Muhammad (saw) na wa kwanza kusali nyuma yake.

Imam Ali (as) hakuwa kiongozi wa Waislamu tu bali wa wanadamu wote. Maisha na mwenendo wa Imam Ali (as) umewavutia watu wote, marafiki na maadui, hali ambayo imemfanya kuwa kiongozi wa umma.

Mtukufu Mtume (saw) alimtangaza mwanzoni kabisa mwa Ujumbe wake katika kile kikao mashuhuri kabisa cha “karamu ya jamaa”, aliposema: “Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu, waziri wangu, khalifa wangu na mrithi wangu. Basi msikilizeni na mumtii.” Hili lilikuwa tangazo la mwanzo kabisa alilolitoa Mtukufu Mtume (saw) kwa ajili ya Imam Ali (as) na aliendelea kuwakumbusha Waislamu kuhusu uongozi wa Imam Ali baada yake katika matukio mengi yaliyofuata baadaye, kama vile katika tukio la Ghadir Khum pale aliposema: “*Man kuntu mauwahu fahadha Aliyyun mawlahu* – Yule ambaye mimi kwake ni kiongozi basi na huyu Ali ni kiongozi wake.” Na mwisho ni tukio la “Karatasi” pale Mtukufu Mtume (saw) alipokuwa ni mgonjwa na maradhi yamemzidi akaomba aletewe karatasi, kalamu na wino, mashuhuri kama “hadithi ya karatasi.”

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwashudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Maalim Dhikir U. Kiondo (ambaye sasa ni marehemu - Allah amrehemu) kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyininge hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.


Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu ya dini na ya kijamii.

**Mchapishaji:**

**Al-Itrah Foundation**

**S. L. P. 19701**

**Dar-es-Salaam.**



## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### BIBLIOGRAFIA UBAINIFU

Tarehe zilizotajwa kwenye bibliografia hii zimetegemea Kalenda ya Kiislamu ambayo ilianza kwa tukio la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuondoka Makka na kwenda Madina. Tukio hilo la kuondoka huitwa ‘Hijiriya’ ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambalo lilitokea mwaka wa 622 Baada ya kuzaliwa Isa (a.s.).

Endapo msomaji anataka kubadilisha tarehe kutoka tarehe za Kiislamu na kuwa kalenda ya Gregory – ya Nchi za Kimagharibi, lazima azingatie tofauti ya miaka 622 kabla ya Hijiriya. Zaidi ya hayo, mwaka wa mwandamo wa mwezi amba Kalenda ya Kiislamu ndio msingi wake, unazo siku 354 tu. Hivyo mwaka huu ni pungufu kwa siku 11 kuliko mwaka wa jua. Kila miaka mia moja ya jua inakuwa miaka 103 ya miaka inayohesabiwa kwa kuandama kwa mwezi. Miaka elfu moja ya jua ni sawa na miaka 1030 inayohesabiwa kwa mwandamo wa mwezi.

### QUR’ANI TUKUFU


#### AMIIINI (Sheikh Hussein Ahmad Al-Amiin)

*Al-Ghadiir* (Tangazo lililosimuliwa la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu Imam Ali hapo Ghadiir Khum), chapa ya pili ilifanywa na Al-Haidari Printing Tehran, 1372 Hijiriya. Al-Amiin ni mwandishi wa historia maarufu wa zama za leo.

#### ASKARI (Sayyid Murtadha Al-Askari)

*Abdallah ibn Saba*, chapa ya pili ilifanywa na Matabi-a Al-Kitab Al-Arabi mjini Cairo, 1381 A.H. Al-Askari ni mwandishi wa historia na theolojia wa zama za leo.

ATHIIR (Ali Ibn Muhammad Al-Shaibani, ajulikanaye kama Ibn al-Athiir)  
*Al-Kamil* (kilicho kamilika), kitabu maarufu cha historia ya Uislamu, kili-



## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

chochapishwa na Al-Azhari Printings 1301 Hijiriya. Pia kimepigwa chapa na Dar-Al-Kitab Al-Lubnani (*The Lebanese House of Books*), 1973 Baada ya kuzaliwa Isa. Nukuu zilizomo humu nyingi zinatoka kwenye chapa ya pili. Ibn Al-Athiir alikufa mwaka wa 750 Hijiriya.

**BALADHURI.** (AL-Baladhuri).

*Ansabul-Ashraf* (Nasaba za Masharifu). Kitabu maarufu cha historia ya Uislamu, kimechapishwa Jerusalem. Al-Baladhuri, ni mwandishi mashuhuri wa historia, alikufa mwaka wa 279 Hijiriya.

**BIRR** (Yusuf Ibn Abdul-Birr)

Al-Istii'ab Fi Maarifat al-Ass'hab (Elimu linganishi kuhusu Masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kitabu maarufu cha historia ya Kiislamu, kimechapishwa na Al-Fajjala Printing, Cairo, mwaka wa 1970 AD. Ibn Abdul-Birr ni mwandishi wa historia maarufu, alikufa mwaka wa 463 Hijiriya.


**BUKHARI** (Muhammad Ibn Isma'il, al-Bukhari).

*Sahih al-Bukhari* (Sahih ya Al-Bukhari), mojawapo ya vitabu sita vilivyo Sahihi vyenye Hadith zilizoandikwa (Hadith ni tamko lililosimuliwa au tendo au uthibitisho wa kimya wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Muhamamd s.a.w.w) Kitabu kilichapishwa na Muhammad Ali Subh huko Al-Azhar, Cairo, Al-Bukhari ni mchaguzi na mwandishi wa Hadith mashuhuri, alikufa mwaka wa 256 Hijiriya.

**DAWUD** (Suleiman Ibn Al-Ash'ath Ibn Shaddad anayejulikana kama Abu-Dawood)

*Sunan Abu Dawood* (Hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilizoandika). Mojawapo ya vitabu sita vya hadith zilizoandikwa, kilichochapishwa na Mustafa Al-Babi al-Halabi – Misri, mwaka 1952 AD. Abu Dawood ni mkusanyaji na mwandishi wa Hadith mashuhuri alikufa mwaka 275 Hijiriya.

**FAIRUZABADI** (Sayyid Murtadha Al-Fairuzabadi).



## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

*Fadha-il Al-Khamsah Min As-Sihah Al-Sitta* (Fadhila za watu watano, zili zoandikwa kwenye vitabu Sahihi Sita), chapa ya tatu ilifanywa na Al-Alami Institute of Printing, Beirut, mwaka 1973 AD, Al-Fairuzabadi ni mkusanyaji wa Hadith, mwanatheolojia na mwandishi wa Hadith wa zama za leo.

HADIID (Izzud-Din, ajulikanaye kama Ibn Abil-Hadiid).

*Sharh Nahjul-Balaghah* (Maelezo kuhusu Njia ya Ufasaha wa maneno yaliyokusanywa ya Imam Ali), kitabu kinachosomwa kwa wingi sana. Kimechapishwa na Dar Al-Kutub Al-Arabiyyah Al-Kubrah (Nyumba Kubwa ya Vitabu vya Kiarabu), ya Mustafa Al-Babi, Cairo, Ibn Abil-Hadiid ni mwanatheolojia na mwandishi wa historia maarufu, alikufa mwaka 655 Hijiriya.

HAIKAL (Dk. Muhammad Husein Haikal)

*Hayat Muhammad* (Maisha ya Muhammad),


Chapa ya tatu iliyofanywa na Dar Al-Kutub Al-Misriyah (The Egyptian House of Books) Cairo, mwaka 1358 Hijiriya. Dr. Haikal ni mwandishi wa historia wa zama za leo.

HAKIIM (Sayyid Muhammad Taqi Al-Hakim)

*Al-Madkhal Ila Darasat Al-Fiqh Al-Muqaran* (Utangulizi kuelekea kwenye masomo ya Fiqhi linganishi) kilichapishwa na Dar Al-Andalus, Beirut. 1963 AD. Hakiim ni mwanatheolojia wa zama za leo.

AL-HAKIM. (Muhammad Ibn Abdullah Al-Nissaburi, ajulikanaye kama Al-Hakim).

*Al-Mustadrak Alas-Sahihain* (Hadithi ambazo sahihi za Al-Bukhari na Muslaim imziacha). Hadith zilizomo kwenye kitabu hiki zinachukuliwa kuwa za kweli na wanachuoni Waislamu, isipokuwa zikataliwe na Al-Dhababi, ambaye maoni yake yamechapwa pembezoni mwa kitabu cha *Al-Mustadrak*, kilichochapishwa na Al-Nasr Printing, Riyadh Saudia Arabia, mwaka 1335 Hijiriya. Al-Hakim ni mwanachuo, mwandishi wa Hadith na mkusanyaji wa Hadith maarufu, alikufa mwaka 405 Hijiriya.



## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

HALABI (Ali Ibn Burhanud-Diin Al-Halabi)

*Al-Siirah Al-Halabiyyah* (Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulioandikwa na Al-Halabi), kilichochapishwa na Al-Maktaba Al-Kubra ya Mustafa Muhammad, Cairo, Al-Halabi ni mwandishi wa historia maarufu, alikufa mwaka 1044 Hijiriya.

HANBAL (Ahmad Ibn Hanbal)

*Musnad Ahmad*, kilichochapishwa na as-Sader Printing, Beirut, mwaka 1969AD. Ibn Hanbal ni mmojawapo wa maimam wa matapo ya Kiislamu, alikufa mwaka 241 Hijiriya.

HISHAMU (Abdul Malik Ibn Hisham)

*Al-Siirah Al-Nabawiyah* (Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kilichochapishwa na Mustafa Al-Babi Al-Halabi, Misri, mwaka 1955 AD. Ibn Hisham ni mwandishi maarufu wa historia ya Kiislamu, alikufa mwaka 281 Hijiriya.

HUSEIN (Dk. Taha Husein)

*Al-Fitnat Al-Kubra* (Mgogoro wa Fitna Kubwa katika dini), Kilichapishwa na Dar Al-Maarif, Misri mwaka 1953 AD. Taha Husein ni mwanachuo na mwandishi wa historia wa zama hizi.

JALALAIN (Jalalud-Din Muhammad Al-Halabi na Julalud-Din As-Suyuti)


*Tafsiirul-Jalalain* (Tafsiri za *Jalal* mbili kuhusu Qur'ani Tukufu)

KHALID (Muhammad Khalid)

*Fi Rihab Ali* (kwenye nyumba ya wageni ya Ali), Khalid ni mwandishi na mwanahistoria wa Misri wa zama za leo.

MAJAH (Muhammad Ibn Majah)

*Sunnan Ibn Majah* (Hadith zilizokusanywa na Ibn Majah). Mojawapo ya vitabu sita viliyvo sahih vya Hadith kilichochapishwa na Dar Ihya Al-Kutub Al-Arabiyyah (Nyumba ya Uhuishaji wa Vitabu vya Kiarabu) ya Isa Al-Babi, Cairo, 1952 AD. Ibn Majah ni mkusanyaji na mwandishi wa



Hadith maarufu, alikufa mwaka 275 Hijiriya.

**MAQSOUD** (Abdul Fattah Abdul-Maqsooud)

*Al-Imam Ali Ibn Abi Talib* (kitabu cha historia ya Imam Ali), kimechapishwa na Al-Irfan Printing, Beirut, Abdul-Maqsooud ni mwandishi na mwanahistoria wa Misri wa zama za leo.

**MUGHNIYAH** (Sheikh Muhammad Jawad Mughniyah).

*Hadhi Hiya Al-Wahhabiyah* (Huu ndio Uwahabbi), Sheikh Mughniyah ni mwanatheolojia maarufu wa zama za leo.

**MUHSIN** (Sayyed Muhsin Al-Amiin)

*Aayan Al-Shi'ah*, kitabu chenyeh maelezo mengi kilichopangwa kwa alfabeti. Sayyid Muhsin ni mwanatheolojia na mwandishi wa historia maarufu wa zama za leo.

**MUSLIM** (Ibn Al-Hajjaj Al-Qusheiri)

*Sahih Muslim* (Ukweli na usahihi wa Muslim). Ni kimojawapo cha Vitabu sahihi sita vya Hadith kilichochapishwa na Muhammad Ali Subh Printing, Misri, mwaka 1349 Hijiriya. Muslim ni mkusanyaji na mwandishi wa Hadith maarufu sana, alikufa mwaka 365 Hijiriya.

**MUTTAQI** (Ali Ibn Hussamul-Diin Al-Hindi Al-Muttaqi)


*Kanzul-Ummal* (Hazina ya waja wa Mwenyezi Mungu), mkusanyiko mkubwa wa hadith. Hadith zilizomo kwenye kitabu hiki zimebekwa katika mfululizo.

**MUTTAQI** (Ali Ibn Hussamul-Diin Al-Hindi Al-Muttaqi)

*Muntakhab Kanzul-Ummal* (hadith zilizoteuliwa kutoka kwenye *Kanzul-Ummal*) zilizochapishwa pembezoni mwa *Musnad Ibn Hanbal*, na as-Sader Printing, Beirut. Al-Muttaqi ni mkusanyaji na mwandishi maarufu wa hadith ambaye aliishi mnamo Karne ya Kumi na Moja, Hijiriya.

**NISABUURI** (Ali-Hasan Ibn Ahmad Al-Nisabuuri)

*Gharaibul - Qur'ani* (fasili juu ya Qur'ani Tukufu) zimechapishwa pembezoni mwa *Jami-ul-Bayan* ya Al-Tabari (fasili zingine na Al-Tabari) na



Al-Matba-ah Al-Meimaneyah, Misri, 1321 Hijiriya. Al-Nasabuuri ni mfasili wa Qur'ani tukufu, alikufa wakati wa karne ya nane Hijiriya.

**NISA'I (Ahmad Ibn Shu'aib Al-Nisa'i)**

*Sunnan Al-Nisa'i* (Hadith zilizokusanywa na Al-Nisai), kutoka kwenye Vitabu Sita Sahihi vya hadith vilivypigwa chapa na Al-Matba-ah Al-Meimaneyah, Misri, 1321 Hijiriya. Al-Nisa-i ni mteuzi na mkusanyaji wa hadith maarufu, alikufa 303 Hijiriya.

**RAYYAH (Mahmood Abu Rayyah)**

*Adhwa-a Ala Al-Sunnah Al-Muhamadiyah* (miale juu ya hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilizosimuliwa) chapa ya tatu imefanywa na Dar Al-Maarif (Nyumba ya Maarifa), Misri, 1957 AD. Abu Rayyah ni mwandishi maarufu wa zama za leo.

**RAZZI (Fakhrud-Diin Muhammad Ar-Razzi)**

*At-Tafsir Al-Kabiir* (Tafsiri pana za Qur'ani Tukufu) chapa ya pili imefanywa na Al-Matba-ah Al-Sarafiyyah, mwaka 1304 Hijiriya. Ar-Razzi ni mwanatheolojia na mfasili wa Qur'ani Tukufu maarufu sana, alikufa mwaka 606 Hijiriya.

**SAAD (Muhammad Ibn Saad Al-Zuhri, ajulikanaye kama Ibn Saad)**


*Al-Tabaqat Al-Kubra* (kitabu maarufu cha historia ya masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wanafunzi wao), kilichapishwa na Dar as-Sader, Beirut mwaka 1960 AD. Ibn Saad ni mtaalamu wa Historia ya Kiislamu maarufu, alizaliwa mwaka wa 168 Hijiriya.

**SHALTUTE (Sheikh Mahmood Shaltute)**

*Tafsir Al-Qur'ani* (Tafsiri za Qur'ani Tukufu), kimechapishwa na Dar-Al-Qalam Printing, mwaka 1960 AD. Sheikh Shaltute ni Sheikh maarufu miongoni mwa masheikh wa Al-Azhar).

**SHARAFUD-DIIN (Sayyid Abdul Husein Sharafud-Diin).**

*Al-Muraj'at* (Majadiliano) kilichapishwa na Al-Irfan, Saida, Lebanon, mwaka 1936 AD. Sayyid Sharafud-Din ni mwanatheolojia na mwandishi wa historia maarufu wa zama za leo.



### SHABLANJI (Mumin Ibn Hussam Al-Shablanji)

*Nurul-Absar* (Nuru ya Macho), chapa ya nane ilifanywa na Atif, mwaka 1973. AD, Misri. Al-Shablanji ni mkusanyaji maarufu wa Hadith, alizaliwa mwaka 1251 Hijiriya.

### TABARI (Muhammad Ibn Jariir Al-Tabari)

*History of Messengers and Kings* (Historia ya Mitume na Wafalme). Al-Tabari ni mwandishi wa historia, mwanatheolojia na mfasili wa Qur'ani Tukufu maarufu, alikufa 310 Hijiriya. Nukuu zote katika Jz. 2, ambazo zilichukuliwa kutoka kwenye historia ya Tabari, zilichukuliwa kutoka Jz. 4, chapa ya 4, na Jz. 5, chapa ya 2, iliyochapishwa na Dar Al-Ma'arif ya Misri.

### TABARI (Muhammad Ibn Jariir Al-Tabari)

*Jami-ul-Bayan* (Ubainifu Mkubwa), Tafsiri ya Qur'ani Tukufu, kilichapishwa na Maimaneyah Printing, Misri, mwaka 1321 Hijiriya.

### TABARSI (Ahmad Ibn Ali Ibn Abi Talib At-Tabarsi)

*Al-Ihtijaji* (mazungumzo) kilichapishwa na Al-Naaman Printing, Al-Najaf, Iraq, 1966 AD. At-Tabarsi ni mwanatheolojia maarufu aliyeishi katika karne ya sita Hijiriya.

### TIR MIDHI (Muhammad Ibn Isa At-Tirmidhi)


*Sunan At-Tirmidhi* mojawapo ya vitabu Sita Sahih vya Hadith. Sehemu ya tano ilichapishwa na Al-Fajjalah Printing, Cairo, 1967AD. At-Tirmidh ni mteuzi na mwandishi wa hadith maarufu, alikufa 279 Hijiriya.

### WAQIDI (Muhammad Al-Waqidi)

*Al-Maghazi* (uvamizi), kilichapishwa na Oxford Printing. Al-Waqid ni mtaalam wa historia Mwislamu maarufu, alikufa mwaka 207 Hijiriya.

### ZUHRAH (Sheikh Muhammad Abu Zuhrah)

*Al-Imam As-Sadiq*, kilichapishwa na Dar Al-Fikr Ak-Arabi (Nyumba ya Fikra za Kiarabu zilizoandikwa) Misri. Sheikh Abu Zuhrah ni mwanatheolojia na mwandishi wa historia wa zama za leo.



## UTANGULIZI

Imam Ali Foundation ilianzishwa kama chama cha kutoa msaada chenye lengo na madhumuni ya kueneza mafundisho ya Uislamu asilia kama ulivyo hubiriwa mwanzo na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kama ulivy-ofafanuliwa na Ahlul-Bait watukufu, watu wa nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na uzao wake.


Kitabu hiki '**Ndugu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)**' ni mojawapo ya vitabu vizuri vilivyoandikwa na marehemu Muhammad Jawad Chirri. Alifafanua historia ya maisha ya Imam Ali (a.s) na akachanganua masuala mbali mbali muhimu ya maisha yake, ama wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au baada ya kifo chake.

Imam Ali (a.s) Foundation ilikiona kitabu hiki kuwa na mvuto na manufaa kwa wasomaji wa Kiingereza hususan ambapo inafahamika kwamba vitabu vichache sana vimeandikwa kuhusu Imam Ali (a.s) kwa lugha ya Kiingereza. Tumepata ari ya kukichapisha tena kitabu hiki kama faida ya Waislamu kwa ujumla na pia wasio Waislamu amba wanataka kujifunza historia ya maisha ya mtu wa pili kwa umashuhuri kwenye Uislamu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Toleo la kwanza la kitabu hiki lilikuwa na juzuuy mbili zilizo tenganishwa. Ili kurahisisha zaidi namna ya kushika na kusoma, tulipendelea kukichapisha katika juzuuy moja.

Imam Ali (a.s) Foundation inakaribisha maoni yako kuhusu yale yaliyomo kwenye kitabu hiki. Kama unataka maelezo zaidi, tafadhali tuandikie.

**Imam Ali (a.s) Foundation.  
18<sup>th</sup> Dhulhija, 1418/16<sup>th</sup> April, 1998.**





## KUHUSU MWANDISHI.

Imam Muhammad Jawad Chirri ni mzalendo wa Lebanon na ni mhitimu (*Graduate*) wa taasisi ya kidini iliyo maarufu ya Najaf nchini Iraq. Yeye ni mwanatheolojia ya Kiislamu, mhadhiri mwandishi na mwanahistoria. Ni mwendeshaji wa kipindi cha redio cha kila wiki kitiwacho '*Islam in Focus*' kinachotangazwa na WNIC. Katika vitabu vyake viliyvo chapishwa ni:

*Muslim Practice.*

*Islamic Teaching*

*Imam Husein, Leader of the Marteyrs.*

*Inquiries About Islam* (Maelfu ya maktaba za Marekani wamekitwaa kitabu hiki - Kitabu hiki pia kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Taasisi ya Al-Itrah Foundation, kwa jina la "***Maswali kuhusu Uislamu***"). '*Al-Khilafatu Fi Al-Dustous Al –Islam*' (The Calphate in the Islam constitution- Arabic).

*Amiir Al-Muminiin* (The leader of Belivers –Arabic).



Imam Chirri alialikwa na Detroit Muslim Community awe kiongozi wao wa kiroho. Alisaidia sana katika ujenzi wa *Islamic Center of Detroit*, mojawapo ya taasisi kubwa sana za Kiislamu - America ya kaskazini. Sasa hivi yeye ndiye Mkurugenzi wa Taasisi hii.

Kazi ya Imam Chirri ilipanuliwa hadi Afrika ya Magharibi. Alipokuwa katika msafara wa kuhadhiri mnamo mwaka 1958, aliweza kuishawishi jamii ya Kilebanoni iliyoko Sierra Leone kujenga hospitali ya watoto kama zawadi kwa wazalendo wa nchi hiyo.

Wakati alipotembelea Mashariki ya kati mwaka wa 1959, mwandishi huyu alilishughulikia tatizo la Kiislamu la siku nyingi na kufaulu kupata ufumbuzi wake. Kwa kipindi cha miaka elfu moja, Waislamu walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili; Sunni na Shi'ah (wala hakuna hata upande moja baina ya hizo pande mbili uliotambua uthabiti wa mafundisho ya kundi lingine licha ya makubaliano ya matapo yote mawili kuhusu mafundisho yote ya Qur'an Tukufu na hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilizosimuliwa kwa usahhihi.

Mwandishi huyu alikutana na marehemu Sheikh mkuu wa Al-Azhar, Sheikh Mahood Shaltut mnamo tarehe 1, Julai, 1959. Alizungumza naye kuhusu suala hilo muhimu. Katika hitimisho la mazungumzo Sheikh Shaltut alikubali uthabiti wa Tapo la Kiislamu la Shia Jaafariya. Mwandishi huyu alimwomba Sheikh kutangaza usawa baina ya tapo la Shia Jaafariya na Sunni. Tangazo (*fatwa*) hilo lilirushwa hewani na kuchapishwa Julai 7, 1959. Tamko hili lilikuwa la kihistoria na la kwanza la namna yake tangu matapo hayo yalipotengana.

Moyo wa udugu wa kweli wa Kiislamu unaweza kuwepo tu kwa uelewano wa pande zote mionganini mwa matapo mbali mbali ya Kiislamu. Ni kwa mtazamo huu kwamba Mwandishi anawasilisha kitabu hiki, '**Ndugu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)**' Bila kuwa na haja ya kusema kwamba mabishano mionganini mwa matapo mbali mbali ya Kiislamu yanazunguka hasa zaidi kwenye historia ya Imam huyu mashuhuri. Ufahamu wa kweli na wa hakika wa nafasi yake katika Uislamu utawafanya Waislamu waelekee kwenye undugu wa kweli zaidi.





## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

# SURA YA KUMI NA SITA

**IMAM WAKATI WA ENZI YA MAKHALIFA WATATU.**

### **Abu Bakr Anachukua Urithi**

Hatimaye, lile lisiloepukika likaja kutokea. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akatawafu, na kifo chake kilikuwa hasara kubwa kuzidi kiasi ambayo hajapata kumkumba mwanadamu. Wahyi wa Mbinguni kwa watu wa duniani ulikoma. Alikuwa ni Mwisho wa Mitume, na hapana Mtume mwingine atakayekuja baada yake.

Waislamu walilemewa sana kwa kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hivyo kwamba ilikuwa vigumu kwa sahaba yejote maarufu kufikiria.

### **Umar Alikana Kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Umar alisimama msikitini, akasema: “Baadhi ya wanafiki wanadai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametawafu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hajatawafu. Yeye alikwenda tu kwa Mola wake Mlezi kama Nabii Musa mwana wa Imr?n alivyokwenda kwa Mola Wake. Aliwaacha watu wake kwa siku arobaini, halafu akarudi kwao baada ya kusemekana kuwa alikuwa. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atarudi kama alivyorudi Musa (a.s.). Atakata mikono na miguu ya watu wanaodai kuwa amekufa.”<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Ibn Hishamu, kwenye kitabu chake cha ‘Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),’ sehemu ya 2, uk. 655.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### KHUTBA YA ABU BAKR.

Abu Bakr alikuwa mkweli zaidi na mwenye akili iliyotulia vizuri kuliko Umar. Alisimama na akasema: "Enyi watu, yeyote aliyekuwa anamuabudu Muhammad sharti ajue kwamba Muhammad amekufa. Yeyote aliyekuwa anamuabudu Mwenyezi Mungu ajue kwamba Mwenyezi Mungu yupo na kamwe hata kufa." Halafu akakariri Aya ifuatayo:

﴿ وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ حَلَّتْ مِنْ قَبْلِهِ الْرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبُوهُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَنْ يُضْرِبَ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ أَلْشَكَرِينَ ﴾

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume. Je akifa au akauawa ndio mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru Mwenyezi Mungu hata kidogo. Na Mwenyezi Mungu Atawalipa wanaoshukuru."

(Qur'ani Tukufu 3:144).

Aliposikia maneno haya Umar alitambua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikwishatawafu na akaanguka chini.

### KUSHUGHULISHWA NA MAZIKO MATAKATIFU.

Uzito wa msiba huu wa kuvunja nguvu, aliyeuhisi zaidi si mwengine isipokuwa Ali na watu wengine wa nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kiliwafanya wakose fahamu ya mambo mengine hapa duniani. Huzuni ya familia hii iliyoondokewa ilikuwa haielezeki kabisa. Walitamani kutoweka duniani hapa pale alipoondoka Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliongea kwa siri na binti yake Fatima Az-Zahra mara mbili wakati anaugua. Wakati mmoja alimjulisha juu ya kifo chake, akalia sana. Kisha alimfahamisha kwamba yeye atakuwa mtu wa kwanza wa familia yake kumfuata yeye, na alicheka. Alifurahi Fatima kujua kwamba hataachanishwa naye kwa muda mrefu.

Mume wake Fatima, Ali (a.s.) aliishi miaka ishirini na tatu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akijitolea maisha yake kwa ajili ya kumlinda yeye (s.a.w.w.) dhidi ya hatari. Ghafla akaona kwamba maisha hayo ya thamani yalikoma ambapo hakuwa na uwezo wa kuyakomboa. Kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kilimuumma sana Ali kuliko kama angekufa yeye mwenyewe.

### KONGAMANO LA KISIASA.

Hata hivyo, msiba haukuwazuia masahaba wengine, wa kutoka Makka na wa Madina kufikiri na kufanya kisiasa kabla hata ya kuzikwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Kama ilivyodokezwa huko nyuma, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijaribu lakini hakuandika wasia, ambamo alitarajiwa kumtaja mrithi. Alijaribu kumtaja mtu ambaye uongozi wake ungeleta usalama kwa umma dhidi ya kukengeuka. Kundi la masahaba likiongozwa na Umar, lilikataa kuandikwa wasia huo, na mbinu ya kukataa kwao ilifanya hati hiyo iliyopendekezwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kukosa maana.

Tangazo la Ghadiir Khum na matamshi mengine ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mahali mbali mbali kuhusu Ali yalidharauliwa. Kinachoweza kusemwa kwa usahihi zaidi kuhusu msimamo wa masahaba kuhusu usemi huo ni kwamba hawakuona ushahidi wa kulazimisha kuhusu uteuzi wa Ali. Watu wa Makka na Madina, walianza na kumaliza mashindano yao ya uongozi kabla Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hajazikwa.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UMAR ALIZUNGUMZIA KUHUSU KONGAMANO.

Umar, wakati wa mwaka wa mwisho wa utawala wake, alizungumza kuhusu kilichotokea baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Aliwataarifu wasikilizaji wake kwamba alipokufa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), watu wa Madina wakiongozwa na Sad Ibn Ubadah walijitenga na watu wa Makka, na watu wao mashuhuri walikutana huko Saqifah Banu Saidah, wakajaribu kuchagua Khalifa kutoka mionganini mwao. Ali Ibn Abu Talib, Zubeir Ibn Al-Awam na wengine waliokuwa pamoja nao wakajiepusha nao, na watu wa Makka walikwenda na Abu Bakr.

Abu Bakr, Umar na Abu Ubeidah Ibn Al-Jarah, walikwenda kwenye kongamano la watu wa Madina kisitisha jaribio lao. Abu Bakr aliwaambia watu hao wa Madina kwamba Waarabu hawangemkubali kiongozi wa koo nyingine isipokuwa koo za Qureishi (watu wa Makka) ambao walikuwa mashuhuri zaidi mionganini mwa Waarabu na kutoka kwenye jiji lenye hadhi kubwa sana. Inasemekena kwamba Abu Bakr aliwaambia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wakati fulani alitangaza kwamba Maimam wanatoka kwa Maquraishi.<sup>2</sup> “Mimi ninaridhika, aliwaambia, na uongozi wa yejote wa hawa watu wawili (Umar na Abu Ubeidah). Mpeni kiapo cha utii yejote kati ya hawa watu wawili ambaye mtamchagua.” Baadhi ya watu wa Madina walishauri kiongozi atoke upande wao na mwingine atoke upande wa watu wa Makka. Mabishano yalikuwa makali na Umar akamwambia Abu Bakr: “Nyoosha mkono wako.” Abu Bakr alifanya hivyo na Umar akampa mkono kutoa kiapo cha utii kwake. Watu wa Makka waliokuwa hapo nao pia walitoa kiapo cha utii na watu wa Madina waliokuwa wanashauriana walifanya hivyo, isipokuwa Saad Ibn Ubadah na watu wanaomuunga mkono.

<sup>2</sup> Dr. Taha Husain, *Al-Fitnatul-Kubra* sehemu ya 1, uk. 35.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Siku iliyofuata, watu walikusanyika msikitini. Umar alisimama na akawaambia wasikilizaji: “Mwenyezi Mungu amewezesha nyinyi kukubali kadiri ya uwezo wenu wote, sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa pamoja naye kwenye pango (Lu Thour wakati wa Hijiriyah). Simameni mtoe kiapo cha utii kwake.”<sup>3</sup> Na walifanya hivyo.

### MASWALI YA KISHARIA NA KIHISTORIA.

Urithi wa Abu Bakr unasababisha maswali haya:

Je! Abu Bakr aliwahi hata kidogo kudai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya yeye mrithi wake?

Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumteua yeye, alionesa dalili za kupendelea kumteua yeye?

Je! Uchaguzi wa Abu Bakr ulikuwa wa hatari kwa mtazamo wa Kiislamu? Hivi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: Maimam wanatoka kwa Maquraishi, na alimaanisha nini kusema hivyo?

Historia inatoa jibu la swali la kwanza kwa kukataa, kwani Abu Bakr kamwe hakudai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya yeye kuwa mrithi wake. Wala hapana sahaba yeoyote ambaye alifanya kazi kwa juhudini katika kuanzisha Ukhilifa wake alidiriki kudai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Abu Bakr mrithi wake. Msomaji unaweza kukumbuka kwamba mabishano ya Abu Bakr ambayo aliyaaanzisha kwenye mkuutano wa watu wa Madina hayakuwa na dokezo zozote za uteuzi wowote wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye aliuambia mkuutano kwamba Waarabu hawangetambua uongozi usiokuwa wa Maquraishi. Kwani Maquraishi, alisema, wanaheeshimiwa zaidi mionganoni mwa Waarabu na wanatoka

<sup>3</sup> Ibn Hishamu, kwenye kitabu chake cha Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sehemu ya 2, uk. 659-660.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kwenye jiji linaloheshimika sana. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angekuwa ameonesha utashi wake wa kumfanya yeye kuwa mrithi wake, Abu Bakr angefanya tamko la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa hoja yake pekee, bila kukimbilia kuwasifu Maquraishi. Pia Umar angenukuu tamko kama hilo kuegemeza hoja yake kuhusu kuchaguliwa kwa Abu Bakr.

Wanachuo wa Madhehebu ya Sunni wanakubaliana kwa pamoja kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kamwe hakumteua mrithi. Hii inamaanisha kwamba wanakubali kwamba hakumfanya Abu Bakr mrithi wake.

Hata hivyo, imesimuliwa kwamba mwanachuo wa zama za sasa wa Madina wa madhehebu ya Wahabi alidai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimteua Abu Bakr kama mrithi wake.<sup>4</sup> Aliegemeza madai yake kwenye hadith isemayo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema:

“Na Mwenyezi Mungu na waumini wanakataa (uongozi wowote) isipokuwa ule wa Abu Bakr.” Pia alidai kwamba hadith hii ni ‘*Mutawatir*’ (imesimuliwa na wahadithiaji wengi sana sifa inayofanya hadith hii kuwa ya kweli).

Hadith ni ile ambayo Muslim ameandika kwenye *Sahih* yake kuitia kwa msimulizi wake hadi kwa Urwah ambaye alisimulia kwamba Aisha alisema: “Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliniambia; ‘mwambie baba yako Abu Bakr aje hapa na kaka yako, ili niweze kuandika maelekezo. Nina hofu kwamba mwenye kutamani anaweza akatamani na msemaji anaweza akasema; Ninayo haki zaidi (ya uongozi kuliko Abu Bakr) na Mwenyezi Mungu na Waumini wanakataa (uongozi wowote) isipokuwa wa Abu Bakr.’”<sup>5</sup>

<sup>4</sup> Sheikh Muhammad Jawad Mugneyah aliandika hadith hii kwenye kitabu chake cha *Hadhihi Hiya Al-Wahabiya* (huu ndio Uwahabi).

<sup>5</sup> Muslim, *Sahih Muslim* sehemu ya 15, uk. 155.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Al-Bukhari aliandika hadith hii kwa namna inayofanana na hii lakini ilikuwa na neno: “Nusura nijaribu kumuita Abu Bakr na mtoto wake na niandike maelekezo ....”<sup>6</sup>

Inafaa kuzingatia kwamba hadith hii si *mutawatir* kama anavyodai huyu mwanachuo wa Madhehebu ya Wahabi, kwani hadith hii haikusimuliwa na masahaba wengi sana. Kwa kweli, ilisimuliwa na Aisha peke yake. Hata hivyo, kuionesha hadith hii kama uthibitisho wa kuteuliwa kwa Abu Bakr kama mrithi ni ushahidi wa kupungukiwa na ujuzi mkubwa wa hadith, kwani hadith hii inapingana na hadith tatu sahihi ambazo zimesimuliwa na Aisha mwenyewe;

## AISHA ALISIMULIA KINYUME

Muslim aliandika kupitia wahadithiaji wake hadi kwa Masrooq kwamba Aisha alisema: “Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuacha dinari au dirham, au kondoo au ngamia, wala hakuacha wasia wa kitu chochote.”<sup>7</sup>

Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angemteua Abu Bakr kama mrithi wake, Aisha hangesema; “Wala yeye (Mtunme) hakuandika wasia wa kitu chochote.” Kwani kama angekuwa amemteua Abu Bakr, angekuwa ameandika wasia wa kitu muhimu sana.

Muslim pia aliandika kupitia kwa wahadithiaji wake hadi kwa Al-Aswad Ibn Yaziid kwamba alisimulia kwamba watu walitaja mbele ya Aisha kwamba Ali alikuwa wasii wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Aisha akasema: “Wakati gani yeye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Ali wasii? Nilikuwa nimeuegemeza mgongo wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye kifua changu (au alisema paja langu). Aliitisha beseni, kisha akazirai

<sup>6</sup> Al-Nawawi kwenye fasili yake ya *Sahih Muslim* aliwasilisha hadith hii.

<sup>7</sup> Muslim, *Sahih Muslim*, Sehemu ya 11 (Kitabu cha Wasia), uk. 89.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kwenye mapaja yangu na sikudhani kwamba alikufa. Wakati gani alimfanya Ali kuwa wasii wake?”<sup>8</sup>

Hadith hii, inaelezea hadith nyingine ambamo Aisha alisema: “Wala hakuandika wasia wa kitu chochote.” Kwenye hadith zote mbili Aisha alikuwa anajaribu kukanusha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Ali wasii wake. Hii kwa jinsi inavyoonekana inaonesha kwamba fikira ya uwasi wa Abu Bakr haikuenezwa kwa watu. Kilichokuwa kimeenea kwa watu ni kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Ali kuwa wasii wake. Kwa hiyo, Aisha alikuwa anajaribu kukanusha kwa juhud kubwa.

Kama Aisha angekuwa amefikiria kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimteua Abu Bakr, angewaambia wale waliotaja jina la Ali kuhusu uwasi kwamba baba yake, na wala sio Ali, alikuwa ndiye wasii.

Muslim pia alisimulia kupitia wahadithiaji wake hadi kwa Abu Malikah kwamba alisimulia yafuatayo; “Nilimsikia Aisha, na aliulizwa: Je, kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angetaka kumteua mrithi, angemteua nani? Alisema; Abu Bakr, wakamwambia; Halafu angemteua nani baada ya Abu Bakr? Aisha alisema: Umar. Halafu akaulizwa: Angemteua nani baada ya Umar? Akasema; Abu Ubaidah Ibn Al-Jarrah. Halafu akaishia hapo.”<sup>9</sup>

Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angesema: “na Mwenyezi Mungu na Waumini wanakataa (uongozи wowote) isipokuwa wa Abi Bakr, angekataa hilo swali la kufikirika kuhusu uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wa mrithi. Kwani uteuzi ungekuwa jambo la kweli na si la dhana na Abu Bakr angekuwa ndiye mteule halisi hasa. Lakini Aisha alilichukua jambo hili kinadharia, kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakufanya tamko la aina hiyo kuhusu Abu Bakr.

<sup>8</sup> *Ibid.*

<sup>9</sup> *Ibid*, Sehemu ya 2, uk. 154.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### CHUKI YA DHAHIRI BILA SABABU

Chuki ya Aisha dhidi ya Ali inaonekana wazi kwenye hadith tatu zilizotajwa kwenye kurasa za nyuma. Kwenye hadith ya Abu Malikah Aisha alijaribu kutuambia kwamba Abu Ubaidah alikuwa anastahili kuwa Khalifa kuliko Ali. Hakuna mtu anayeunga mkono jambo hili, kwani Waislamu kwa pamoja wanakubali kwamba Ali alikuwa na daraja la juu zaidi na alikuwa kipenzi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zaidi ya Abu Ubaidah.

Kwenye hadith ya Al-Aswad Ibn Yaziid, Mama wa Waumini alijaribu kukanusha uwasii wa Ali bila ya uthibitisho wowote. Natukubaliane kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikufa wakati ameegemea kifua cha Aisha na kwamba hakumfanya Ali kuwa wasii wake wakati huo, tukio hili halikanushi uwasii wa Ali. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema hadharani mahali paitwapo Ghadiir Khum, kwa niaba ya Ali, aliwaambia maelfu ya mahujaji kwamba Ali alikuwa *Mawla* (Mlezi) wa walioamini na kwamba yu kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika kuwa na haki zaidi juu yao kuliko walivyo na haki kwao wao wenyewe.

Zaidi ya hayo, Umm Salamah alisimulia kile kinachopingana na madai ya Aisha. Al-Hakim, kuititia kwa wahadithiaji wake ambao ye ye na Al-Thahabi waliiona kuwa ni sahihi, alisimulia kwamba Umm Salamah (mke wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) alisema: "Kwa Yule ambaye kwa Jina lake mimi ninaapa, Ali alikuwa mtu wa mwisho kugusana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla hajatawafu. Tulimtembelea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla ya Adhuhuri na alikuwa anasema kwa kurudia rudia: "Ali amekwisha kuja?" Fatima alisema: "Inaonekana kama vile umemtuma kwenye kazi." Yeye (Umm Salamah) akasema: "Ali akaja, na nilidhani kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na jambo la kumwambia kwa faragha. Tuliondoka chumbani na tukaketi mlangoni, na mimi nilikuwa karibu zaidi na mlangano. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliinama kuelekea kwa Ali akiwa anamwambia siri kwa kusema kwa kunong'ona, halafu Mtukufu Mtume

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

(s.a.w.w.) akatawafu mnamo siku hiyo. Hivyo Ali alikuwa mtu wa mwisho kuwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hadi anakata roho.”<sup>10</sup>

### HADITH YA MAGHAFIIR

Aisha alikuwa na desturi ya kusimulia baadhi ya matukio ambayo hayaku-tokea kamwe, kama riwaya ingekidhi matamanio aliyoystaka mwenyewe. Hadith ya Maghafiir (utomvu mzito unaotoka kwenye miti maalum) inajulikana sana katika historia ya Kiislamu na imetajwa kwenye Qur’ani Tukufu Sura ya 66 iitwayo ‘Al-Tahriim.’ Yeye (Aisha) na Hafsa (binti ya Khalifa wa pili) walikula njama kwamba kila mmoja wao akiwa peke yake na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitakiwa amwambie Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Ninapata harufu ya Al-Maghafiir kutoka kwako,” ambapo wote wawili walijua kwamba huo ni uwongo.

Al-Bukhari aliandika kwenye *Sahih* yake kwamba Ubaid Ibn Umair alisimulia kwamba Aisha alisema: “Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na tabia ya kunywa asali nyumbani kwa Zainabu, Binti yake Juhsh (mke mwingine wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) na kukaa naye. Hafsa na mimi tukala njama ya kumwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atakapokuja kwa yejote mmoja wetu amwambie: Umekula Maghafiir. Ninahisi harufu ya Maghafiir” Akasema: Hapana; lakini nilikuwa ninakunywa asali nyumbani kwa Zainabu, na sitafanya hivyo tena. Na ninaapa kwamba hau-tamwambia yejote kuhusu tukio hili.”<sup>11</sup>

Aisha alimsaliti Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kutoa siri ambayo alimu-muru aifiche. Mwenyezi Mungu akamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) juu ya jambo hilo na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na hili lilimfanya akasirike. Sura *Al-Tahriim* iliteremshwa kwa ajili ya tukio hili. Yaliyomo humo ni haya yafuatayo:

<sup>10</sup> Al-Hakim, *al-Mustadrak*, Jz. 3, uk. 139

<sup>11</sup> *Sahih Bukhari*, Jz. 6, ‘Kitabu juu ya tafsiri ya Qur’ani.’ Iko kwenye tafsiri ya **Suratut-Tahriim**, uk. 194

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

﴿ وَإِذْ أَسْرَ الَّنَّبِيَّ إِلَى بَعْضِ أَرْوَاجِهِ حَدَّيْشَا فَلَمَّا نَبَأَتْ بِهِ وَأَظْهَرَهُ اللَّهُ عَلَيْهِ عَرَفَ بَعْضَهُ وَأَعْرَضَ عَنْ بَعْضٍ فَلَمَّا نَبَأَهَا بِهِ قَالَتْ مَنْ أَنْبَأَكَ هَذَا قَالَ نَبَأَنِي الْعَلِيمُ الْخَيْرُ إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَّتْ قُلُوبُكُمَا وَإِنْ تَظَاهِرَا عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَاهُ وَجَبَرِيلُ وَصَالِحُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَلِكَ طَهِيرُ ﴾

“Na Nabii alimwambia mmoja wa wake zake jambo la siri. Basi alipolitangaza yule mke, na Mwenyezi Mungu akamdhahirishia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alimjuvya sehemu na akaacha nyingine. Alipomwambia hayo huyo mke akasema; Nani aliyeqwambia haya? Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye khabari zote! “Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwishaelekea huko. na mkisaidiana dhidi yake (Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)), basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye kipenzi chake, na Jibril na waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia.” (*Qur’ani Tukufu*; 66:3-4)

Al-Bukhari pia alisimulia kupitia wahadithiaji wake hadi kwa Ubeid Ibn Hunein, kwamba alisema: Nilimsikia Ibn Abbas akisema: Nilikaa mwaka mzima nikijaribu kumuuliza Umar Ibn Al-Khattab kuhusu Aya fulani ya Qur’ani na nisingweza kuuliza kwa sababu ya khofu, hadi alipoondoka kwenda Hija na mimi nilikuwa naye. Tulipokuwa barabarani, tunarudi Madina, alichepuka kuelekea kwenye kichaka ili ajisitiri. Ibn Abbas akasema: Nilimngoeja hadi alipomaliza, halafu nilitembea naye. Nikasema: Ewe Amiri wa Waumini, ni nani hao wawili mionganoni mwa wake zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao walisaadiana dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Umar akasema: Hao ni Hafsa na Aisha.”<sup>12</sup>

<sup>12</sup> *Sahih Al-Bukhari*, sehemu ya 6, uk. 195.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UMAR ALIUONA UCHAGUZI KAMA NI “VURUGU”

Kama mtu yejote ataulizia kutaka ushahidi zaidi kuhusu ukweli kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumfanya Abu Bakr mrithi wake, tamko la Umar lifuatalo kuhusu uchaguzi wa Abu Bakr linatosha kuondoa shaka juu ya jambo hili kwa ukamilifu.

Al-Bukhari kwenye *Sahih yake*,<sup>13</sup> Ibn Hishamu kwenye kitabu chake cha Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),<sup>14</sup> na Imam Ahmad kwenye *Musnad yake*,<sup>15</sup> wameandika kwamba Umar alisema kwenye khutba yake aliyohutubia wakati wa mwaka wake wa mwisho wa ukhalifa wake:

“..... Nimepata taarifa kwamba mtu mmoja kutoka mionganini mwenu anasema; Kwa jina la Mwenyezi Mungu, endapo Umar anakufa nitamchagua fulani (mtu ambaye jina lake Umar hakutaka kulitaja). Mtu yejote naasijidanganye kwa kujisemea mwenyewe kwamba uchaguzi wa Abu Bakr ulikuwa ni ‘vurugu’ na ni jambo liliopita. Hakika uchaguzi wa Abu Bakr ulikuwa ‘vurugu’ (kitendo kilichofanywa haraka bila uangalifu ...)”

Jambo hili linaonesha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kamwe hakudhihirisha nia yake ya kumfanya Abu Bakr Khalifa wake. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angekuwa ameonesha nia kama hiyo au alisema alivyosimulia Aisha, uchaguzi wa Abu Bakr haungekuwa kitendo cha purukushani zaidi, kingekuwa kitendo kilichopangwa vizuri na Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume Wake (s.a.w.w.).

<sup>13</sup> Al-Bukhari, kwenye *Sahih yake*, sehemu ya 8, uk. 210

<sup>14</sup> Ibn Hishamu kwenye kitabu chake Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sehemu ya 2, uk. 658.

<sup>15</sup> Imam Ahmad kwenye *Musnad yake*, sehemu ya 1, uk. 55.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### TAMKO LA MWISHO LA UMAR

Hata hivyo, Khalifa wa Pili aliondoa wasiwasi wote baada ya kuchomwa kisu. Muslim katika *Sahih* yake,<sup>16</sup> na Ibn Saad kwenye *Al-Tabaqat*,<sup>17</sup> na Ibn Hisham kwenye kitabu chake cha Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),<sup>18</sup> waliandika kwamba Abdullah Ibn Umar alisema kwamba alimshauri baba yake kumtaja mrithi wake na Umar alisema: “Kama sikumtaja mrithi, basi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumtaja mrithi na kama nikamtaja mrithi, Abu Bakr alimtaja mrithi.”

Al-Bukhari kwenye *Sahih* yake aliandika kwamba Abdullah Ibn Umar alisema kwamba baba yake aliambiwa: “Kwa nini humtaji mrithi?” Akasema: “Kama nikamtaja mrithi mtu ambaye ni bora zaidi yangu, Abu Bakr alimtaja mrithi. na kama sikumtaja mrithi aliye bora zaidi yangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumtaja mrithi.”<sup>19</sup>

### JE! MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) ALITAKA KUMTEUA ABU BAKR KUWA MRITHI WAKE.

Matukio ya siku za mwisho za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalionesha kwa wazi kabisa kwamba urithi wa Abu Bakr haukuwepo katika fikira ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hakuna kinachothibitisha hilo kama ilivyokuwa kuhusu msafara wa kijeshi wa Usama. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Usama Ibn Zayd Ibn Harith kamanda mkuu wa jeshi na alitoa maelekezo ya kumuamuru avuke mipaka ya Al-Balqa na Al-Daroon nchini Palestina. Watu walijitayarisha na muhajirina wa mwanzo walijiunga na jeshi la Usama.<sup>20</sup>

<sup>16</sup> Muslim kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 12, uk. 206.

<sup>17</sup> Ibn Saad kwenye *at-Taqqat* yake, sehemu ya 3, uk. 342.

<sup>18</sup> Ibn Hisham kwenye kitabu chake Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sehemu ya 2, uk. 653

<sup>19</sup> Al-Bukhari kwenye *Sahih* yake sehemu ya 9, uk. 100.

<sup>20</sup> Ibn Hisham kwenye kitabu chake ‘Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),’ sehemu ya 2, uk. 642.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Kutoka kwenye matukio yanayo julikana sana ya historia kwenye msafara wa Usamahni haya yafuatayo:

Abu Bakr, Umar na wengine miongoni mwa muhajirina walikuwa kwenye jeshi la Usama.<sup>21</sup>

Ali Ibn Abu Talib hakuwemo kwenye jeshi hilo.

Inaonesha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakutaka Ali ashiriki kwenye vita zaidi baada ya kuanzishwa dola ya Kiislamu kwenye Rasi ya Arabia kama matokeo ya vita vya kujihami ambamo Ali alikuwa shujaa mkubwa. Hakumruhusu (au angalau hakumuagiza) Ali ashiriki vita vya Mutah ambapo alilipeleka jeshi la Waislamu chini ya uongozi wa Zayd Ibn Harith (baba yake Usama) kwenye mipaka ya Syria, ambako Zayd, Ja'far Ibn Abu Talib na Abdullah Ibn Rawahah walieuawa. Wala hakumruhusu Ali kuungana naye kwenye kampeni ya Tabuk. Aliamua kumweka Madina ili amrithi yeeye anapokuwa hayupo.

Misingi ya dola ya Kiislamu ilikwishaanzishwa na ilikuwa si muhimu kuyapeleka maisha ya Ali kwenye hatari zaidi. Kwa hiyo, hakumpeleka kwenye jeshi la Usama. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumpa uongozi wowote Ali kwenye vita vyovoyote. Yeye alikuwa mbeba bendera wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika vita vyote ambavyo viliongozwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe.<sup>22</sup> Na alikuwa kamanda Mkuu wa misafara yote ya kijeshi ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka Ali.

<sup>21</sup> Hadith hii imeandikwa na Ibn Al-Athiir kwenye *Al-Kamil* na Ibn Saad, *Al-Tabaqat*, sehemu ya 2, uk. 290, na Al-Dahlani, na Al-Tabari, kwenye kitabu chake cha ‘Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),’ (zote hizi zilihadithiwa na Sharraful-Diin kwenye *Al-Murajaat*).

<sup>22</sup> Ibn Saad, kwenye *Al-Tabaqat* yake sehemu ya 3, uk. 25, na Al-Hakim kwenye *Al-Mustadrak* yake sehemu ya 3, uk. 111.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Wasomaji wa historia ya Uislamu walijua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpa Abu Bakr na Umar ukamanda wa jeshi kwenye vita vyta Khaybar kwa muda wa siku mbili mfululizo. Wakati huo Ali alikuwa anaumwa ugonjwa wa kuvimba macho ambaa ulimzuia asishiriki kwenye vita. Macho yake yalipotibiwa na kuponywa kwa muujiza mnamo siku ya tatu, Ali akawa kamanda Mkuu na Masheikh wawili Abu Bakr na Umar na masahaba wengie wakawa chini ya uongozi wake.

Ibn Saad amesimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya Usama kamanda wa jeshi. Jumatano ilipofika, maradhi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalianza kumsumbuu, alikuwa na homa na kuumwa kichwa, siku ya Alhamisi Asubuhi alimpa bendera Usama. Usama alibeba bendera, halafu ye ye akampa Buraidah Al-Aslami na wakapiga kambi huko Al-Jurf. Masahaba wote mashuhuri wa kutoka Makka na Madina pamoja na Abu Bakr, Umar Ibn Al-Khattab, Abu Ubaidah Ibn Al-Jarrah na Saad Ibn Abu Waqqas walijiunga na jeshi la Usama.”<sup>23</sup>

3. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliugua baada ya kumpa Usama bendera. Jeshi lilikuwa bado karibu na Madina na bado lilikuwa halijaanza safari yake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alishangazwa na mwendo wa kujikongojja wa jeshi na kutokuwa tayari kwa wapiganaji kuondoka Madina. Kwa hiyo, alikwenda Msikitini mara mbili akiwa katika hali ya kuumwa na kuwaamuru waanze safari yao na kwa mwendo wa haraka. Alirudia agizo hili mara tatu kwenye khutuba moja.<sup>24</sup>

Alifanya yote haya ambapo anatambua ukaribu wa kifo chake. Utambuzi wa kifo chake umesimuliwa kwenye hadith zifuatazo:

Ibn Hisham aliandika kwamba Abu Muwaihibah alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikwenda naye kuzuru makaburi ya Al-Baqii

<sup>23</sup> Ibn Saad, *Al-Tabaqat*, sehemu ya 2, uk. 249.

<sup>24</sup> Ibn Saad, *Al-Tabaqat*, sehemu ya 2, uk. 248.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

usiku kabla ya kuanza kuugua. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisimama kwenye uwanja wa makaburi na kuwapa hongera wakazi wa humo kwa kuepushwa na migogoro ya kupima imani ya siku za usoni. Abu Muwaihibah alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: Abu Muwaihibah, nimepewa funguo za hazina za dunia hii na maisha milele ndani yake pamoja na Peponi. Nilipewa chaguo hilo baina ya hilo na kukutana na Mola wangu Mlezi na Pepo. Abu Muwaihibah akasema: Baba na mama wawe kafara ya kukukomboa wewe. Chukua funguo za hazina za dunia hii na za maisha ya mielele ndani yake, pamoja na Peponi. Akasema: Hapana, Abu Muwaihibah, nimechagua kukutana na Mola wangu Mlezi na Pepo.”<sup>25</sup>

Na alipoketi kwenye mimbari yake alihutubia ambapo alikuwa mgonjwa, yeze kwa mujibu wa Ibn Hisham alimaliza hutuba kwa kusema: Kwa hakika Mwenyezi Mungu amempa chaguo mmojawapo wa waja Wake (Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anasema hivi kuhusu yeze mwenyewe) baina ya dunia hii pamoja na Akhera, na kile alichonacho Mola Mlezi. Mja alichagua kile alichonacho Mola Mlezi (alichagua kukutana na Mola wake Mlezi).<sup>26</sup> Hivyo, alikuwa anawataarifu wasikilizaji wake kwamba alikuwa amekaribia kuondoka hapa duniani.

Muslim aliandika kwenye *Sahih* yake kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Binti yake Fatima alipokuwa anaumwa maradhi ambayo ndiyo yaliyomuua: “Jibril alikuwa na desturi ya kuititia Qur’ani Tukufu akiwa na mimi mara moja au mbili kwa mwaka na sasa ameipitia akiwa na mimi mara mbili.” Halafu akamwambia Binti yake: “Ninahisi kwamba kifo changu kiko karibuni, Mtii Mwenyezi Mungu na uwe mvumilivu, mimi ni mzazi wako mwema .....”<sup>27</sup>

<sup>25</sup> Ibnu Hishamu, ‘Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)’ sehemu ya 2, uk. 642.

<sup>26</sup> Ibnu Hishamu katika ‘Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)’ sehemu ya 2, uk. 649

<sup>27</sup> Muslim, kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 17, uk. 7.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Al-Bukhari kupitia wahadithiaji wake hadi kwa Aisha aliandika kwamba alisema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuita Fatima (a.s), akiwa anaugua maradhi yaliyomuua, na akamwambia jambo kwa siri, naye akalia: halafu akamwambia jambo jingine kwa siri na Fatima akacheka. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipomuuliza binti yake kuhusu jambo hilo, Fatima alisema: Alinitaarifu kwamba alitarajia kufa kwa ugonjwa huu alionao sasa, na mimi nikalia. Halafu akanitaarifu kwamba mimi nitakuwa mtu wa kwanza mionganoni mwa watu wa Nyumba yake kumfuata yeye, na nikacheka."<sup>28</sup>

Hadith zote hizi zinashuhudia kwamba alikuwa anatambua kwa ukamilifu ukaribu wa kifo chake. Endapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anataka kumteua Abu Bakr kuwa mrithi wake ambapo alikuwa anatambua ukaribu wa kifo chake, hangemuagiza kuondoka Madina haraka. Badala ya kumhamasisha Abu Bakr na wenzake kuondoka Madina, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angemzuia Abu Bakr kujunga kwenye msafara wa jeshi.

Kwa msafara wa Usama kufika Palestina, apigane na kurudi Madina ingechukua miezi miwili au zaidi, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa upande mwingine angekwisha tawafu siku chache baada ya jeshi kuondoka, na yeye mwenyewe alikuwa anatarajia kufa baada ya muda si mrefu. Hakumteua Abu Bakr kabla ya jeshi kuondoka. Hangemteua baada ya kurudi toka Palestina kwa sababu Abu Bakr hangeweza kumuona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akingali hai. Hangemteua Abu Bakr wakati hayupo Madina, kwani haingeingia akilini kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angeruhusu jiji lisiwe na Khalifa baada ya kifo chake kwa kipindi cha miezi miwili au zaidi ambapo alitambua hatari zilizokuwa zinatishia Madina na Dini ya Kiislamu.

Zaidi ya hayo, Abu Bakr angeweza kuuawa wakati akiwa kwenye mapambano ya kivita. Kifo cha Khalifa vitani wakati wa kipindi hicho cha hatari kingelielekeza umma wa Waislamu na Uislamu kwenye matokeo mabaya sana.

<sup>28</sup> Al-Bukhari, kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 7, uk. 12..

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Endapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angekuwa anataka kumteua Abu Bakr kuwa mrithi, hangemruhusu kuwemo kwenye jeshi hilo. Lakini ukweli ni kwamba kuchelewa kwa kuondoka kwa Abu Bakr na masahaba wengine ilikuwa kinyume na alivyotaka Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na aliwadhi-hirishia wazi. Alisisitiza sana watekeleze msafara wa Usama, na kurudia misisitizo huo mara kadhaa alipokuwa kwenye mimbari na kwenye kitanda chake.

Hivyo, Abu Bakr, licha ya kuwa na nafasi ya juu na mapenzi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) juu yake, hakukusudiwa na Mtukufu Mtume kuwa mrithi wake.

\* \* \* \* \*

### JE! KUCHAGULIWA KWA ABU BAKR KULIKUWA NI HALALI?

Waislamu walikuwa na haki ya kumchagua Abu Bakr kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuchagua mtu mwagine kumrithi yeye. Na Abu Bakr alikuwa na haki ya kukubali uchaguzi. Uchaguzi kama huo unafanyiza mkataba ambao unalazimisha kutoka pande zote mbili utimilifu wake kwa mujibu wa masharti ambayo uchaguzi huo ulitegemezwa. Pale ambapo masharti ya uchaguzi yanamtaka mtu aliyechaguliwa kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kwamba mpiga kura anatakiwa amheshimu mteule katika kile kinachofikiriwa kuwa utii kwa Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Wake, uchaguzi ungekuwa mkamilifu na wa kuwajibisha pande zote.

Hata hivyo, uchaguzi kama huo, licha ya kuwa ni halali, ulikuwa na pande mbili zinazohasi:

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

**Haki ya kutokubaliana na walio wengi.** Kwa kuwa urithi wa Abu Bakr ulipatikana kwa kura ya walio wengi na si kwa uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Mwislamu mwema angekataa kuungana na waliomchagua bila kutenda dhambi. Kila Mwislamu anastahili kuwa na uhuru wa kisiasa, na hapana yejote ambaye ana haki ya kumlazimisha yejote kufanya asilolitaka, au kumbambikiza kwake sharti ambalo halikutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtu asilazimishwe kumchagua mtu ambaye hataki kumpa mamla-ka.

Ni ukweli huo huo kwamba wachache hawana haki ya kuwapinga walio wengi katika kuendesha mambo ya nchi alimuradi yapo makubaliano kama hayo, kwamba walio wengi ndio wenye haki ya kuendesha nchi. Hata kukiwa hakuna makubaliano kama hayo, walio wengi wanayo haki ya kuendesha nchi. Hii ni kwa sababu wachache hawana haki ya kuendesha mambo ya walio wengi, na endapo walio wengi wanawekewa pingamizi na wachache, nchi lazima itaangamia.

Kwa kuwa kila mtu binafsi anayo haki kutokubaliana na walio wengi ingekuwa ni dhuluma kwa upande wa walio wengi kuwalazimisha walio wachache kukubaliana nao. Kwa hili, tunafikiri ilikuwa ni dhuluma kumlazimisha Zubeir Ibn Al-Awwam kumchagua Abu Bakr, ijapokuwa alikuwa na sifa za kustahili kuwa kiongozi. Abu Bakr hakuteuliwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.) na kukataa kwa Zubeir kumchagua yejye hakukuleta uvunjaji wa amri ya Mwenyezi Mungu. Abu Bakr na masahaba walio wengi waliingia kwenye mkataba, na Zubeir alikuwa na haki ya kutokuafiki mkataba huo. Kumlazimisha aingie kwenye mkataba kama huo ilikuwa ni kuingilia haki zake.

Ilikuwa ni kitendo cha kutomtendea haki Ali kujaribu kumlazimisha kuungana na wapiga kura baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kumtangaza yejye kuwa *Mawla* (Mlezi) wa kila Mwislamu, pamoja na Abu Bakr. Haki ya mtu binafsi au walio wachache kutokubaliana na walio wengi ni ya kuheshimiwa na ya kuangaliwa katika chaguzi zote za kidemokrasia. Pale ambapo

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wagombea zaidi ya mmoja hushindana kwa nafasi ya juu, na mmojawapo wa wateule anapata kura nyingi, walio wengi hawafanyi jaribio la kuwalazimisha wapiga kura kumchagua aliyeshindwa kuungana nao wamchague mshindi. Hata hivyo kwenye umma wenyewe chama kimoja, ambapo serikali huwataka watu wapige kura ya ndio au hapana matokeo yanapoju likana kamwe serikali haiwalazimishi watu waliosema ‘hapana’ waseme ‘ndio.’ Huu ni msimamo wa Uislamu, dini ya haki.

Kuwalazimisha watu kufanya vile wasivyotaka kufanya ni uchokozi na Mwenyezi Mungu hawapendi wachokozi.

Imam Ali alichaguliwa baada ya kifo cha Uthman, Abdullah Ibn Umar, Saad Ibn Abu Waqqas, Usamah Ibn Zayd na masahaba wengine walikataa kumchagua yeye. Imam hakuwalazimisha waungane na walio wengi, wala hakuwafikiria wao kuwa wavunja sheria. Jambo moja tu alilotaka wafanye ni kutokuzuia utawala wake.

Masahaba walioishi wakati huo wa kuchaguliwa kwa Abu Bakr walikuwa na haki ya kumchagua au kukataa kumchagua yeye, na walikuwa na haki ya kuamini au kutokuamini sifa zake za kumfanya astahili kuchaguliwa. Kama ndivyo, vizazi vyta Waislamu ambao walizaliwa baada ya uchaguzi huo walikuwa na hali hiyo hiyo. Hawatakuwa wanatenda dhambi kwa kuchukua msimamo wa kukubali au kukataa Ukhilifa wa Abu Bakr.

Kutokana na hali hii inadhahirika wazi kwamba kuwatia hatiani kwa pamoa Waislamu wa leo kwa ama kuchukua msimamo wa kukubali au kukataa ukhalifa wa Abu Bakr ni wenyewe makosa na kunawakilisha fikira za ukereketwa usio na kipimo.

Kipengele cha pili chenye mwelekeo hasi cha aina hii ya uongozi ni kwamba haufanyi neno au tendo la Khalifa kuwa sharia tukufu. Kabla ya kuchaguliwa alikuwa hana kinga ya kutenda dhambi kama sahaba mwengine ye yote, na angeendelea kuwa hivyo hata baada ya kuchaguliwa. Uchaguzi

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

haubadilishi haiba yake, wala hauongezi elimu na ujuzi wake. Uchaguzi hamnyanyui juu ya waumini wengine bora mbele ya Mwenyezi Mungu wala haufanyi maneno yake na matendo yote kuwa sawa. Sana sana labda yeche angeweza kuwa ‘mujitahidi’ mwadilifu (mwanachuo mwenye uwezo kufanya maoni yenyeye kujitegemea kuhusu sharia ya Kiislamu). Wanachuo wengine wanayo haki kutokukubaliana naye, na Waislamu wa kawaida wanayo haki ya kuwafuata wanachuo wengine badala yake.

Mujitahidi mwingine anapoamini kwamba Khalifa kama huyo ni mwenye makosa kwenye maneno na matendo yake, hapasi kumfuata. Kuwataka Waislamu kufuata uamuzi usio sahihi ni kuwataka watu wafuate muelekeo ambao si wa Mwenyezi Mungu, na kuongezeka kwenye dini jambo amba-lo halitokani kwenye dini.

### MTEULE WA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.).

Hizi pande mbili za uchaguzi wa uongozi zenyeye mwelekeo hasi zisingekuwepo kwenye uongozi ulioegemezwa kwenye uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Endapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alichagua kiongozi, uamuzi wake ungekuwa wenye kumfunga kila Mwislamu, na kwa mujibu wa Qur’ani Tukufu, hapana yeyote ambaye angekuwa na haki ya kuukana.

**“Haiwi kwa muumini mwanamume wala muumini mwanamke kuwa na hiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume basi hakika amepotea upotofu ulio wazi.”<sup>29</sup>**

Watu wanapotoa kiapo cha utii kwa mteule wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wangekuwa kwa kweli wanafanya hivyo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

<sup>29</sup> Qur’ani Tukufu - *al-Ahzaab*; 33:36.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Na yeote anayotoa kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angekuwa anatoa kiapo cha utii kwa Mwenyezi Mungu. Qur'ani Tukufu inatangaza:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَنْ نَكَثَ فَإِنَّمَا يَنْكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ وَمَنْ أَوْفَ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهَ فَسُيُّونَتِهِ أَجْرًا عَظِيمًا﴾

“Bila ya shaka wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake, na anayetekeleza aliyomuahidi Mwenyezi Mungu atamlipa ujira mkubwa.” (Qur'ani; 48:10).

Khalifa aliyeteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anao utakatifu utokanao kwenye utakatifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Waislamu wanazake wa zama za uhai wake wanatakiwa kufuata maagizo na sheria zake, na ni vivyo hivyo kwa vizazi vitakavyofuata baada yao. Kwa kiwango fulani, anayo mamlaka ya kisheria yanayofanana na yale ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), isipokuwa yeye sio Mtume. Hatarajiwi kuongeza au kupunguza kanuni za Kislamu. Hapatakuwepo Mtume baada ya Muhammad (s.a.w.w.), na kanuni za Muhammad ni za daima na zitaendelea kuwepo hadi Siku ya Hukumu. Khalifa aliyeteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) humwakilisha yeye, na kwa sababu hiyo anatakiwa kuwa mjuzi wa Qur'ani Tukufu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kiwango cha juu sana. Lolote atalakolihalalisha litakuwa halali, na lolote atakalo liharamisha litakuwa haramu. Hapana Mwislamu atakayekuwa na haki ya kutokubaliana naye. Yeye ni mjuzi wa ngazi ya juu na utiifu kwake ni sawa na utiifu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### MAQURAISHI NA UKHALIFA.

Hivi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba Maimam wanatoka kwa Maquraishi? Na kama alisema hivyo, alikuwa na maana ya kusema kuwa ukhalifa utapatikana kwa njia ya uchaguzi au urithi, au kwa uteuzi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe?

Hadithi nyingi kuhusu mada hii zimeandikwa kwenye Sahih na vitabu vingine, ambazo baadhi yake ni kama zifuatazo:

Muslim aliandika kwamba Abu Hurairah alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Watu ni wafuasi wa Maquraishi. Waislamu wao wanawafuata Waislamu, na makafiri wao (asiye mumini ) wanawafuata makafiri wao.”<sup>30</sup>

Pia aliandika kwamba Jabir Ibn Abdullah alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: Watu ni wafuasi wa Maquraishi katika mema na maovu.”

Muslim pia anaandika kwamba Abdullah alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema; “Mamlaka ya Kiislamu (ukhalifa) yatakuwa kwa Maquraishi alimuradi watu wawili watakuwa hai hapa duniani.”

Pia aliandika kwamba Jabir Ibn Samurah alisumulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Dini hii itaendelea kudumu hadi Siku ya Hukumu inawadia au mpaka wawatawale ni nyinyi makhalifa 12 kutoka kwa Maquraishi.”

Al-Bukhari aliandika kwamba Ibn Umar alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Mamlaka haya ya Kislamu yatakuwa katika

<sup>30</sup> Hadith hii na hadith tatu zifuatazo zimeandikwa na Muslim kwenye *Sahih* yake, Jz. 12 Kitabu cha *Al-Imarah*, uk. 200-202.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

miliki ya Maquraishi almuradi watu wawili kutoka kwa Maquraishi wanaendelea kuishi.”<sup>31</sup>

Aliandika kupitia kwa wahadithiaji wake hadi kwa Jabir Ibn Samurah kwamba alisema: Nilimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: “Watatokeza watawala kumi na mbili. Halafu akasema neno ambalo sikulisikia, na baba yangu alisema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: Maimam wote hao watatokana na Maquraishi.” Al-Tirmidhi aliandika hivyo hivyo, isipokuwa alisema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Watatokeza watawala kumi na mbili baada yangu,” na kwamba baba yake na Jabir alisema: Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Maimam hao wote watatokana na Maquraishi.”<sup>32</sup> Al-Hakim kupitia kwa wahadithiaji wake hadi kwa Masrooq aliandika kwa kusema: Tulipokuwa tumeketi na Abdullah (Ibn Umar), mtu mmoja alimuuliza: ‘Ewe Abu Abdul-Rahman, je wewe na masahaba wengine mliwahi kumuuliza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni makhalifa wangapi watatawala umma huu?’ Abdullah akajibu: ‘Hapana mtu mwengine ambaye ameniuliza swali hili kabla yako tangu nimekuja Iraq.’ Halafu akasema: “Tulimuuliza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasema; Kumi na mbili, idadi sawa na wawakilishi wa wana wa Israeli aliokuwa nao Musa (a.s.).”<sup>33</sup>

Imam Ahmad aliandika kwamba Abu Bakr alisema: (kumwambia Saad Ibn Abadah) “Na wewe, Saad ulijua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema wakati ulikuwa umeketi: Maquraishi ndio watu wa mamlaka haya. Waadilifu mionganoni mwa watu ni wafuasi wa waadilifu wao, na waovu mionganoni mwa watu ni wafuasi wa waovu wao.”<sup>34</sup>

<sup>31</sup> Al-Bukhari, *Sahih Al-Bukhari* (kwenye kitabu cha Al-Ahkam) sehemu ya 9, uk. 78.

<sup>32</sup> Al-Tirmidhi, kwenye *Sunan* yake, sehemu ya 2, uk. 35 (Al-Fairuzabadi kwenye kitabu chake cha *Fadha-il Al-Khamsah* – fadhila za watano) sehemu ya 2, uk. 23.

<sup>33</sup> Al-Hakim, *Al-Mistadrak*, sehemu ya 4, uk. 501.

<sup>34</sup> Imam Ahmad, kwenye *Al-Musnad* yake, sehemu ya 1, uk. 5.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Ni dhahiri kwamba hadith ya kwanza haisemi kitu kuhusu ukhalifa. Kwani Maquraishi wote wakati wa ukhalifa walikuwa hawajagawanyika kati ya Waislamu na wasio Waislam. Maquraishi wote walikuwa wamekubali Uislam wakati huo. Inaonesha kwamba hadith hii ilikuja wakati ambapo Maquraishi walio wengi walikuwa makafiri. Hadith inazungumzia ushawishi wa Maquraishi juu ya makabila ya Waarabu. Kwani walikuwa wapinzani wa Uislam wakati Maquraishi walikuwa wanapigana nao. Na Maquraishi walipoingia kwenye dini hii mpya Waarabu wengi walikimbilia imani hiyo. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hadith hii hakuwa anajaribu kutangaza sharia ya Kiislamu au kutoa agizo kwa Waislamu. Alikuwa anasema kuhusu ukweli. Ambao ni mvuto wa Maquraishi na athari zake kwa makabila mengine ya Waarabu.

Hadith ya pili, kama ile ya kwanza, haizungumzii habari za ukhalifa, wala kuhusu nani atakuwa Khalifa. Ni taarifa ya hali ambayo ilikuwepo wakati wa hadith hiyo.

Kuhusu hadith sita za mwisho, kwa wazi zinazungumzia ukhalifa. Hadith hizi zinatofautiana kuhusu yale yaliyomo katika kila hadith bila kupingana. Baadhi ya hadith hizo zinasema kwamba unamilikiwa na Maquraishi. Hadith nyingine zinaongeza kwamba ukhalifa utaendelea kuwa miliki ya Maquraishi hadi mwisho wa dunia. Na nyingine zinaongeza kwamba makhalifa ni 12 na nyingine zinasema kwamba idadi ya makhalifa ni 12 lakini hazisemi kwamba wanatokana na Maquraishi.

Ili hadith hizi zieleweke, tunatakiwa kuziweka pamoja hadith mbili za Abdullah Ibn Umar, ambazo ndani ya mojawapo alisimulia kwamba ukhalifa utaendelea kuwa miliki ya Maquraishi hadi mwisho wa dunia, na katika hadith nyingine ambamo alisimulia kwamba idadi ya makhalifa ni 12 kama wawakilishi wa wana wa Israeli. Hadith hizi mbili zina hali ya hadith moja inaeleza mambo ya hadith nyingine na zinakubaliana na hadith ya Jabir Ibn Samurah ambayo ni mahsusizi zaidi mionganoni mwa hadith hizi zote na inayoweza kuzielekeza zile ambazo si mahsusizi mionganoni mwao.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Hivyo, hadith hizi zinatutaarifu kwamba watu amba si Maquireshi hawatakuwa makhalifa na kwamba makhalifa ni kumi na mbili tu, na kwamba ukhalifa utaendelea kuwa miliki ya Maquraishi almuradi watu wawili waliendelea kuishi duniani.

Matamko yanaweza kufasiliwa kwa mojawapo ya njia zifuatazo:

### **Je, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Alikuwa Anatabiri?**

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwa anajaribu kuwaelekeza Waislamu na kuwataarifu kile wanachotakiwa kufanya baada yake kuhusu Ukhilifa. Alikuwa, badala yake, alipozungumza nao kuhusu siku za usoni, akibashiri kwamba ukhalifa utakuwa chini ya miliki ya Maquraishi, daima hadi Siku ya Hukumu. Hivyo, anatutaarifu kwamba ukhalifa kamwe hautaingiliwa kati almuradi watu wanaishi kwenye uso wa ardhi na kwamba kila Khalifa atakuwa Quraishi, na kwamba makhalifa watakuwa kumi na mbili.

Kama mambo yalivyo, hii haiwezi kuwa kweli kwa sababu ukhalifa uliingiliwa kati na kukoma kwa sababu makhalifa walio wengi kama vile Uthmainiyah hawakuwa Maquraishi ama Waarabu.

Nyongeza ya haya, kusema kuwa makhalifa ni kumi na mbili haiwezi kuwa kweli kama ilikuwa na maana ya makhalifa amba ni waadilifu tu au wote pamoja na wasio waadilifu. Kwani idadi ya makhalifa waadilifu haikufika kumi na mbili, na kama tukiwajumlisha pamoja na idadi ya wasio waadilifu idadi yao ni kubwa zaidi ya kumi na mbili.

### **Je! Utawala wa Maquraishi ni Wakurithiana**

2. Njia ya pili ya kufasili hadith hizo hapo juu ni kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anajaribu kutoa maelekezo na kuwasilisha kwa Waislamu amri ya kidini, kwa hiyo, aliuambia umma wake kwamba baada yake makhalifa watatokana na Maquraishi na hapana mtu anayestahiki

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

kuwa Khalifa isipokuwa Qureishi. Hii ni kwa sababu Maquraishi wanao ukhusiano wa udugu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wa karibu au wa mbali, kwani wanaungana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupitia kwa baba wa babu yao “Fihr Ibn Malik.” Kwa sababu hii, Quraishi Mwislamu angestahili kuwa na sifa za kuwa Khalifa na asiyekuwa qureishi hängestahili kuwa Khalifa.

Kama tunakubali fasili hii, tutakuwa tunakiri kwamba mamlaka ya Kiislamu ni kwa kurithiana na kwamba haki ya kurithiana haingeacha ndugu wa karibu wa Mtukufu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ni pana zaidi hasa vyta kutosha kujumuisha koo zote za Maquraishi ambao ni kizazi cha ‘Fihr Ibn Malik.’

Kuamini kwamba Maquraishi Waislamu wanazo sifa za ukhalifa kwa sababu ya kuwa ndugu wa karibu au mbali wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ni sawa na kukubali nadharia ya kurithiana ambayo sharia ya mirathi ya Kiislam haiikubali. Kama mamlaka ya Uislam yanaweza kurithiwa kupitia undugu wa kuzaliwa, ndugu wa karibu huwazuia ndugu wa mbali kurithi, kwa mujibu wa sharia ya Kislamu.

Zaidi ya hayo, kuzuiwa kwa idadi ya makhalifa kuwa kumi na mbili inakuwa haina mantiki kwani waadilifu mionganini mwa makhalifa wa Qureishi haikufika idadi ya kumi na mbili na wasio waadilifu mionganini mwao walikuwa wengi zaidi ya kumi na mbili.

**Je! Makuraishi ni Bora Zaidi?**

3. Fasili ya tatu ya hadith hizi ni kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa njia ya matamko haya alikuwa anatangaza sheria ya kidini ambayo huu-fanya ukhalifa kuwa haki ya pekee ya Maquraishi. Hii si kwa sababu wanao uhusiano wa kindugu naye bali ni kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwapendelea wao zaidi ya wale wasio Maquraishi. Kama tukichukua fasili hii, tunapaswa lazima tukubali dhana mbili zinazopingana:

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

- a). Ukhilifa hauwi ni kwa njia ya uchaguzi wa Waislamu. Bali ni kwa uteuzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni Yeye Ndiye Aliyeamuru kwamba makhalifa wawe Maquraishi, watu wakubali ama wakatae.
- b). Dini ya Uislamu inawataka wafuasi wake kuamini ubora wa kikabila na utawala wa kabilia la Maquraishi ambao watu wake bila kujali kiwango cha imani yao wanapendelewa na Mwenyezi Mungu kuliko watu wengine, hata kama watu wengine wangkuwa washika dini zaidi, wenye hekima zaidi na wenye ujuzi zaidi.

Tunasema fikra hizi mbili zinapingana kwa sababu kama ukhilifa unapatikana kwa amri ya Mwenyezi Mungu, Muweza wa Yote anategemewa kumteua kwa uongozi wa waumini yule aliye na hekima zaidi na mwenye elimu na mwadilifu zaidi. Haingekuwa na mantiki kusema kwamba Mwenyezi Mungu anampendelea Abu Sufyani zaidi ya Ammar Ibn Yasir, kwa sababu Abu Sufyani alipigana na Uislamu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa muda wa miaka ishirini na moja.

Historia inakumbuka kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mnamo siku ya kutekwa Makka alisimama na kutangaza ifuatavyo:

“Enyi watu wa Qureishi, kwa hakika Mwenyezi Mungu amekomesha majivuno ya fikra za kabla ya Uislamu na maringo ya wahenga. Watu wanatokana na Adam na Adam alitokana na udongo.” halafu alikariri Aya ifuatayo:

**“Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye Mbora zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ni mcha- Mungu zaidi katika nyinyi.”** Hivyo kuwaweka Maquraishi juu ya wengine, si kwa sababu yoyote isipokuwa tu kwamba wao ni Maquraishi, inapingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa maneno na matendo.

Tena kuzuiwa kwa idadi ya makhalfa kuwa kumi na mbili ingekuwa si haki kwa sababu ile ile tuliyoitaja kabla.

### Kwani Watu Waliteuliwa Kwa Uadilifu Wao Tu?

4. Njia ya nne ya kufasili Hadith hizi ni kusema Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anajaribu kuwapa taarifa Waislamu kwamba Mwenyezi Mungu aliwateua watu kutoka kwa Maquraishi kuwa makhalfa. Hakuwateua watu hawa kwa sababu walikuwa na uhusiano wa kindugu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wala si kwa sababu walikuwa Maquraishi. Aliwachagua wao kwa sababu walikuwa ndio bora zaidi mionganini mwa Waislamu. Watu hawa ndio Makhalifa wa halali, kwa vyovyyote vile, watu wachague au wawakatae.

Hadith sita za makhalfa wa Kiquraishi zinaonesha wazi kabisa kwamba Mwenyezi Mungu hakuwaachia Waislamu fursa kamili katika kuteua makhalfa wao. Bali hasa aliamua kwamba makhalfa wao walikuwa watokane na Maquraishi. Haingekuwa na mantiki kuamini kwamba alifanya hivyo kwa sababu Maquraishi ni ndugu zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au kwa sababu Maquraishi ni bora zaidi kuliko Waislamu wengine. Hii ingekuwa ni kukaribisha utawala wa kikabila, jambo ambalo ni geni kwa imani ya Uislamu inayodai usawa, hutukuza waadilifu na huwadharau wahalifu. Historia ya Uislamu inashuhudia kwamba Maquraishi walio wengi walikuwa na chuki sana kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na dini yake kabla ya wao kukubali kuwa Waislamu, na waliokuwa na imani dhaifu kuliko wengine baada ya kukubali Uislamu.

Ingekuwa na mantiki tu kusema kwamba Uqureishi wa Makhalifa ni kama Uqureishi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Mwenyezi Mungu hakumteua Muhammad kwa sababu alikuwa anatokana na Maqureishi au kwa sababu alikuwa Bani Hashim au kutoka kwa dhuriya ya Abdul

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Mutalib au kutoka Makka. Alimteua yeye kwa sababu alikuwa ndiye mbora kabisa mionganoni mwa watu hapa duniani na ilitokea kwamba aliye mbora mionganoni mwa watu wa dunia alikuwa Qureishi, kutoka kwa dhuriya ya Abdul Mutalib. Na kwa hiyo makhalifa ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizungumza habari zao waliteuliwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu walikuwa ni watu bora zaidi mionganoni mwa watu wa dunia na ilitokea kwamba walikuwa wanatoka kwa Maquraishi. Fasili hii yenye mantiki inakubaliana na madhehebu ya Shia. Mwenyezi Mungu anapomteua mtu kuwa Imam wa watu, atakuwa Imam ijapokuwa Waislamu watamkubali au watamkataa, kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu anavyotuea Mtume, atakuwa Mtume hata kama watu wawe hawaamini Utume wake.

### MAQURAISHI NA UCHAGUZI HAVIPATANI.

Ni jambo lisiloweza kupatanishwa kusema kwamba Mwenyezi Mungu ameamuru kwamba makhalifa watoke kwa Maquraishi na kwamba aliwaachia Waislamu suala la kuwachagua makhalifa kutoka mionganoni mwa Maquraishi.

Mwenyezi Mungu ameamuru kwamba Khalifa watoke kwa Maquraishi ili wawaongoze Waislamu kwa kile kilicho bora zaidi kwao. Kama aliacha uteuzi wa Khalifa kutoka kwa Quraishi kuwa chaguo la Waislamu, angeacha ukhalifa wa siku za usoni katika jinsi ya kubahatisha. Kuchaguliwa na watu haina maana ya kupatikana uongozi ulio bora kabisa kwani watu hawajui nini kilichojificha ndani ya nyoyo za watu. Mwenyezi Mungu Ndiye tu anayejua hayo.

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu hakuacha ukhalifa kuwa chaguo la watu moja kwa moja na aliamuru kwamba makhalifa wao wapatikane kutoka kwenye kundi la Maquraishi, chaguo lote lazima liwe la kwake. Hangegawa chaguo baina Yake na Waislamu na Yeye kubaki na chaguo la

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

kabila na uchaguzi wa mtu, kutoka kwenye kabila ufanywe na Waislamu.

Mwenyezi Mungu anatarajiwa kuchagua kabila kwa ajili ya upatikanaji wa mteule na si kumteua mtu kwa ajili ya kabila. Mwenyezi Mungu amechagua ukoo wa Hashim na kabila la Qureishi kwa ajili ya upatikanaji wa Muhammad, na hakumchagua Muhammad kwa sababu yeye ni wa ukoo wa Hashim na kabila la Quraishi. Kuchagua mtu badala ya ukoo ndipo unapopatikana uongozi ulio bora. Hivyo, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake walipotuambia kwamba makhalifa walipatikana katika kabila la Qureishi, kwa usahihii walikuwa wanatuambia kwamba wapo watu mahsusii waliotokea kwenye kabila la Quraishi, na waliteuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa makhalifa. Walichaguliwa kwa sababu ya sifa zao za juu sana za kuwafanya wastahili kuwa makhalifa na si kwa sababu ya wao kuwa ni Maquireishi.

\* \* \* \* \*

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### SURA YA KUMI NA SABA

#### ALI ANAUTAZAMA HUO URITHI.

Ipo nadharia inayodai kwamba vita vyatia wenyewe kwa wenyewe vilivyo otokea wakati wa utawala wa Abu Bakr vingeepukwa endapo Ali angemirthi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Nadharia hii ya kuvutia (ambayo mimi wala sithibitishi ama kukanusha) imeegemezwa kwenye sababu zifuatazo:

1. Tangazo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hapo Ghadiir Khum alipokuwa anarudi kutoka kwenye Hija yake ya mwisho, liliwafanya maelfu ya mahujaji kuamini kwamba alikuwa amemchagua Ali kumrithi yeye.

Walicho kielewa kutoka kwenye tangazo kilionekana kuendana na mila yao ambayo humpa mamlaka ndugu aliye karibu sana na kiongozi. Walipotambua kwamba Abu Bakr ndiye aliyepewa uongozi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), baadhi yao waliipinga serikali mpya na wakakataa kutoa Zaka (kodi ya Kiislamu). Wengine walifika mbali zaidi kwa kuukimbia Uislamu, wakifikiria kwamba masahaba waliasi tangazo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Walidhani kwamba masahaba hawakuwa makini katika kuukubali Uislamu. na kwa hiyo, makabila ya Waarabu walifikiri kwamba walikuwa na haki ya kuacha Uislamu na kurudi kwenye upagani.

2. Kama Ali angepata uongozi baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sifa yake ya kivita ingeweza kumzuia yeyote ambaye angetaka kumpa changamoto kuhusu uongozi wake. Hadith kuhusu ushujaa wake zilikuwa zinakumbukwa na kila Mwarabu. Mabedui pamoja na wakazi wa vijiji na mijini waliona na kushuhudia vitendo vyake vyatia katika kipindi cha miaka kumi ya mwisho ya uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa nini wathubutu kukabiliana naye kwenye vita ambavyo hawatashinda?

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Endapo kama nadharia hii ni sahihi au si sahihi, vita vyta wenyewe kwa wenyewe vilikuwa vyta uamuzi kuhusu Ali. Vilimlazimisha kusitisha upinzani wake kwa Abu Bakr na kuahidi msaada wake ili serikali ya Waislamu isije kudhoofu katika mapambano yake dhidi ya walioritadi. Ali alikuwa mcha-Mungu mno kuweza kuendeleza upinzani wake ambapo hatari zilikuwa zinatishia msingi wa Uislamu.

Kwa miezi kadhaa Imam Ali alikataa kuungana na wale waliomchagua Abu Bakr, na alitarajiwa kuendelea kufanya hivyo. Vita vyta wenyewe kwa wenyewe hata hivyo, vilifanya alazimike kubadilisha msimamo wake.

Mtazamo wa Imam unaweza kuwasilishwa kama ifuatavyo:

Aliamini kwamba uongozi ni haki yake yeye peke yake. Alikuwa hazina ya ujuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), chaguo lake na ndugu yake wa karibu sana. Inasimuliwa kwamba wakati Abu Bakr alipomtaka Ali aungane na watu waliomchagua yeye, Ali alijibu: Mimi ndio ninayo haki ya uongozi. Sitakuuata wewe ambapo wewe ndiye unayetakiwa kunifauta mimi.” Abu Bakr alipomuuliza Ali: “Hivi kuchaguliwa kwangu hakutokani na ridhaa ya walio wengi?” Ali akajibu: “Lakini uliwaambia Maquraishi na watu wa Madina kwamba wewe unstahili uongozi kwa sababu una uhusiano wa kindugu na Muhammad, na wakakubaliana na wewe. Mimi ninayo hoja hiyo hiyo dhidi yako.” Halafu akasema: “Sisi tunayo haki zaidi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), awe hai au amekufa. Sisi ni watu wa Nyumba yake, sehemu yake na kuhifadhia siri, hazina ya elimu yake na hekima. Hapana mtu ye yeyote katika umma huu anaweza kuja karibu na nafasi za watu wa Nyumba ya Muhammad. Na wale ambaa wanapaswa kuwashukuru kwa wema wao wasilinganishwe nao.”<sup>35</sup>

<sup>35</sup> Abdul Fattah Abdul Maksuud, *Al-Imam Ali Ibn Abu Talib*, sehemu ya 1, uk. 179.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Alisema pia: "Mimi ni wasii wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), waziri wake na mdhamini wa siri zake na ujuzi wake ..... Mimi ni mtu wa kwanza kumwamini yeye, mimi ni mtetezi wa nguvu sana wa Uislamu miongini mwenu katika kupambana na makafiri, mjuzi wa kiwango cha juu sana wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na mwenye uwezo mkubwa wa kubashiri athari za matokeo ya matukio. Hadi lini mtaendelea kukataa kutupatia uongozi wetu? Tupeni haki, na mzikubali haki zetu kama watu wa Madina walivyofanya kwenu."<sup>36</sup>

Ali hakukosa kuwa na ushahidi wa uwasiwake au waziri wake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpa kazi ya uwasiwake alipokusanya ndugu zake wa karibu, miaka kumi kabla ya Hijiriya. Kwenye mikutano huo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia watu wa ukoo wake, wakati mkono wake ulikuwa kwenye shingo ya Ali; "Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na mrithi wangu. Msikilizeni na mumtii." kuhusu kazi yake ya uwaziri, tamko la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambalo lililosimuliwa kwa usahihi, linashuhudilia: "Ewe Ali, hungefurahi wewe kuwa kwangu kama Haruna kwa Musa (a.s.), lakini hapatakuwepo na Mtume tena baada yangu?" Haruna alikuwa waziri wa Musa (a.s.) kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu:

**"Na nipe waziri katika watu wangu, Haruna ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu, na mshirikishe katika kazi yangu."**<sup>37</sup>

Kuhusu udhamini wa siri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ujuzi wake, inatosha kukumbuka kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Mimi ni Jiji la Elimu na Ali ni Lango Lake. Yeyote anayetaka kuingia kwenye Jiji lazima apite kwenye Lango."

**Yeye Aliamini Kwamba Kuchaguliwa Kwa Abu Bakr Hakukuambatana Na Masharti.**

<sup>36</sup> Al-Tabarsi, *Al-Ihtijaj* sehemu ya 1, uk. 95.

<sup>37</sup> **al-Qur'an; 20: 28-31**

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Imam aliuona uchaguzi wa kumweka madarakani Abu Bakr haukuambatana na masharti yenye kuwabana wale waliomchagua. Kwa dhahiri aliamini kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimteua yeze kuongoza umma na kuendesha mambo yake baada yake, na kwamba chaguo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) liliambatana na masharti kwa umma. Hivyo, umma hauna haki ya kuchagua kiongozi mwingine. Kama Imam hangekuwa ameaminii hivi hangewaambia watu wa Madina kubadilisha msimamo wao baada ya kumchagua Abu Bakr. Uchaguzi uliokamilika ni mkataba unaotakiwa kutimizwa, na Ali alikuwa mwadilifu sana kiasi cha kutoweza kuwataka watu kuvunja mkataba halali.

Yeye na mke wake Fatima Az-Zahra (mama wa nuru), binti yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), waliwatembelea masahaba wa Madina kwa madhumuni ya kutafuta kuungwa mkono nao na kuwaomba wabadili msimamo wao kuhusu Abu Bakr.

Muawiya, kwenye mojawapo ya barua zake kwa Imam alisema: Na ninakumbuka ulikuwa na desturi ya kumbeba mke wako wakati wa usiku juu ya punda ambapo mikono yako ikiwa juu ya mikono ya watoto wako Al-Hasan na Al-Husein, baada ya kuchaguliwa kwa Abu Bakr. Ulimtembelea kila shujaa wa Badr na karibu kila Mwislamu wa siku za mwanzo ili wakuunge mkono na uliwaendea ukiwa na mke wako, ukiwaonesha watoto wako wawili, na ukiwaomba wakupe msaada dhidi ya sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ...”<sup>38</sup>

<sup>38</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, fasili yake ya *Nahjul Balaghah*, Juz. 1, uk. 131.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### Hakutaka Kufikia Lengo Lake Kwa Nguvu.

Licha ya imani kuwa haki yake iliporwa hakutaka kuirejesha kwa nguvu, wala hakutaka kuharibu mshikamano wa Waislamu. Imam alitambua kwamba alikuwa hana msaada mkubwa. Watu wote wa Makka walikuwa wapinzani wake kabisa. Kwao, alikuwa mtu ambaye aliwauwa baba, kaka, watoto na ndugu zao wengi katika kampeni yake ya kuuhami Uislamu. Watu wa Madina walikuwa karibu naye kuliko Maquraishi, lakini hawakuwa na dhamira ya kujitoa mhanga kwa ajili ya uongozi wake. Walikwishawekeana mkataba na Abu Bakr, na walidhani kwamba kiapo chao cha uaminifu kililenga mahali pake.

Ali alikuwa na watu kadhaa mionganoni mwa masahaba mashuhuri waliomuunga mkono kama vile: Bilal, Salman Al-Farsi, Abu Dharr, Al-Bursa Ibn Azib, Ammar Ibn Yasir, Al-Miqdad Ibn Al-Aswad na Zubeir Al-Awwam. Lakini masahaba hawa hawakuwa na wafuasi. Hivyo Imam akaona kwamba hakuwa na chaguo lingine isipokuwa uvumilivu.

### Alibadili Msimamo Wake kwa Ajili ya Kudumisha Umoja.

Angeweza kuendelea na upinzani dhidi ya Abu Bakr alimuradi Abu Bakr aliendelea kuwa hai. Saad Ibn Ubadah aliendelea na upinzani hadi mwisho wa uhai wa Abu Bakr. Hata hivyo, vuguvugu la makabila ya Waarabu kuikimbia imani, kwake hilo likawa jambo la kusababisha aamue vinginevyo. Upinzani wake kwa Abu Bakr haukusabishwa na tamaa ya makuu. Badala yake msimamo huo ulisababishwa na kutaka kwake kuwaweka Waislamu kwenye njia ya kweli ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Uislamu ulipotishiwa na harakati za kuuhami, Ali aliona si busara kujihusisha na mbinu ya kuwaongoza Waislamu ambapo kuwepo kwa Uislamu wenyewe kulikuwa kunakabiliwa na hatari kubwa.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Al-Baladhuri aliandika kwamba Waarabu walipokimbia dini ya Uislamu Uthman alimwendea Ali akisema: “Ewe binamu, hakuna mtu atakayepigana na adui wakati wewe unakataa kusuluhiishana na Abu Bakr.”<sup>39</sup> Alimshawishi Imam kwenda naye kwa Abu Bakr; pale Abu Bakr alipo-muona Imam, walikumbatiana na kulia. Waislamu walifurahishwa na tukio hilo na kuazimia kupigana na wale wanaoritadi.

Al-Bukhari, kwenye *Sahih* yake aliandika kwamba Imam alimwambia Abu Bakr walipokutana: “Tunatambua msimamo wenu na kile ambacho Mwenyezi Mungu amewapeni lakini mmechukua uongozi bila kushauriana na sisi. Tunaamini kwamba tunao mgawo wetu na haki yetu katika uongozi kwa sababu ya uhusiano wetu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).” Abu Bakr akalia; waliahidiana kukutana msikitini, usiku. Ali alikwenda Msikitini na kawaambia watu kwamba upinzani wake haukusababishwa na wivu juu ya Abu Bakr wala kukanusha nafasi yake; “lakini tunaamini, kwamba tunayo haki katika uongozi huu, na alichukua uongozi huu bila kushauriana na sisi, hivyo, tulihisi wasiwasi.”<sup>40</sup>

Imam alisema kuhusu kile kilichotokea katika kipindi hicho kwenye ujumbe aliotuma kwa watu wa Misri, alipompeleka Malik Al-Ashtar kuwa gavana:

“..... Na nilizua mkono wangu hadi hapo nilipoona watu waliokuwa wanakimbia Uislamu wanatangaza kuangamiza dini hii ya Muhammad. (Wakati hatari hii ilijitokeza, mimi nilibadili msimamo wangu) na niliamua kuusaidia Uislamu na wafuasi wake, isijekuwa nikashuhudia kuangamizwa kabisa kwa Uislamu au sehemu yake, halafu msiba kwangu unakuwa mkubwa zaidi kuliko kupoteza uongozi wenu ambao ni wa kupita.”<sup>41</sup>

<sup>39</sup> Sayed Murtadha Al- Askari aliwasilisha kwenye kitabu chake; *Abdallah Ibn Saba*, uk. 73.

<sup>40</sup> Al-Bukhari, *Sahih* yake sehemu ya 5, uk. 108.

<sup>41</sup> *Nahjul Balaghah*, sehemu ya 3, uk. 198-199.

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

### **SURA YA KUMI NA NANE**

#### **ABU BAKR AMTAJA MRITHI WAKE.**

Abu Bakr alikufa, na maisha yaliyojaa mafanikio muhimu yalikoma.

Aliwadhibiti waliokuwa wanakimbia imani na ambao walizua kulipa Zaka. Aliyarudisha makabila ya Waarabu kwenye Uislamu, na akawafanya kuwa wapiganaji walinzi wa Uislamu baada ya kuwa maadui.

Kwa Amri yake Aya na Sura za Wahyi zilikusanywa kwenye kitabu cha Uislamu, Qur'ani Tukufu.

Alipeleka imani ya Uislamu nje ya mipaka ya Rasi ya Bara Arabu. Alikufa ambapo majeshi ya Waislamu yalikuwa yanapambana na majeshi Uajemi ndani ya Iraq na majeshi ya Kirumi ndani ya Syria.

Kifo cha Abu Bakr kilipokaribia aliamua kumteua mrithi, na hii ilikuwa ni haki yake. Aliamua asiliache jambo hili la uongozi wa dola kwenye hatma ya kubahatisha.

Kama historia ingekuwa na mantiki, Ali angemrithi Abu Bakr. Alirukwa baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu uchaguzi ulifanyika haraka bila mpango wala kushauriana. Inasemekana kwamba dharura iliyosababishwa na mkutano wa watu wa Madina huko Saqifa Banu Sa'idah, na kutokuwepo kwa Ali ambaye alijishughulisha na maziko ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliwfanya masahaba wasimtilie maanani Ali (a.s.) na sifa zake.

Kama huu ndio ulikuwa ukweli, Ali angelikumbukwa wakati huo. Hapangekuwepo na dharura yoyote na Khalifa aliweza kumteua ye yeyote aliye mtaka. Bado Ali hakutiliwa maanani na Khalifa.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Maquraishi walismama dhidi yake kwa sababu nyingi, na sifa zake bainishi za kiwango cha juu pamoja na yeye kuwa na uhusiano wa karibu wa kindugu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilikuwa ndio sababu kuu.

Koo za watu wa Makka zilipigana vita vya gharama kubwa dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu hawakutaka ukoo wa Hashim kuwa na sifa ya pekee ya kutokeza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mionganoni mwao. Msimamo huu ulizifanya koo za watu wa Makka kuuzuia ukoo wa Hashim kuwanayo sifa nyingine ya pekee ya kumruhusu Ali kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ushawishi wa Maquraishi ulikua haraka wakati wa utawala wa Abu Bakr. Kukua kwa haraka kwa mvuto wa Maquraishi kulitarajiwa kuongeza umbali baina ya Ali na hicho Cheo cha Juu.

Mtu anaweza kusema kwamba Abu Bakr asingefuata msimamo wa Maquraisha usio wa haki kuhusu Ali baada ya kuwa amesikia matamko mengi sana ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambayo yalionesha kwamba Ali alikuwa chaguo lake. Lakini Abu Bakr alionesha kutokuamini kwamba matamko ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu Ali yaliwalazimisha Waislamu kumfuata yeye. Kama angeamini hivyo, hangekubali kuwa Khalifa wa kwanza. Kwa kuwa nayo maoni ya aina hii, alidhani alikuwa na hiyari ya kumchagua Ali au mtu mwingine yejote kutoka mionganoni mwa masahaba mashuhuri. Hakumchagua Ali, kwa sababu alikuwa mshindani wake mkubwa. Alimteua Umar Ibn Al-Khattab, msaidizi wake mkuu, mtu mpangaji wa kuchaguliwa kwake na mtu wa karibu sana katika mambo yake yote.

Msomaji anaweza kukumbuka kwamba Ali alipoelewana na Abu Bakr alilalamika kwa nini Abu Bakr hakutaka ushauri wake wakati alipochagiuliwa na kwamba alichukua kutoka kwa Ali kile ambacho kilikuwa stahili ya Ali. Abu Bakr alisikiliza malalamiko yake na akalia. Machozi ya Abu Bakr yalionesha dalili kwamba hangerudia tena kosa kama hilo. Alikuwa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

anatarajwa kutaka ushauri wa Ali na watu wengine wa ukoo wa Hashim, pamoja na masahaba waliokuwa wanamuunga mkono Ali. Abu Bakr hakufanya hivyo.

Inafaa kuzingatia kwamba Fatima Az-Zahra, Binti yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alikuwa hawasemi vizuri na Abu Bakr, na alikuwa anawasihi watu wa Madina kumuunga mkono Ali badala ya Abu Bakr. Fatima alimkasirikia Abu Bakr kwa sababu ya ukhalifa na kwa sababu alitaifisha ‘Fadak’ (viunga vya bustani) ambayo alipokea kutoka kwa baba yake na alitakiwa kuwa navyo kama zawadi au urithi. Lakini Abu Bakr alitoa taarifa na kusema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema; Sisi, Mitume hatuachi vitu vya kurithiwa.

Fatima alikanusha kwamba baba yake hakusema hivyo, kwa sababu alivyosema Abu Bakr ni kinyume cha Qur’ani ambayo inasema kwamba Suleiman alipokea urithi wake kutoka kwa baba yake Daudi. Wote wawili, Daudi na Suleiman walikuwa Mitume.

Abu Bakr alijitahidi kufanya uhusiano uwe wa kawaida bila kubadili msimamo wake kuhusu Fadak, lakini Fatima alikataa kusema naye, na alipokufa Abu Bakr hakuambiwa kuhusu kifo chake, ili asije akahudhuria maziko yake.<sup>42</sup>

Abu Bakr alihangaishwa sana na hasira za Fatima kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Fatima ni pande la nyama yangu. Yeyote anayemkasirisha yeye amenikasirisha mimi.” Pia alisema: “Fatima ni kiongozi wa wanawake wa Peponi.” (Hadith hizi mbili zimeandikwa na Al-Bukhari kwenye *Sahih* yake, sehemu ya uadilifu wa Fatima).

<sup>42</sup> Al-Bukhari ameandika kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 5, uk. 178. Pia Muslim aliandika kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 12 ‘*Hukm ya Al-Fei*’ (utajiri upatikanao kutoka kwa maadui wa Uislamu) uk. 77.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Kwa yote haya, Khalifa mwadilifu angetarajiwa kumtaja Ali mrithi wake, kwani kitendo hicho kingemfurahisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu kingemfurahisha Fatima, ingawa kwa kuchelewa. Abu Bakr haku-fanya hivyo, wala hakutaka ushauri wa Ali au mtu yejote wa ukoo wa Hashim pamoja na Al-Abbas mjomba wake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Kwa kweli, Abu Bakr hakutaka ushauri wa sahaba yejote kuhusu nani amrithi yeye. Hakuwapa chaguo la baina ya wagombea wawili au zaidi. Aliwataka ushauri masahaba wachache kuhusu Umar na Umar pekee yake. Waliotakiwa kutoa ushauri ni Abdul-Rahman Ibn Awf, Uthman Ibn Affan na Usaid Ibn Hudheir. Hawa walikuwa watu wanaomuunga mkono Umar. Talha, binamu yake Abu Bakr hakuwemo kwenye orodha ya washauri, na alipomshutumu Umar, Abu Bakr aling'aka kwa hasira.

Kwa nini tusiyaite matukio haya kwa majina yao? Abu Bakr alikuwa anamwia Umar katika kuchaguliwa kwake na kuanzisha uongozi wake. Alikuwa msaidizi wake mkuu wakati wa Ukhilifa wake. Abu Bakr alitaka kulipa fadhila kwa rafiki yake mzuri. Tunasema hivi, bila kujali kupunguza uaminifu wa Khalifa wa Kwanza.

Alipokuwa anafariki, Abu Bakr alimuamuru Uthman kuandika wasia wake. Alipofika kwenye maneno yafuatayo: "Nimemteua kama mrithi," alipoteza fahamu kabla ya kutamka jina la mteule wake. Alipopata fahamu tena alimwambia Uthman amsomee yale aliyokwishaandika, na kwa mshangao wake, Uthman aliandika jina la Umar. Abu Bakr alifurahishwa sana na hilo.

Kama mambo yalivyo, Khalifa mpya alifurahishwa zaidi na kitendo cha Uthman. Alikumbuka kitendo hiki cha upendeleo kwa Uthman. Alimpa zawadi ya upendeleo wa iana hiyo hiyo mwishoni mwa utawala wake.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### SURA YA KUMI NA TISA.

#### UMAR ANARITHI.

Umar alichukua nafasi kuwa Khalifa wa Pili miaKa 14 baada ya Hijiriyah (635 A.D). Alithibitisha kuwa Khalifa aliyefaa sana mionganini mwa makhalifa katika kuelekeza sera ya Dunia ya Kiislamu na matukio yake.

Kipindi cha uongozi wake kilijaa mafanikio ya kustaa jabisha na matukio yaliyo dhahiri. Kama kawaida sera ya kiongozi wa nchi huwa na vipengele vyya ndani na nje ya nchi, sera ya Umar ilikuwa na vipengele vyote hivyo, pamoja na vipengele vyya siku za nyuma na za usoni, kwani ushawishi wake ulivuka nje ya mipaka ya utawala wake, yenyewe athari nyingi sana.

Kufuzu kwa sera yake ya nje kulikuwa kunag'ara kwenye macho ya wanahistoria, Waislamu na wasio Waislamu. Alirithi kutoka kwa Abu Bakr Vita ya Dunia dhidi ya dola mbili kuu za wakati huo; Dola ya Uajemi na Rumi.

Majeshi ya Waislamu wakati wa utawala wake, yalipambana na majeshi ya Uajemi na yaliweza kuiweka Iraq na Ajemi pamoja na Al-Ahwaz na Azarbaijan, chini ya himaya ya Uislamu. Majeshi ya Waislamu yaliyokuwa Kaskazini Magharibi yaliweza kuyashinda majeshi ya Rumi na kuingiza Syria na Misri kwenye mamlaka ya Kiislamu.

Hivyo, chini ya uongozi wake, majeshi ya Waislamu yaliweza kuzisambaratisha dola mbili mashuhuri za wakati wake. Ushindi wa kiroho uliotokea sambamba na ule wa kijeshi ulikuwa mkubwa zaidi. Sera yake kuhusu wakazi wasio Waislamu wa nchi zilizotekwa, ilikuwa ya hali nzuri. Alitoza kodi kwa nchi iliyotekwa, pamoja na kodi ya kila mtu mzima mwanamume. Hapana yejote mionganini mwa wafuasi wa dini nyinginezo aliyeonewa wakati wa utawala wake. Alitambua haki zao za msingi na

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

uhuru wao. Historia iliandika neno lake kama lilivyoelekezwa kwa Amr Ibn Al-Aas, ambaye alikuwa gavana wa Misri wa kuteuliwa na yeye ambaye mwanae wa kiume alimpiga Mkristo Mkibti. “Amr, ni lini ulipo wafanya watu watumwa ambapo walizaliwa wakiwa huru?”<sup>43</sup>

Sera yake ya ndani hasa zaidi ilikuwa imefuzu. Inaweza kufupishwa ifuatavyo: Kuhusiana na familia yake, Waislamu kwa ujumla, kuhusiana na wenzake mionganoni mwa sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuhusiana na watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

**Kuhusu yeye na familia yake:** Sera yake ilikuwa kamilifu. Mamia ya mamiloni ya dirham (dirham ya wakati wake ilikuwa sawa na dola moja ya wakati wetu) zilikuwa zinamiminika kwenye hazina ya serikali ya Kiislamu. Japokuwa alikuwa na mamlaka yasiyo na mipaka, yeye na familia yake waliishi kwenye umasikini. Imesimuliwa kwamba alisema; “Ninashughulikia hazina ya Waislamu kama ninavyoshughulikia mfuko wa mayatima. Kama sihitaji, siigusi, na kama ninahitaji ninatosheleza mahitaji yangu tu.”

**Kuhusiana na Waislamu kwa ujumla:** Sera yake ilijulikana kuwa ya uadilifu, thabiti na ya kusaidia. Aliwapa wapiganaji na familia zao na wakazi wa Madina pamoja na wengine wengi mahitaji ya kutosha.

**Kuhusu uhusiano wake na masahaba:** Aliwagawia mahitaji yao kwa mujibu wa jinsi walivyoshiriki katika kutetea Uislamu. Alijaribu kuwazuia masahaba wasivutiwe na tamaa ya utajiri au kuogopa kutumia uzoefu wao mzuri sana katika kuendeleza mvuto wao, aliwazuia masahaba wasiishi kwingineko popote isipokuwa Madina. “Mimi ninasimama kwenye lango la Madina, alisema, akishikilia makoo ya Maquraishi na mikanda wasije wakaangukia motoni.”<sup>44</sup> Hivyo, aliwadhibiti masahaba wa Mtukufu

<sup>43</sup> Ibn Saad, *Al-Tabaqat*, sehemu ya 3, uk. 276.

<sup>44</sup> Abdul-Fattah Abdul-Maqsoud, *Al-Imam Ali Ibn Abu Talib*, sehemu ya 1, uk. 223.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Mtume (s.a.w.w.) wenye tamaa ya makuu kwa uangalifu mkubwa.

**Kuhusu watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):** Sera yake ilichanganyika na uvutiwaji na tahadhari. Hakumpa yeote mionganoni mwao kazi yeote ya kiserikali. Hata hivyo, wasiwasi baina yake na Ali ulioanza baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuendelea wakati wa kipindi cha Abu Bakr ulipungua na badala yake hali ya urafiki ilishika nafasi hiyo polepole na kukua jinsi muda ulivyosonga mbele. Umar alikuwa na desturi ya kukimbilia kwa Ali kutaka ushauri kuhusu matukio makubwa, akitafuta ufumbuzi wa matatizo makubwa.

Alipopewa taarifa kwamba serikali ya Uajemi imeandaa jeshi kubwa sana kwa lengo la kupigana na Waislamu, alitaka ashiriki katika vita hivyo ili kuhamasisha jeshi la Kiislamu. Alipotaka ushauri kutoka kwa Imam Ali na masahaba wengine, Imam alimwambia: Njia ya Kiislamu haikushinda au kushindwa kwa ukubwa au udogo wa idadi. Ni dini ya Mwenyezi Mungu ambaye Ndiye aliyeifanya iendelee kudumu na jeshi lake ambalo alilian-daa na kupanuka hadi kufika hivi lilivyo na kuonekana kama liliy-oonekana. Tumeahidiwa na Mwenyezi Mungu na Atatimiza ahadi yake na kulisaidia jeshi lake. Nafasi ya kiongozi ni nafasi ya kamba (uzi) kwenye shanga. Uzi huukusanya shanga na kuziunganisha na kuwa pamoja, kama uzi ukikatika, shanga zitasambaa na kamwe hazitakuwa pamoja kabisa. Ingawa Waarabu ni wachache leo kulinganishwa na wengine, wao ni wengi kupitia Uislamu na wanazo nguvu kwa sababu ya kuungana kwao. Wewe kama muhimili wa kinu, kiruhusu kinu kizunguke na waruhusu Waarabu washiriki vitani bila wewe kuwepo. Ukiondoka utakuwa umeacha nyuma yako hatari ambazo zitakuhangaisha zaidi kuliko yale utakayo kabiliana nayo vitani.

Kama Waajemi watakuona wewe kwenye uwanja wa vita, watasema: ‘Huyu ndiye chanzo cha hatari. Mkimwangamiza mtashinda.’ Vita vyao vitakuwa vikali sana na matumaini yao kuwashinda Waislamu yataongeze-ka zaidi.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Kama ulivyosema kuhusu Waajemi kutembea kwa lengo la kupigana na Waislamu, Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote anayachukia matembezi yao kuliko kama unavyoyachukia wewe, na Yeye anao uwezo wa kubadili kile asichokipenda. Kuhusu idadi yao kubwa, sisi kamwe hatukupigana kwa nguvu ya wingi wa idadi. Sisi tulipigana kwa msaada tu wa Mwenyezi Mungu na kusaidiwa na Mwenyezi Mungu.”<sup>45</sup>

## UMAR NA ELIMU YA ALI

Umar alipendezewa sana kwa ujuzi mkubwa wa Ali. Inasemekena kwamba alisema; “Hapana mtu ambaye ataruhusiwa kutoa fatwa kama Ali yupo kwenye Msikiti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).” Umar alipofanya uamuza mbaya kuhusu kanuni za Kislamu, Ali alikuwa na desturi ya kumsahihisha. Mara kwa mara alikuwa akisema: “Kama Ali hangekuwepo, Umar angekwisha angamia (kiroho).”<sup>46</sup> Umar alionesha kuwa anahitaji sana ujuzi wa Ali kwa kusema: “Mwenyezi Mungu na aniepushe na tatizo linapotokea Abu Hasan akiwa hayupo.”

Mwanamke alishitakiwa kwa sababu alijifungua mtoto miezi sita baada ya kuolewa. Umar aliamua mwanamke huyo apigwe mawe hadi kufa. Ali akamwambia: “Ewe kiongozi wa Waumini, mwanamke huyu akikata rufaa kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kwa kuhoji uamuza wako, atakushinda. Mwenyezi Mungu anasema; Vipindi vyta mimba na kunyonyesha ni miezi thelathini.” Tena Mwenyezi Mungu anasema: “Akina mama hunyonyesha watoto wao kwa miaka miwili kamili kwa yejote anayetaka kipindi kamili cha kunyonyesha.” Kama tukitoa miezi ishirini na nne kutoka kwenye miezi thelathini, miezi itakayo bakia ni sita. Umar alibadilisha uamuza na akamwachia huru mwanamke huyo.

<sup>45</sup> Al-Sayyed Al-Radhi, *Nahjul Balaghah*, sehemu ya 2, uk. 29-30.

<sup>46</sup> Abul-fattah Abdul Maqsoud, *Al-Imam Ali Ibn Abu Talib*, sehemu ya 1, uk. 226.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Wakati fulani Ali alikuwa na Umar ambapo watu wengine walikuwepo. Ali alipoondoka hapo, mmojawapo wa watu waliokuwepo hapo alianza kumshutumu na kumlaumu kwamba ni mtu mwenye majivuno na mbinasi. Umar akasema: Mtu kama Ali anastahili kujivuna. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, bila ya upanga wake nguzo ya Uislamu haingesimamishwa. Yeye ni hakimu wa daraja la juu sana katika umma huu, ni Mwislamu wa kwanza na wa kuheshimiwa sana.”<sup>47</sup> Mtu aliyekuwa anamshutumu aliuliza kitu gani kilichomzuia yeye (Umar) kumpa uongozi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Umar alijibu: Hatukuupenda umri wake mdogo, na mapenzi yake kwa ukoo wake.”

Hata hivyo, hii haina maana kusema kwamba Umar alikuwa anamtaka ushauri Ali kuhusu mambo yote au alikuwa akifuata maoni yake yote ya dini. Umar alikuwa anajitegemea sana. Wakati fulani alionekana kama vile alikuwa akipingana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifanya kuwa wajibu wa hujaji yeyote ambaye hakufuatana na wanyama wa kuchinja sadaka ya Hija ya ‘tamattu’ (ambamo hujaji huacha kufuata masharti yanayolazimishwa mwanzoni mwa vitendo vya Hija). Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliamuru mtu kama huyo kufanya mizunguko saba kuzunguka Kaaba na kufanya matembezi ya baina ya As-Safa na Marwa mara saba; halafu itakuwa halali yeye kumkurubia mke wake kabla ya kuendelea na Hija yake tena kabla ya kuondoka Arafa.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia alihalalisha ndoa ya Mutta. Umar aliamua kuharamisha pamoja na kumwadhibu vikali yeyote aliyemuoa mwanamke kwa kipindi cha mapatano (Muta). Muslim kwenye *Sahih* yake aliandika kwamba Abu Nudrah alisema ifuatavyo; Ibn Abbas (binamu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) alikuwa na desturi ya kuhalalisha ‘Muta’ na Ibn Zubeir alikuwa na desturi ya kuharamisha. Niliposema hivyo kwa Jabir Ibn Abdallah (sahaba mashuhuri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)), alisema:

<sup>47</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, fasili yake ya *Nahjul Balaghah*, juz. 3 uk. 179.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Yafuatayo yalitokea mbele yangu: “Tulitekeleza ndoa ya Muta wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) .... Umar alipopata ukhalifa alisema: Mwenyezi Mungu alikuwa na desturi ya kumhalalishia Mtukufu Mtume Wake (s.a.w.w.) chochote alichotaka, kupita chochote alichokitaka. Qur’ani iliteremshwa kwa lengo la kulinganaia maisha yetu. Lazima umalize Hijja na Umrah (inayotangulia hija) kama Mwenyezi Mungu alivyoamuru kufanya (bila kuacha masharti ya kawaida kabla ya kwenda Arafa). Acheni kuoa mwanamke kwa ndoa ya Muta. Kama mwanamume alioa mwanamke kwa ndoa ya Muta na akaletwa kwangu, nitampiga mawe (hadi afe).”<sup>48</sup>

Maoni haya ya Khalifa wa pili kuhusu Hija, yanaonekana kупingana moja kwa moja na Qur’ani:

﴿فَإِذَا أَمْتُمْ فَمَنْ تَمَثَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجَّ فَمَا أَسْتَيْسِرَ مِنَ الْهُدَىٰ ﴾  
 فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجَّ وَسَبْعَةٌ إِذَا رَجَعْتُمْ  
 تِلْكَ عَشَرَةً كَامِلَةً ذَلِكَ لِمَنْ لَمْ يَكُنْ أَهْلُهُ حَاضِرٍ الْمَسْجِدُ الْحَرَامُ﴾

“..... na mtakapokuwa salama, basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliywepesi kumpata. Na asiyepata afunge siku tatu katika Hija na siku saba mtakaporudi, hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu.....” (Qur’ani 2:196).

Hadith hii hata hivyo inaonesha wazi kwamba ndoa ya Muta ilikuwa halali wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kwamba hakuhamisha baada ya kuhalalisha. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angeharamisha ndoa ya namna hii, Khalifa wa pili angewakumbusha masahaba kuhusu

<sup>48</sup> Muslim kwenye *Sahih* yake, Sehemu ya 8, uk. 169.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

uharamisho huo. Yeye (Umar) kusema: “Acheni kuoa mwanamke kwa ndoa ya Muta, inatuambia kwamba masahaba walikuwa bado wanaendelea kutekeleza ndoa ya Muta wakati wa uhai wake. Vinginevyo, hangewaamuru kuacha kufanya hivyo. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angekuwa ameharamisha ndoa ya Muta baada ya kuhalalisha, masahaba hawangeendelea na ndoa ya Muta, na Khalifa wa pili hangewaonya na kuwatishia kuwapiga mawe wale walioendeleza ndoa hiyo.

Kuhusu Hija ya ‘Tamattu,’ Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akiwa kwenye Hija yake ya mwisho alisema alipokuwa Makka:

“Kama ningekuwa mwanzoni mwa Hija yangu, nisingefuatana na wanyama wa kuchinjwa kwa sadaka, na ningefanya kuwa Umra (kutenganisha na hija kwa kusitisha masharti ya Ihram). Yeyote ambaye hakufuatana na wanyama wa sadaka, lazima aache kuвая vazi la Ihram na kufanya iwe Umra.” Suraqah Ibn Malik Ibn Jaasham alisimama na akamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): Ni kwa ajili ya mwaka wetu pekee au itadumu milele? Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliweka vidole vyta mikono yake katikati ya kila kimoja na alisema: Umra iliingia kwenye Hija (alirudia tamko hilo mara mbili). Si kwa ajili ya mwaka huu tu. Ni daima milele.”<sup>49</sup>

Hivyo kujamini mno kwa Khalifa wa pili ni msimamo uliomfanya aharamishe Hija ya Al-Tamattu na kuhalalisha kuuawa kwa mtu atakayeo mwanamke kwa ndoa ya Muta. Lakini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaamru Waislamu kutekeleza hija ya Al-Tamattu na kuhalalisha ndoa ya Muta.

Mtu ambaye anajiamini mno kifikira hangetarajiwa kutaka ushauri wa Imam Ali kwa kila tatizo au kufuata maoni yake yote. Hata hivyo alimuona Ali kuwa ni sahaba mwenye utambuzi mkubwa zaidi mionganini wa masahaba na mamlaka ya juu zaidi yanayohusuu dini.

<sup>49</sup> Muslim, *Sahih Muslim*, sehemu ya 8, uk. 172-179.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### MAJADILIANO YAHUSUYO UKHALIFA.

Ukhusiano baina ya Khalifa na Imam uliendelea kuboreka na hatimaye Umar alimuoa Umm Khulthum, binti yake Imam. Licha ya uhusiano kuwa mzuri, historia kwa kadiri nijuavyo haikuandika mazingumzo yoyote baina ya Khalifa na Imam kuhusu Ukhilifa. Lakini Khalifa alipata kufanya mazungumzo mara kadhaa na Abdullah Ibn Abbas (binamu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) kuhusu kutokuelewana baina ya Imam na yeye. Katika mazungumzo haya, Umar alionekana kuridhika na yale yaliyotokea mojawapo ya mazungumzo yalikwenda ifuatavyo:

**Umar:** “.....Jamii ya Maquraishi haikutaka kuwaruhusu nyinyi (Bani Hashim) kuwa na sifa mbili; Ukhilifa na Utume, ili mridhie haki ya jamii yenu. Maquraishi walijichagulia wenyewe. Walifaulu na walifanya uamuzi ulio sahihi.

**Ibn Abbas:** Ulisema kwamba Maquraishi hawakutaka kuturuhusu kuwa na sifa zote mbili yaani ukhalifa na utume. Lakini Muweza wa Yote ali-wazungumzia watu wengine kuwa na chuki' aliposema: “kwa sababu walichukia kile alichokiteremsha. Mwenyezi Mungu, alibatilisha matendo yao mema.” Ulisema kwamba jamii ya Maquraishi walijichagulia wenyewe na kuwa walifaulu na walifanya uamuzi ulio sahihi. Kama wangechagua kile ambacho Mwenyezi Mungu aliwachagulia, haki ingekuwa upande wao, haingejadiliwa wala kuonewa wivu...”<sup>50</sup>

Kwenye mazungumzo mengine Umar alimwambia Ibn Abbas ifuatavyo: Palikuwepo maneno ya hali ya juu sana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) (kuhusu Ali). Lakini maneno hayo hayakuwa na uthibitisho ulio wazi juu ya uongozi wake, wala hayakuondoa vipingamizi vyovyote (kwa wale ambao hawakumuunga mkono). Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa

<sup>50</sup> Ibn Al-Athir, kwenye kitabu chake *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 31

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

anajaribu kumpa Ali uongozi. Alitaka kuandika jina lake alipokuwa mgonjwa mahututi, lakini mimi nilimzuia asifanye hivyo, kwa maslahi ya Uislamu. Kwa jina la Mola wa Kaaba, Maquraishi hawatamuunga mkono kamwe. Kama angepata mamlaka mara tu baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Waarabu wangeasi dhidi yake.” Kwenye mazungumzo mengine, maongezi hayo yalifanyika ifuatavyo:

**Umar:** “Ewe Mwana wa Abbas mtu huyu anafanya jitihadi katika ibada hadi amekonda, akijaribu kuonesha uchaji Mungu.”

**Ibn Abbas:** “Mtu huyu ni nani?”

**Umar:** “Huyo ni binamu yako (Ali)”

**Ibn Abbas:** “Ananufaika nini anapoonesha ucha-Mungu wake?”

**Umar:** “Anataka kujidhihirisha kwa ajili ya ukhalifa.”

**Ibn Abbas:** “Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimteua yeze kwa nafasi ya ukhalifa na hakuipata.”

**Umar:** “Alikuwa katika ujana wake na Waarabu walidhani kwamba alikuwa bado mdogo sana. Lakini sasa amefika umri wa kukomaa. Hukutambua kwamba Mwenyezi Mungu hakumtuma Mtume mwenye umri chini ya miaka arobaini?”

**Ibn Abbas:** “Watu wenye hekima na uamuzi mzuri wanamfikiria yeze kuwa bora na amekomaa kwani Mwenyezi Mungu alinyanyua nuru ya Uislamu. Lakini wanamuona yeze amenyang’anywa na hana bahati.”

**Umar:** Atafika hapo baada ya matatizo, halafu mguu wake utateleza na hataweza kufikia lengo lake. Abdullah utashuhudia hilo. Halafu wote watapambanukiwa. Halafu utaona ukamilifu wa msimamo wa muhajirina wa mwanzoni (masahaba) ambao walichepua uongozi usiwe kwake.”

Kwenye mazungumzo mengine, Umar anaonekana kuwa na majuto kwa jinsi ambavyo Ali alitendewa. Alimwambia Ibn Abbas walipokuwa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wanatembea kwenye mojawapo ya mitaa ya Madina, huku wameshikana mikono:

**Umar:** “Nadhani kwamba Ali hakutendewa haki.”

**Ibn Abbas:** “Ewe Amiri wa Waumini, mrudishieni haki yake.”

Umar aliondoa mkono wake kwenye mkono wa Ibn Abbas, na akaondoka huku anasema peke yake kwa hasira. Halafu alisimama na akamuita Ibn Abbas. Pale Ibn Abbas alipofika karibu, Umar akasema: “Kilichowafanya Maquraishi wasimpe uongozi ilikuwa umri wake. Walidhani alikuwa bado mdogo mno.” Ibn Abbas akajibu: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu wala si Mwenyezi Mungu ama Mtume Wake alimfikiria Ali kuwa mdogo mno walipomuamuru achukue Sura ya ‘Bara-ah’ kutoka kwa mtu wenu (Abu Bakr) alipokuwa anajitayarisha kuondoka kwenda hija na kuitangaza huko.”

Aliposikia hivi, Khalifa aligeuka na kuondoka haraka. Kwenye maongezi mengine na Ibn Abbas, Umar alionekana mtulivu isivyo kawaida. Akamwambia Ibn Abbas: “...unaweza kudhania kwamba Abu Bakr alikuwa wa kwanza kuwasukuma Bani Hashim nyuma. Hakuwa na maana hiyo. Kuna jambo lilitokea na hakuwa na njia zaidi nyingine ya kuchukua ya busara zaidi ya hiyo. Kama hangekuwa na mawazo yake kuhusu mimi angekupa wewe mgawo wako wa uongozi. Kama angefanya hivyo, watu wenu (Maquraishi) hawangewaacheni mfurahie uongozi..... Wanawatazameni nyinyi kama fahali wa ng’ombe amuangaliavyo mchindaji wake.”<sup>51</sup>

<sup>51</sup> Ibn Abil-Hadiid ameyaandika mazungumzo haya katika *Sharh Nahjul-Balaghah*, Jz. 3, uk. 94

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UKUBWA WA SERA YA UMAR

Msimamo wa Khalifa wa pili juu ya Maquraishi na mkondo wake wa fikira ulikuwa na athari nyingi katika matokeo yake. Tunaweza kuona athari zake katika matukio yaliyotokea kabla na baada ya utawala wake ambamo ilielekeza sera za siku zilizofuata za ulimwengu wa Waislamu kwa kiwango kikubwa.

Ushawishi wake ulionekana dhahiri wakati wa kipindi cha Abu Bakr. Yeye alikuwa ndio yuko nyuma ya kuchaguliwa kwake na msaidizi wake mkubwa mwenye nguvu zaidi katika kusimamisha uongozi wake.

Ifuatayo ni Hadith fupi inayoonesha kiwango cha ushawishi wake wakati wa utawala wa Abu Bakr: Uyainah Ibn Hissn na Al-Aqra Ibn Habis walikwenda kwa Abu Bakr na wakasema: Khalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): Kipo kipande cha ardhi kisichotumiwa kwa uzalishaji wowote, hakioti mimea na hakifai. Tunakuomba utupati kipande cha ardhi hicho ili tulime na kupanda mimea humo. Mwenyezi Mungu anaweza akatupatia riziki kuititia humo mnamo siku za usoni.” Abu Bakr aliwataka ushauri masahaba waliokuwa wamemzunguka. Wakati masahaba walikuwa wanampa ushauri kuhusu jambo hilo, yeye alikuwa anaandika waraka, akaweka sahihi yake na masahaba waliokuwa wanashuhudia pia waliweka sahihi zao. Halafu akawapa hao watu wawili nyaraka hiyo.

Kwa kuwa Umar hakuwepo mionganoni mwa masahaba wake watu wawili walikwenda kwake wakampe nyaraka hiyo ili asaini. Kwa kuwa walimkutta anashughulika na kazi ya kumpaka ngamia lami, walimwambia kwamba Khalifa aliwapa nyaraka wampelekee ili aisaini. Walimuuliza kama angependa kusoma kwanza au wao wamsomee. Aliwaambia wamsomee. Baada ya kusikia yale yaliyokuwa kwenye barua hiyo, aliichukua nyaraka hiyo, akaitemea mate na akafuta maandishi yaliyokuwa humo. Watu hao

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wawili walikasirika ghafla na wakasema maneno yasiyopendeza. Aliwaambia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na desturi ya kuwatuliza hao pale ambapo imani ya Uislamu haikuwa na nguvu. Mwenyezi Mungu aliuimarisha Uislamu. “Ondokeni nendeni’ Aliwaambia, “na fanyeni lolote lililoko katika uwezo wenu.” Walikwenda kwa Abu Bakr huku wanalalamika na wakamwambia: “Hatuju mtawala ni nani. Ni wewe au Umar?” Abu Bakr akajibu: “Yeye ni kiongozi kama anataka kuwa.”

Umar alipokwenda kwa Abu Bakr mazungumzo baina yake na Abu Bakr yalifanyika ifuatavyo:

**Umar:** “Niambie kuhusu ardhi ambayo umewapa watu hawa wawili. Ardhi hii ni yako au ni mali ya Waislamu wote?

**Abu Bakr:** “Ni mali ya Waislamu wote.”

**Umar:** “Kitu gani kimekufanya uwape ardhi hii watu hawa wawili na kuwaacha Waislamu walio wengi?”

**Abu Bakr:** “Nilipata ushauri wa masahaba waliokuwapo hapo na wakakubali.”

**Umar:** “Umewaambia Waislamu wote na wakakuruhusu?”

**Abu Bakr:** “Nilikwisha kukuambia kwamba wewe ni mwenye uwezo zaidi kuliko mimi katika kushughulikia mambo ya umma, lakini wewe ulishinda juu yangu na ukafanya mimi Khalifa.”<sup>52</sup>

Si rahisi kuelewa ni vipi Umar alimtarajia Abu Bakr kutaka ushauri kuto-ka kwa Waislmu wote kwa hili jambo la kipande cha Ardhi kisichozalisha

<sup>52</sup> Ibn Abu Al-Hadiid fasili zake za *Nahjul Balaghah*, Juz. 3, uk. 108-109.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

chochote, ambapo hakuwataka ushauri Waislamu wote wakati wa kumpa Abu Bakr uongozi. Uongozi kwa Waislamu ulikuwa ni jambo la muhimu zaidi kuliko kipande cha ardhi, hata hivyo, tukio linatuambia ukubwa wa uathiri wa Umar wakati wa utawala wa Abu Bakr.

Ushawishi wake ulienea si tu katika kipindi cha Abu Bakr. Ulionekana pia wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anaumwa. Wasomaji wa vitabu vya *Sahih wanajua kwamba Mtukufu Mtume* (s.a.w.w.) alitaka kuandika waraka wakati akiwa mgonjwa mahututi ili kuhakikisha kwamba umma hau-tapotdea. Umar alipinga kuandika kwa waraka wa aina hiyo, na akasema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anaweweseka kwa sababu ya maradhi au kwamba alikuwa anaota njozi. Kwa kukataa kwake, Waislamu walinyimwa fursa ya kuipata nyaraka ambayo ilitarajiwa kutia nuru kwenye njia ambayo ingefuatwa na umma katika siku zake za usoni na kuupatia usalama dhidi ya upotofu.

### ALIANDAA MAPEMA KABLA JUU YA MUSTAKABALI WA WAISLAMU.

Ushawishi wa sera yake Umar katika kuelekeza mustakabali wa Waislamiu wote duniani unaweza kuonekana dhahiri kwenye maamuzi yake mengi ambayo aliyafanya akidhani yalikuwa kwa maslahi ya umma. Lakini yali-jaa vitisho na matokeo ya hatari. yafuatayo ni machache tu ya maamuzi hayo:

Aliacha kufuata mbinu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) (ambayo Abu Bakr alifuata) ya kugawa fedha ya hazina ya umma miongoni mwa Waislamu katika usawa unaotakiwa. Umar alipoulizwa kuhusu ugawaji wake usiofuta usawa, alisema, "Sitawagawia sawa wale waliompiga vita Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wale waliomsaidia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuupiga vita upagani." Alitenga dirham elfu tano kama mshahara wa mwaka kwa kila sahaba aliyeshiriki katika Vita vya Badr; na alitenga dirham elfu nne kama mshahara wa mwaka kila sahaba aliyeshiriki Vita vya Uhud. Alimpa kila mtoto wa mtu aliyeshiriki Vita vya Badr dirham elfu mbili

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

isipokuwa Al-Hasan na Al-Husein. Aliwapa hawa watoto wawili mshahara sawa na baba yao kwa sababu ya uhusiano wao na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alitenga dirham elfu kumi na mbili kwa kila mmojawapo wa wake zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Kwa watu ambao walihama kabla ya kutekwa kwa Makka, aliwapa mshahara wa mwaka wa dirham elfu tatu na wale waliokubali kuwa Waislamu baada ya kutekwa Makka aliwapa mshahara wa mwaka wa dirhamu elfu mbili kila mmoja. Halafu akawaweka Waislamu katika kundi moja, kwa kuwapa kila mmoja wao dirhamu ishirini na tano kwa mwaka, au kufuatana na daraja zao za kidini, kusoma Qur'ani Tukufu na jitihada ya kila mmojawao katika kuutetea Uislamu.

Watu wa Yemen na Qaisite ambao walikuwa katika huduma ya jeshi huko Iraq na Syria aliwapa mshahara wa mwaka wa dirhamu kati ya elfu mbili na elfu tatu kila mmoja. Aliweka kiwango chao cha chini cha mshahara cha dirhamu mia tatu kwa kila mmoja kwa mwaka.<sup>53</sup>

Khalifa alitiwa hamasa kwa nia njema alipowapendelea Waislamu wa siku za mwanzo na watetezi wa Uislamu. Alikuwa na sababu ya kuridhisha kabisa katika kuwapendelea ndugu zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na angewapa zaidi ya alivyowapa yeye, kwa sababu walistahili kupewa angalau moja ya sita (1/6) ya moja ya tano (1/5) ya ngawira kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu.

**“Na jueni kwamba ngawira mnayoipata basi Khums (sehemu moja ya tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri, ikiwa nyinyi mmemwamini Mwenyezi Mungu na tuliyoyateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuo, siku yalipokutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”<sup>54</sup>**

<sup>53</sup> Ibn Saad kwenye *Al-Tabaqat* yake, sehemu ya 3, uk. 296-297.

<sup>54</sup> Quran Tukufu, Sura 8:41.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Hata hivyo, ni vigumu sana kuhalalisha kidini upendelepo wake wa watu waliopigana Vita vya Badr zaidi ya wale waliopigana Vita vya Uhud na wa Uhud zaidi ya wale waliokubali kuwa Waislamu kabla ya kutekwa Makka na wale amba walikubali Uislamu wakati wa kutekwa Makka juu ya wale Waislamu waliokubali baada ya kutekwa Makka. Hatuwezi kuhalalisha upendeleo kama huu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyegawa hazi-na ya Kiislamu sawa sawa miongoni mwa Waislamu.

Lilikuwa tamko zuri la kishairi kwa upande wa Khalifa aliposema: "Siwezi kuwalinganisha sawa wale watu waliopigana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wale waliomsaidia katika kuutetea Uislamu, na ingekuwa ukamilifu mkubwa kama angewapendelea Waislamu wa mwanzo kwa kuwatukuza na kuwaweka kiroho juu ya wengine.

Upendeleo katika ugawaji wa hazina pia ungeruhusiwa kama fedha hiyo ingekuwa mali binafsi ya Khalifa. Lakini ilikuwa si haki kuwapa kundi moja zaidi ya mengine kutoka kwenye hazina ambayo inamilikiwa na Waislamu wote sawa sawa. Ruzuku aliywapendelea Waislamu wa siku za mwanzo, ilikuwa inamilikiwa na Waislamu wote na aliichukua kutoka kwao bila ya ruhusa yao.

Kama ruzuku ingekuwa ni stahili ya makundi yaliyopendelewa, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angewapa wao badala ya Waislamu wote vinginevyo angekuwa anagawa miongoni mwa Waislamu wote kile ambacho kilikuwa mali ya Waislamu wa siku za mwanzo.

Hivyo ama tutalazimika kusema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ali-wanyima Waislamu wa siku za mwanzo kutokana na kile walichostahili katika ruzuku au kwamba Umar aliwanyima Waslamu wengi kutoka kwenye haki yao kwenye ruzuku ambayo aliwapendelea Waislamu wa siku za mwanzo. Tuchague nadharia ipi?

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### Matokeo Yasiyopendeza.

Kama ugawaji ulikuwa wa upendeleo, ulikuwa halali au si halali, kwa hakika hali hiyo ilisababisha kutengenezeka kwa tabaka la matajiri miongoni mwa Waislamu. Kundi la wachache lililofaidika kutokana na sera ya ugawaji wa upendeleo, wahusika walipata zaidi kuliko walivyohitaji katika matumizi. Hivyo, wahusika wa watu hao wachache waliweza kuweza fedha zao za ziada kwa kununua na kuuza rasilimali na biashara.

Matokeo yake, jamii ya Kiislamu iligawanywa na kutokeza tabaka la matajiri sana, na lingine ambalo lingeweza kukidhi mahitaji yake bila kutajirika, kundi la tatu, lilinyimwa na kushindwa kupata nguo za muhimu na chakula cha muhimu. Hata hivyo, matokeo ya mgawanyiko huu katika jamii hayakujirokeza kuwa ya kusababisha vurugu wakati wa utawala wa Umar.

Kwa hakika, Khalifa wa pili alishuhudia ishara za uovu wa mgawanyiko huu mwishoni mwa utawala huu, pale aliposema kwa masikitiko ya wazi: "Kama nikipewa fursa ya kufanya tena, ningechukua fedha za ziada za matajiri na kuzirudisha kwa mafakiri." Lakini muda ulikwishamtupa mkono. Alikufa kabla hayarekebisha hali hiyo.

Inafaa kuzingatia kwamba matabaka yaliyopendeleta yalifurahia kile walichokipata na kuamini kwamba walikuwa wanastahili kidini kile wali-chopata. Imam alipokalia kitu cha ukhalifa na akataka kurejesha mbinu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwarudishia walionyimwa kile kilichokuwa chao, wale wachache waliopendeleta wakafanya maasi dhidi yake. Walitumia kila njia iliowezekana kupambana naye ili wadumishe upendeleo wao. Kwa nini isiwe hivyo? Walikuwa wamefurahia haki hiyo ya pekee kwa zaidi ya miaka ishirini, na kwa uelewa wao waliifanya kuwa haki ya msingi.

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

### **WATU WACHOCHEZI KWENYE MFUMO WA UTAWALA WA KHALIFA**

Bila kujali hatari zilizoonekana wazi, Khalifa wa pili aliwapatia kazi kubwa watu wa kutoka kabilia la Qureishi amba walikuwa na tamaa ya makuu kisiasa, na wasio waadilifu kidini. Hali hii ilisababisha matokeo ya hatari baada ya kifo chake.

#### **IBN AL-AAS.**

Alimteua Amr Ibn Al-Aas gavana wa Misri. Kabla hajakubali kuwa Mwislamu, Amr alikuwa na chuki kubwa sana kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na alikuwa anambughudhi sana. Alimkaripia sana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa beti sabini za mashairi.

Kwa kuchelewa sana Amr aliamua kuwa Mwislamu baada ya kuona yajayo siku za mbele kutohana na woga wake na akili yake kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wafuasi wake lazima wangeshinda.

Njama za Amr zilidhiiri baadaye alipokuwa msitari wa mbele katika uchochezi dhidi ya Uthman, baada ya Uthman kumfukuza kazi ya ugavana na kumweka Abdullah Ibn Sarh badala yake. Aliendelea na kampeni ya kumuonea kijicho Uthman hadi alipouawa. Halafu akatumia mauaji ya Uthman kwa malengo yake maovu. Alikuwa mtu wa pili katika kundi la wachochezi lililopigana na Ali, Imam wa haki, kwa kisingizio cha kulipa kisasi kumwagika kwa damu ya Uthman ambaye kifo chake kilisabaishwa na uchochezi wa Amr na wengine kama yeye.

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

### **UKOO WA BANI UMAYYAH ULIINGIA KWENYE UONGOZI**

Khalifa wa pili alimteua Muawiyah, mtoto wa Abu Sufyani, kama gavana wa Damscus. Akamteua kaka yake Yazid Ibn Abu Sufyani gavana wa Jordan. Yazid alipokufa, Khalifa wa pili aliiongoza Jordan kwa utawala wa Muawiya.<sup>55</sup>

Kwa tukio hili, mamlaka ya Muawiyah yalianza kuongezeka kisiasa na kijeshi. Wakati wa utawala wa Umar, Muawiya alikuwa mtu muhimu, hivyo kwamba alitosha aogopwe na watu na kuzingatiwa. Umar alipochomwa kisu, aliwaambia wajumbe waliokuwa kwenye mkutano wa uchaguzi kwa mujibu wa Ibn Abbas alisimulia: “.....Na mkibadilishana wivu na chuki na mkatae kuungana pamoja, Muawiya atapora mamlaka ya ukhalifa kutoka kwenu.”<sup>56</sup>

### **UKOO WA HASHIM WATOLEWA KWENYE UONGOZI.**

Khalifa wa pili hakumweka yejote katika watu wa ukoo wa Hashim kwenye uongozi wowote wenye mamlaka, japoikuwa walikuwa ni watu hodari kama vile Ibn Abbas. Umar aliulizwa kwa nini hakumpa yeye (Ibn Abbas) ugavana wa jimbo japoikuwa anao ujuzi na uwezo. Khalifa alione-sha uelewa wake kwamba Ibn Abbas angeweza kutafsiri aonavyo kanuni za Kiislamu.

Ni dhahiri kwamba, Khalifa wa pili alidhani kwamba Ibn Abbas angeweza kuhalalisha kwa ajili yake mwenyewe au ndugu zake kuchukua kile amba-cho Mwenyezi Mungu aliwatengea ndugu zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye Qur’ani Tukufu ambayo ni moja ya tano (1/5) ya ngawira.

<sup>55</sup> Dkt. Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra*, sehemu ya 1, uk. 118.

<sup>56</sup> Ibn Abu Al-Hadeed kwenye fasili zake za *Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, uk. 62.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Khalifa alionekana kuwaweka watu wa ukoo wa Hashim mbali na kazi za mamlaka makubwa kwenye jimbo lolote la Kiislamu, wasije wakapata umaarufu kwenye maeneo hayo. Alidhani kwamba watu wa majimbo hayo wangeanza kuwatukuza wao kwa sababu walitokana na ukoo wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Akiwa anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.), Khalifa alitarajiwa kutowapa kazi yoyote Bani Umayyah kwenye mfumo wa utawala wake kwa sababu ya upinzani wao kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Pia alitegemea kuwapa ukoo wa Hashim nafasi kubwa katika mfumo wa utawala wake kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kinyume na matarajio yote, Khalifa wa pili hakuwapa kazi kubwa ukoo wa Hashim na akawaingiza Bani Umayyah na akawapa mamlaka makubwa.

Khalifa alimwacha Muawiyah aendelee na ugavana japokuwa alitambua vema kwamba alikuwa na tamaa ya makuu na alivyoshuhudia kukua kwa mamlaka yake. Alimweka katika kazi hiyo katika kipindi cha utawala wake, kinyume na mbinu yake ya kuwafukuza magavana wake aliowateua ye ye mwenyewe na kuwaweka wengine badala yao.

Khalifa alionekana kupendezwa na uwezo wa Muawiyah wa kuendesha mambo, na uhodari wake wa kulinda mipaka yake iliyokuwa jirani na Ufalme wa Rumi. Bado, Umar alikuwa akiamini kwamba ushindi wa Waislamu na kufuzu kwao hakukutegemea mtu au watu, bila kujali uwezo wao, kwani Mwenyezi Mungu huwasaidia Waislamu kwa nguvu ya Uislamu, na si kwa uwezo wa watu. Alimfukuza Khalid Ibn Al-Waliid kutoka kwenye ukamanda wa msitari wa mbele wa Syria baada ya kuwa maarufu sana. Badala yake alimpeleka Abu Ubaidah Ibn Al-Jarrah ambaye alikuwa hajulikani hata kidogo kuwfanya Waislamu watambue kwamba Mwenyezi Mungu angewasaidia wao bila ya kuhitaji uongozi wa Ibn Al-Waliid.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Inawezekana Khalifa aliliwazwa na utiifu wa Muawiya kwake. Hivyo alitaka anufaika kwa akili yake na uwezo wake wa utawala, na Muawiya alikuwa na shaksia kali na hakuna Mwislamu ambaye angediriki kumpa changamoto.

Utii wa Muawiya kwake hata hivyo haungemfanya asahahu yale anayoya-jua kuhusu hatari ya watu wa ukoo wa Muawiya juu ya Uislamu wa baadaye. Kwani Umar alisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kile kilichomtenganisha yeeye na wao. Alimwambia Ibn Abbas kwamba alisikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: “Wana wa Umayah watapanda kwenye mimbari yangu, na niliwaona katika ndoto wanarukaruka kwenye mimbari kama nyani.” Na kuhusu wao aya ifuatayo iliteremshwa “.... na hatukifanya ndoto tuliokuonesha ila ni kuwajaribu watu, na mti uli-olaaniwa katika Qur’ani .....”<sup>57</sup>

Pia Umar alimwambia Al-Mughirah Ibn Shu’bah (ambaye alikuwa na jicho moja): “Mughira, umepata kuona kitu chochote kuitia jicho lako baada ya kulipoteza? Mughira alipojibu kinyume chake, Umar alimwambia: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, wana wa Umayah wataufanya Uislamu upoteze jicho kama lilivyopotea jicho lako. Halafu wataupofusha Uislamu hadi ushindwe kutambua uelekee wapi na uje kutokea wapi.”<sup>58</sup>

<sup>57</sup> Ibn Abdul-Hadiid, fasili zake za *Nahjul Balaghah*, juz. 2, uk. 376. Zipo hadith zaidi zilizoandikwa na Imam Al-Razi kwenye fasili zake za Qur’ani Tukufu, Sura 17, sehemu ya 5, uk. 423-424.

<sup>58</sup> Ibn Abu-Al-Hadiid, Fasili ya *Nahjul Balaghah*, Juz. 2, uk. 277.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UTAWALA WA BANI UMAYYAH ULIKUWA SI WA KUEPUKIIA.

Labda yale aliyoyasikia Khalifa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu wana wa Umayyah yalimfanya aamini kwamba wao kuchukua uongozi ilikuwa ni jambo lililokwishawekewa hatima na lisingeepukika. Kwa hiyo alijiruhusu kutembea kwenye njia hii iliyowafikisha Umayyah kwenye mamlaka haraka. Hivyo, alifanya hivyo akiwa anaridhia yale aliyodhani kuwa ni matokeo yaliyokwishapangwa.

Huenda imani yake kwamba kufika kwa Bani Umayyah kwenye kazi ya mamlaka kubwa ni mpango ambaa haungezuijika ulimfanya amwambie Ibn Abbas kwamba Ali ataufikia ukhalifa baada ya ghasia kubwa, halafu atateleza na hatafanikisha lengo lake. Halafu akamwambia Ibn Abbas: Abdullah utashuhudia, na mambo yatakuwa wazi kwa kila mtu mwenye akili, halafu utaona ukamilifu wa msimamo wa muhajirina wa mwanzo ambaa walichelea Ukhilifa usimfikie yeye.”

Kama mambo yalivyo, kufikia kwa dhuriya wa Umayyah kwenye mamlaka likawa jambo linaloelewka na lililotarajiwa baada ya wao kuwa sehemu muhimu sana ya Dola ya Waislamu. Kuwepo kwa Muawiya na wengine wa aina yake kwenye nafasi za mamlaka ilitarajiwa kuwa kipingamizi muhumu ambacho Ali angekabiliana nacho kama angeweza kupata mamlaka.

Kwa kweli, matatizo na vipingamizi ni hali iliyokuwa inazidi kuongezeka na kulundikana wakati wa utawala wa Umar na iliendelea kuongezeka baada ya kifo chake hadi ikawa hakuna uwezekano wa Ali kutawala kwa amani.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Hali hii haikusababishwa na udhaifu wa Ali, bali ilisababishwa na matukio yaliyotokea kabla yeye hajapata mamlaka ya uongozi. Matukio yankeeupukwa, kwani matukio hayo yalitengenezwa na mtu na utashi wake na hayakuwa hatima iliyowekwa na Mwenyezi Mungu. Kama Umar hangemweka Muawiya kwenye nafasi ya mamlaka au kama hangemuweka kwenye uongozi Muawiya hangekuwa kipingamizi kwa Ali, kwani bila ugavana wa Syria, Muawiya angekuwa mtu wa kawaida.

### KILICHOMAANISHWA NA UBASHIRI WA KINABII

Jambo alilosema Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika ubashiri wake ambamo aliwaona dhuriya wa Umayyah wanapanda kwenye mimbari ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), lilikuwa onyo kwa umma kwamba ufuate njia ambayo haitaufikisha kwenye tukio hilo lilllobashiriwa. Lakini umma ulifuata njia ambayo iliwafikisha Bani Umayyah kwenye mimbari hiyo.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliuambia umma kwamba mjukuu wake Al-Husein angeuawa, na kwamba Ali angepigana na wale waliovunja mkataba, kundi la wakosaji na Khawariji (Waliojiten). Pia alimtaarifu Ali kwamba umma ungemsaliti yeye. Alimwambia Zubeir kwamba angepigana na Ali bila haki. Alimtaarifu mama wa Waumini, Aisha kwamba angebewekewa na mbwa wa Al-Houab, ambapo angekuwa anacheputa na kuacha njia ya haki na kufuata njia ya uovu. Pia aliwaambia Waislamu kwamba kundi la wenye shari lingemuua Ammar Ibn Yasir.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwajulisha Waislamu matukio yote haya kwa kuwajulisha kwamba yalamuliwa na Mwenyezi Mungu. Hakuwa na maana ya kuwaambia Waislamu kwamba matukio yaliyotabiriwa hayankeeupukwa na kwamba utashi wa mwanadamu haungekuwa kipengele cha kuyasababisha au kuyazuia.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Kama angekuwa ana maanisha hivyo basi wasiotii, watenda dhambi, wauaji wavunja mikataba na wakosaji hawangelaumiwa. Alichotaka kusema Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni kwamba matukio haya yaliyotarajiwa, ambayo yalimhuzinisha, yangetokea kwa sababu ya maamuzi yasiyo sahihi ambayo yangefanywa na umma, au na baadhi ya viongozi wao.

Msimamo wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika kuyabashiri matukio haya ni sawa na msimamo wa bingwa wa tiba anayemtahadharisha mtu ambaye amedhoofu maungo yake kile kitakachomtokea kama hatachukua hatua za kinga ambazo alimwelezea.

Kama mgonjwa akikataa kuchukua dawa za kinga, halafu akaugua, ugonjwa wake hautakuwa matokeo ya majaa liwa wala si kwamba matokeo hayo hayangeepukwa. Ugonjwa wake ungekuwa matokeo ya kushindwa kwake mwenyewe na uamuzi usio sahihi.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alibashiri matukio haya mabaya ambayo alitegemea na akaueleza umma hatua sahihi za kuzuia yasitokee, yaani kuambatana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya watu wa Nyumba yake. Aliwaambia Waislamu kwamba wao wangeshikamana na vitu hivi viwili wangekuwa na uhakika wa usalama wa umma dhidi ya matukio mabaya na uovu wa kila aina. hata hivyo, umma haukuzingatia onyo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wala haukutambua vyema uzito na ukubwa wa matamko yake. Umma ulifuata njia ya uovu ambayo ulielekeza kwenye matukio hayo maovu.

Kwa hili ninaamini kwamba Khalifa wa pili alikosea alipomwambia Ibn Abbas kwamba mwanga wa nuru ungetokeza kwa ye yeyote mwenye akili na kwamba Ibn Abbas mwenyewe angekuwa shahidi na kugundua ukamilifu wa msimamo wa muhajirina wa siku za mwanzo ambapo waliuchepua Ukhilifa usimfikie Ali.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Ukweli ni kwamba kile kilichomtokea Ali hakikuthibitisha ukamilifu wa msimamo wa muhajirina wa siku za mwanzo. Badala yake, kilithibitisha kwamba walifanya kosa lenye gharama na la kuogofya. Kama hawangechepua ukhalifa kutoka kwa Ali baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), mawingu hayangetanda kwenye upeo wa ujuzi wake wala vipingamizi na matatizo ni mambo ambayo hayangelundikana kwenye utendaji wake.

Ali angefika kwenye utawala wa amani hata baada ya ukhalifa kukwepeshwa mara mbili kutoka kwake. Kama Khalifa wa Pili angetumia mvuto wake mkubwa katika kuwatiisha Maquraishi na kuwaelekeza kwa Ali, Ali angefanikisha lengo lake. Endapo hangewaingiza Bani Umayyah katika mfumo wa utawala wake na kuepuka kutengeneza tabaka la watu wa kupendelewa na masahaba wa mwanzo kuitia mgawo wake wa kupendelea wa hazina ya umma, Ali hangepata matatizo makubwa.

Hata baada ya matukio yote haya kutokea, Ali angeweza kuwa na utawala wa amani kama Umar angemtaja ye ye kuwa mrithi au angeunda Jopo la mkutano wa uchaguzi la wajumbe wenye msimamo mzuri kwa Ali, badala ya Uthman. Kama Ali angefaulu kufika kwenye mamlaka kwa amani, Waislamu wangeepushiwa ghasia zote za kupima imani ambazo zilielekwa baada ya kifo cha Uthman.

\* \* \* \*

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### SURA YA ISHIRINI.

#### JOPO LA MKUTANO WA UCHAGUZI.

Khalifa wa pili aliuawa wakati anasali na kumwomba Mola Wake Mlezi kwenye msikiti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Madina. Kwa mauaji yake maisha ya mmoja wa wajenzi wakuu wa historia yalikoma. Utawala wake haukuzidi miaka kumi, bado ulijaa matukio ambayo yalibadilisha mkondo wa historia. Maisha yalikoma, lakini mvuto wake haukukoma. Hakufa kabla ya kuusukuma umma kwenye mimba ya matukio muhimu ya siku za usoni, ufunguo wa matukio ni Jopo la Mkutano wa Uchaguzi ambalo alil-iunda wakati yu mahututi kitandani.

Muslim kwenye *Sahih* yake ameandika kwamba Abdullah Ibn Umar, alimwambia baba yake: “Wanadai kwamba hutaki kumtaja mrithi wako. Kama unaye mchungaji wa kondoo au ngamia wako, na akarudi kwako na kuwaacha bila mchungaji, utamuona ni mzembe. Kuchunga watu ni muhimu zaidi kuliko kuchunga wanyama.”

Abdullah alisema: “Maneno yangu yalionekana kumpendeza. Aliweka kichwa chake chini kwa muda mfupi, halafu akakinyanya akisema: “Kama sitamtaja mrithi nitakuwa ninafuata mfano wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). kama nikintaja mrithi, nitakuwa ninafauta mfano wa Abu Bakr.”<sup>59</sup>

Khalifa, mwanzoni alikataa kumtaja mtu yeoyote. At-Tabari na Ibn Al-Athiir walismulia kwamba Umar alishauriwa kumteua mtu mmoja baada yake, lakini akasema: “Kama Abu Ubaidah Ibn Al-Jarrah angekuwa hai, ningemteua yeye. Kama Mwenyezi Mungu akiniiuliza, nitasema: “Nilimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Wako akisema: Abu Ubaidah ni

<sup>59</sup> Muslim kwenye *Sahih* yake, Sehemu ya 2, uk. 206.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

mwaminifu wa umma huu.”

Kama Salim huria wa Abu Hudhaifa angekua hai, ningemteua yeye. Kama Mwenyezi Mungu ataniuliza, nitamwambia Yeye: “Nilimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Wako anasema: “Salim anayo mapenzi makubwa kwa Mwenyezi Mungu.” Umar alikataa kumteua mwanae Abdullah kwenye kazi hiyo kubwa, akasema: “Nitawezaje kumteua mtu ambaye alishindwa kumtaliki mke wake, au alisema hajui kumtaliki mke wake?”<sup>60</sup>

### WATEULE SITA.

Kwa mara nyingine, alishawishiwa kumteua mrithi, lakini alikataa, akasema: Baada ya kusema neno langu la mwisho niliamua kumchagua mtu mwenye sifa ya juu katika kuuongoza umma huu kwenye njia iliyonyooka (huku akimnyooshea kidole Ali). Halafu nikazirai, na wakati nipo kwenye kuzirai, nilimuona mtu ameingia kwenye bustani. Aliokota kila tunda bichi na lenye kuiva akaondoka nayo, na akayaweka chini yake. Nikatambua kwamba Mwenyezi Mungu aliamuru kitu fulani na Atashinda. Sikutaka kuchukua wajibu wake, niwe hai au maiti. Ninawapendekeza hawa watu sita ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alithibisha kwamba ni kutoka watu wa Peponi: Ali, Uthman, Abdul-Rahman, Saad Ibn Abu Waqass, Zubeir Ibn Al-Awam na Talha Ibn Ubeidullah. Watu hawa wanatakiwa kumteua Khalifa kutoka mionganii mwao. Kama wakimteua mmojawao, mnatakiwa kushirikiana naye na kumsaidia.”

Wakati Ali na ndugu zake walipoondoka nyumbani kwa Khalifa, Abbas (ammi yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) alimshauri Ali asiingie kwenye jopo hilo. Ali akasema: “Sipendi mfarakano; Abbas akajibu: Na utapata kile usichokipenda.” hata hivyo, Khalifa hakufafanua kuhusu jambo hili, wala hakubainisha mbinu ambayo ingetumika kumteua Khalifa kutoka kwa hawa watu sita.

<sup>60</sup> Ibn Al-Athir, *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 34. (mchapishaji Dar Al-Kitab Al-Arabi, Beirut, Lebanon).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### MAELEKEZO YA UTARATIBU.

Mnamo siku ya pili, Khalifa alibainisha mbinu ya uchaguzi. Aliwaambia waliokuwepo katika hao watu sita: Nikifa, kutaneni kwa siku tatu, na Suheib ndiye atakayeongoza Swala. Itakapofika siku ya nne muwe mmek-wisha chagua kiongozi; Abdulah Ibn Umar lazima ahudhurie mikutano yenu kama mshauri, lakini hana sehemu katika ukhalifa. Talha ni mwen-zenu katika jambo hili (hakuwepo). Kama akija katika kipindi cha siku tatu, mchukueni awe na nyinyi. Kama siku tatu zikipita bado hajafika, fanyeni uamuzi wenu ....Ninafikiria mmoja tu kati ya watu wawili, Ali na Uthmna, atakuwa Khalifa. Kama Uthmna akichaguliwa, udhaifu wake ni huruma yake. Kama Ali akichaguliwa, dosari yake ni uchangamfu wake. Na ni mwenye sifa bora zaidi kustahili kuongoza watu kwenye njia iliyonyooka.”

Khalifa alimuamuru Abu Talha (kutoka watu wa Madina) achague watu kamsini kutoka watu wa Madina na wawe walini wa Jopo la Mkutano wa uchaguzi, na kusisitiza kwamba wachague Khalifa kutoka mionganii mwao baada ya maziko ya Khalifa. Aliwaambia wao: “Kama watano kati ya sita wanakubaliana, na mmoja anakataa muueni. kama wanenye wanakubaliana na wawili wakakataa, waueni hao wawili. Kama wanagawika sawa kwa sawa, mfanyeni Abdulah Ibn Umar kama mpatanishi. Kama hawatakubaliani na upatanishi wake, muungeni mkono Abdul-Rahman Ibn Auf na waueni wengine kama hawakubaliani na wanachokubali watu.”<sup>61</sup> Imesimuliwa pia kwamba alisema: “Kama siku tatu zinapita kabla hawa-jaamua nani atakuwa kiongozi, waueni wote na Waisilamu wachague kiongozi wenyewe.”<sup>62</sup>

<sup>61</sup> Ibn al-Athiir, *Al-kamil*, sehemu ya 3, uk. 35.

<sup>62</sup> Ibn Saad, *Al-Tabaqat*, sehemu ya 3, uk. 342.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Wajumbe wa Jopo la Mkutano wa Uchaguzi walikutana baada ya maziko ya Khalifa. Walibishana na hawakukubaliaana. Imetaarifiwa kwamba Talha alijiondoa kwenye kundi la kumuunga mkono Uthman na Zubeir alijiondoa kwenye kundi la kiumuunga mkono Ali na Saad Ibn Abu Waqass akajiondoa kwenye kundi la kumuunga mkono Binamu yake Abdul-Rahman. Kama hii ilikuwa kweli au si kweli, ingejulikana sana kwamba Abdul-Rahman alishauri kwamba ajitoe kwenye kinyang'anyiro, na kwamba apewe mamlaka ya kuchagua mmoja kati ya wawili. Ali au Uthman. Uthman aliukubali bila kusita. Ali hakumruhusu hadi alipomfanya atoe kiapo cha kuwa mkweli, asifuate utashi binafsi, asipendee ndugu na kujitahidi kufanikisha maslahi ya umma. Abdul-Rahman alikuwa shemeji yake Uthman (alimuona dada yake Uthman Umm Khuluthumu).

Saad Ibn Abu Waqass alimshauri binamu yake Abdul-Rahman ajichague mwenyewe. Lakini Abdul-Rahman alisema: "Sipendi mtindo huo kwa sababu kwenye ndoto yangu usiku wa jana niliona mbuga iliyojaa majani mabichi. Ngamia mzuri aliingia humo na alipita bila kula jani lolote. Ngamia mwingine alipita humo na alifanya kama alivyofanya ngamia wa mwanzo. Ngami wa tatu na mkubwa alifuata na alifanya kama alivyofanya ngamia wa mwanzo. Halafu ngamia wa nne aliingia kwenye mbuga na alianza kula yale majani kwa ulafi. (Alifasili ngamia wanen kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na makhalifa watatu baada yake, na mbuga ya majani kuwa hazina ya umma).

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mimi sitakuwa ngamia wa nne," Alisema: "Mtu atakayemrithi Abu Bakr na Umar kamwe hataweza kuwardhisha watu."

Abdul-Rahman aliwataka ushauri marafiki zake akiwaauliza angemchagua nani. Maquraishi walio wengi walimtaka Uthman, masahaba mashuhuri wasio Maquraishi walimtaka Ali. Alikutana na Ali na Uthman kila mmoja kwa wakati wake. Mnamo siku ya tatu Abdul-Rahman alinua kulifikisha jambo hili kwenye hatima yake. Watu walikusanyika kwenye Msikiti

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Mtukufu majira ya Asubuhi. Msikiti ulijaa watu.

Abdul-Rahman alisimama na akasema: “Watu wageni waende kwenye miji yao. Nipeni ushauri. Ammar Ibn Yasir alisimama na akamwambia yeye: “Kama ukitaka usitokee mfarakano mionganoni mwa Waislamu. Mchague Ali.” Al-Miqdadi Ibn Al-Aswad, sahaba mwiningine mashuhuri alimuunga mkono Ammar, akasema: “Ammar amesema kweli. Kama ukimteua Ali tumesema: Tumesikia na tunatii.”

Masahaba hao wawili walipingwa na Abdullah Ibn Abu Barh, ambaye alimwambia Abdul-Rahman: “Ukitaka Maquraishi wasifarakane, mchague Uthman.” Abdullah Ibn Abu Rabi’ah kutoka ukoo wa Makhzoom alimuunga mkono akasema: “Umesema kweli. Kama Abdul-Rahman akimchagua Uthman, tutasema: “Tulisikia na tutatii.” Ibn Abu Sarh alitabasamu lakini Ammar alimwambia: “Ni lini ulikuwa mwaminifu kwa Waislamu?” (Ibn Abu Sarh alikubali kuwa Mwislamu wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Halafu akaikimbia imani. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaamuru Waislamu wamuue popote watakapo muona).

Ukoo wa Hashim walizungumza na vivyo hivyo ukoo wa Umayya walizungumza. Ammar aliongea na watu akasema: “Enyi watu, hakika Mwenyezi Mungu ametuenzi sisi kwa kutupatia Mtukufu Mtume Wake (s.a.w.w.) na akatuimarisha sisi kwa dini Yake. Wapi unakotaka kuugeuzia ukhalifa kutoka kwenye Nyumba ya Mtume wenu?” Mtu kutoka ukoo wa Makhzuum alimpinga kwa kusema: “Ewe mwana wa Sumayah, wewe ni nani kuwaambia Maquraishi nini cha kufanya kwa ajili yao wenywewe?” Saad Ibn Abu Waqas akamwambia binamu yake Abdul-Rahman: Limalize jambo hili kabla watu hawajafarakana.”

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### **ABDUL-RAHMAN ALIMCHAGUA UTHMAN.**

Abdul-Rahman alimuita Ali. Akam wahidi kwamba angekuwa Khalifa kama angekubali sharti jipya: "Utamtii Mwenyezi Mungu na umuhidi Yeye kwamba utafuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kufuata nyayo za Makhalifa wawili (Abu Bakr na Umar) baada yake?" Ali akajibu: "Nitafuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na nitafuata elimu yangu iliyo bora na kujitahidi kadiri ya uwezo wangu wote."

Kwa kuwa hakukubali sharti alilopewa, Abdul-Rahman alimgeukia Uthman na kumpa sharti hilo hilo, na Uthman alikubali sharti hilo. Inasemekana kwamba Abdul-Rahman alimpa kila mmoja wao sharti hilo mara tatu, Ali alikataa na Uthman alikubali.

Baada ya tukio hilo, Abdul-Rahman alinyanya kichwa chake na kuangalia kwenye dari ya Msikiti akisema: "Mwenyezi Mungu, awe shahidi yangu, nimehamisha wajibu kutoka kwangu na kumpa Uthman." Halafu akatoa kiapo chake cha utii na uaminifu kwa Uthman.

Ali alitamka maneno machache kuhusu tukio hilo akasema: "Hii si mara ya kwanza nyinyi kushirikiana katika usaliti dhidi yetu, watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa jina la Mwenyezi Mungu, umempa yeye uongozi ili tu baadaye aurudishe kwako. Mwenyezi Mungu anao uwezo wa kubadilisha hali hiyo." Halafu akawageukia wote wawili Abdul-Rahman na Uthman akasema: "Mwenyezi Mungu na awapeni masaibu ya uadui wa daima milele." Abdul-Rahman alijibu kwa hasira akasema: "Ewe Ali, usijitafutie matatizo juu yako (akimkumbusha kwamba Khalifa alimwagiza kumuua yejote asiyekubaliana na mawazo ya wenzie)."

Ali aliondoka baada ya kutoa kiapo chake cha uaminifu kwa Uthman, akisema: "Kile kilichoandikwa kuhusu matukio yaliyowekewa muda

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

mwisho wake utafika.”

Ammar alimwambia Abdul-Rahman: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, umemwacha mtu wa ukweli na maamuzi sahihi!” Al-Miqdad Ibn Al-Aswad alimuunga mkono Ammar akasema: Wallahi, sijapata kamwe kushuhudia jambo lolote linalofanana na hili ambalo wamefanyiwa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) baada ya kifo chake. Nimeshangazwa na Maquraishi ambao wamemuacha mtu ambaye halin-ganishwi na yeote kwa ujuzi, ucha-Mungu, na kupenda haki. Kama nitakuwa na wanaoniunga mkono, nitapigana na Maquraishi sasa, kama nilivyopigana nao kwenye vita vya Badr na Uhud.” Abdul-Rahman aka-jibu: “Ewe Miqdad, muogope Mwenyezi Mungu. Ninahofia kwamba wewe utasababisha mfarakano mionganoni mwa Waislamu.” Al-Miqdad ali-jibu kwa hasira, akasema: “Yule ambaye anasababisha mfarakano ni yule anayefuata maslahi yake binafsi.”<sup>63</sup>

### MAONI YA KUZINGATIA.

Kama ambavyo tumewasilisha matukio ya Jopo la Mkutano wa Uchaguzi kwa ufupi, ingefaa kutoa maoni yafuatayo:

1. Khalifa wa Pili alisema kwamba kama Abu Ubaidah Ibn Al-Jarrah na Salim mtumishi wa Abu Hudhaifa, wangkuwa hai, angemteua mmoja wao, kwani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Abu Ubaidah ndiye mwaminifu wa umma huu, na Salim anayo mapenzi makubwa na kwa Mwenyezi Mungu.” Alikataa kumteua Ali ambaye kuhusu yeche alisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) matamko mengi sana. Matamko hayo hayakuhusu sahaba mwingine yoyote.

<sup>63</sup> Ibn Al-Athiir, kwenye *Al-Kamil* yake, sehemu ya 3, uk. 32-35, na Ibn Abu Al-Hadiid kwenye fasili zake za *Nahjul- Balaghah*, Juz. 1, uk. 63-65.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Tudhanie kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba Abu Ubadiyah alikuwa mtu mwaminifu katika umma huu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia alisema: "Ali anatokana nami na mimi natokana naye na hapana yejote anayestahili kuniwakilisha mimi isipokuwa Ali."<sup>64</sup>

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumpa mamlaka Abu Ubaidah wala yejote kutoka mionganoni mwa masahaba kuwasilisha amana alizokuwa nazo za watu wa Makka wakati alipokuwa anahama Makka kwenda Madina (hijiriyah). Alimkabidhi kazi hiyo Ali tu kwa niaba yake. Pia alimkabidhi kuwasilisha Sura ya Bara'ah kwa mahujaji, na alimuagiza aichukue Sura hiyo kutoka kwa Abu Bakr baada ya kumpa mamlaka ya kuwasilisha. Jibril alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Hapana mtu mwengine atakayewasilisha kwa niaba yako isipokuwa wewe au mtu kutoka katika kundi la watu wa Nyumba yako."<sup>65</sup>

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa mujibu wa Umar, alisema: "Salim anayo mapenzi makubwa kwa Mwenyezi Mungu," lakini hakusema kwamba Mwenyezi Mungu anampenda Salim. Khalifa huyu ambaye alikuwa katika dakika za mwisho wa uhai wake, angekumbuka kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Mwenyezi Mungu ameniamuru mimi kuwapenda watu wanne na ameniambia kwamba Yeye anawapenda watu hawa." Halafu akasema: "Ali ni mmojawapo," akarudia usemi huo mara tatu. Endapo Khalifa hakusikia tamko hili kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hakika alisikia kutoka kwake, pale Khaybar tamko la muhimu zaidi. Jeshi la Kiislamu chini ya uongozi wa Abu Bakr na Umar lilishindwa kuteka ngome ya Khaibar. Katika kipindi kile cha hatari, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Nitampa bendera kesho mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.) na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.) wanampenda yejote. Mwenyezi Mungu atafungua ngome

<sup>64</sup> Al-Tirmidh, *Sunan Al-Tirmidhi* sehemu ya 5, uk. 300, hadith Na. 3803.

<sup>65</sup> Al-Hakim, *Al-Mustadirak*, sehemu ya 3, uk. 51.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

hizo kwa kutumia mikono yake.”<sup>66</sup>

Umar alikuwa na desturi ya kusema kwamba hakutamani uongozi kamwe isipokuwa siku hiyo, ili kwamba maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yaweze kuwa ni kwa ajili yake yeye. Siku iliyofuata Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpa Ali Ibn Abi Talib bendera, baada ya kumtibu macho yake mawili kwa muujiza, yaliyokuwa na maradhi ya kuvimba. Na mnamo siku hiyo Muweza wa Yote alifungua milango ya ngome kwa kutumia mikono ya Ali.

Hata hivyo, wala si matamko haya ama matamko mengine muhimu kuhusu Ali yangeweza kumshawishi Khalifa aliyeokuwa katika dakika zake za mwisho wa uhai wake kumteua Ali kushika kazi hiyo kubwa.

### JE HADITH HII NI SAHIHI?

Ni vigumu sana kuamini kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba Abu Ubaidah alikuwa mtu wa kuaminika zaidi katika umma. Abu Ubaidah hakuwa mwaminifu zaidi ya Ali au Abu Bakr au Umar. Inawezekana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitamka maneno hayo kwa utani. Labda alisema kwamba Abu Ubaidah ni mmojawapo wa watu waaminifu katika umma huu na Umar hakuelewa tamko hilo, na hali hii ingekuwa ya kawaida, Umar na mwanae walipitiwa na kwa makosa waliona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Maiti ataadhibiwa kwa sababu ya kuliliwa sana na familia yake.” Muslim kwenye *Sahih* yake ameandika kwamba Aisha alikanusha tamko hilo la kusingiziwa, akasema: “Umar na mwanae wala si waongo ama kutoaminika. Lakini mara nyingine sikio husikia vibaya. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema tu kwamba Mwenyezi Mungu huongeza adhabu ya asiyemini anapokufa na kuliliwa sana na

<sup>66</sup> Al-Bukhari, *Sahih Al-Bukhari*, sehemu ya 5, uk. 171, na Muslim, kwenye *Sahih* yake, sehemu ya 15, uk. 170-171.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

familia yake.” Halafu alikariri Aya ya Qur’ani:

**“Na hakuna nafsi itakayoadhibiwa kwa dhambi za nafsi nyingine.”**  
**(sehemu ya 6, uk. 230-232).**

### JE, MTU ASIYE QUREISHI ANGEWEZA KUWA KHALIFA?

2. Khalifa aliyejikuwa katika dakika za mwisho za uhai wake kwa mfululizo alikuwa anatetea kwamba ukhalifa ulikuwa haki ya pekee ya Maquraishi. Alirudia usemi huo mara kwa mara wakati wa utawala wake na Abu Bakr. Bado alitamani Salim, mtumishi wa Abu Hudhaifa, angekuwa hai. Kwani angemteua yeche kuwa mrithi wake, anbapo Salim wala hakuwa Quraishi ama Mwarabu. Mtu huyu alitoka Ustokhar. Alifanya mtumwa na kuuzwa mara kadhaa. Hatimaye akamilikiwa na Abu Hudhaifa, na kwa sababu baba yake hakujulikana, akapewa jina la Salim, mtumwa wa Abu Hudhaifa.<sup>67</sup>

Hivyo, Khalifa huyo aliyejikuwa mahututi alikuwa tayari kumteua Salim ambaye wala hakuwa Quraishi, ama Mwarabu, lakini hakuwa tayari kumteua Ali ambaye alikuwa binamu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamfanya kuwa ndugu katika udugu wa Kiislamu.

### MASAHLABA WA MADINA WAACHWA KABISA.

3. Khalifa huyo mahututi aliteua masahala sita kutoka kwenye kundi la Maqurasihii kuwa wajumbe wa Jopo la Mkutano wa Uchaguzi. Aliwapa haki ya kugombea ukhalifa wao peke yao, na aliwapa haki ya kumchagua Khalifa wao peke yao. Aliwaamuru Waislamu wote wawafuate wao na

<sup>67</sup> Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra*, sehemu ya 2, uk. 37.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kuzingatia uamuzi wao. Umma, kufuatana na msimamo wake haukuwa na haki ya kukataa lolote lililoamuliwa na wajumbe hao. Katika wajumbe sita aliongeza wa saba (Abdullah, mwanae) kama mshauri na mpatanishi, na mshauri huyo alikuwa Quraishi pia.

Khalifa hakumpa sahaba yejote kutoka Madina kazi ya kupiga kura au kama mshauri. Khalifa si Khalifa wa Maquraishi tu. Yeye ni Khalifa wa Waislamu wote. Watu wa Madina hawakupewa haki ya kumchagua Khalifa kutoka mionganini mwao, lakini walikuwa na haki sawa na ile ya Maquraishi ya kumchagua Khalifa kutokana na Quraishi yejote.

Ni dhahiri kwamba, Khalifa huyu mahututi aliwaengua watu wa Madina kwa sababu: Watu wa Madina walio wengi walikuwa wanamuunga mkono Ali. Kama angejumuisha wajumbe kutoka mionganini mwao, wangeweza kumpa Ali ushindi katika uchaguzi na Umar hakutaka itokee hivyo. Mbinu aliyotaka wajumbe wa mkutano wa uchaguzi wafuate katika kuteua Khalifa kwa wazi kabisa ilikuwa na mwelekeo wa jambo hilo kuwa kinyume na Ali. Wajumbe sita ambao ndio tu aliwapa haki ya kugombea uongozi na kumchagua kiongozi, kila mmoja wao alikuwa na mwelekeo wake uliojulikana kwa Khalifa. Uthman alikuwa anautaka ukhalifa, Abdul-Rahman alikuwa shemeji yake, Saad Ibn Abu Waqass alikuwa binamu yake Abdul-Rahmna, na hangempinga. Talha Ibn Ubaidullah alitokea kwenye ukoo wa Abu Bakr ambao ulikuwa na uhasama na Ali kwa sababu ya ushindani baina yake na Khalifa wa kwanza. Hivyo wajumbe walio wengi wa Jopo la Mkutano wa Uchaguzi walikuwa hawampendi Ali.

Ali aligundua kuwepo kwa tatizo hili alipomsikia Khalifa wa pili anatoa maelekezo kwa wajumbe sita kuhusu mbinu ya kumteua Khalifa. Alipoondoka nyumbani kwa Umar, Ali aliwaambia ukoo wa Hashim: “Endapo watu wenu (Maquraishi) watapewa heshima, hamtaufikia uongozi kamwe.” Alimwambia mjomba wake Al-Abbas: “Mjomba, uongozi tayari umekwisha ondoshwa kutoka kwenu..... Umar alimlinganisha Uthman na mimi na akawaagiza watu kuwafuata walio wengi mionganini

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

mwa wajumbe wale sita. Endapo wanagawanyika sawa kwa sawa, aliwaambia Waislamu wamuunge mkono Abdul-Rahman, na Abdul-Rahman ni shemeji yake Uthman. Saad ni binamu yake Abdul-Rahman, na hawawezi kупingana wao kwa wao, kama wajumbe wengine wawili wataniunga mkono mimi, hawatanufaika.”<sup>68</sup>

Kama Khalifa angeongeza wajumbe wengine zaidi wachache ambao hawakuwa na malengo yao, Ali angeshinda uchaguzi. Wakati anaelekea kufa, Khalifa wa pili alirudia mara kwa mara kusema kwamba Ali alikuwa na sifa bora zaidi za kumstahilisha kuongoza umma kwenye njia iliyonyooka mionganoni mwa wajumbe sita. Ushahidi huu unaendana na usemi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao alitangaza kwamba Ali kamwe hakuachana na Qur’ani Tukufu na kwamba alikuwa mshirika mkubwa wa ukweli.

Kama Khalifa aliyeoonesha imani yake kubwa kwa Ali, alitarajiwa kuten-geneza mazingira ya kumwelekeza Ali kwenye ushindi kwa kuwashauri wajumbe wa mkutano wa uchaguzi kumuunga mkono yeye endapo pange-tokea mgawanyiko. Kinyume na mategemo hayo, Khalifa wa pili aliwaambia wajumbe wa mkutano wa uchaguzi kukubali upatanishi wa mwanae endapo wangegawanyika sawa kwa sawa. Kama wangekataa upatanishi wake, Khalifa aliamuru wamfuate Abdul-Rahman Ibn Awf (badala ya Ali). Inajulikana kwamba, kitendo cha Khalifa hakikulingana na kutangaza uthibitisho wake kuhusu Ali.

### **ABDULLAH IBN UMAR.**

4. Tunaona katika kuingizwa kwa Abdullahi Ibn Umar kwenye Jopo la uchaguzi kama mshauri na mpatanishi kuwa hiyo ni dosari nyingine. Sahaba huyu mwadilifu alikuwa kwa mujibu wa ushahidi wa baba yake,

<sup>68</sup> Ibn Al-Athiir, *Al-Kamil* sehemu ya 3, uk. 33.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

hawezি kufanya uamuzi kuhusu kumwacha au kuendelea kuishi na mke wake. Mwanamume ambaye hana uwezo kiasi kile hangefanywa kuwa mshauri au mpatanishi kwenye jambo kubwa kama la ukhalifa ambamo hatima ya Uislamu inategemea.

Udhaifu na chuki ya Abdullah kwa Ali ni hali iliyodhihirika baada ya kupita miaka baada ya kifo cha baba yake. Dunia yote na Waislamu, isipokuwa Muawiya na wafuasi wake wa Syria, ilimchagua Imam Ali baada ya kifo cha Uthman. Lakini Abdullah alikataa kupiga kura ya kuchagua Imam. Utawala wa Imam ulidumu takriban miaka mitano na Abdullah aliendelea kukataa kumtii Ali kwa kipindi chote cha utawala wake japokuwa alikuwa anafahamu aliyyoyasema Mtukufu Mtume kuhusu yeye. Abdullah huyu huyu baadaye alikuwa tayari kutoa kiapo cha kumtii Yaziid Ibn Muawiya. Muslim kwenye *Sahih* yake aliandika ifuatavyo:

“Abdullah Ibn Umar alikwenda kwa binamu yake Abdullah Ibn Mutii wakati Vita vya Al-Harrah vilipotokea (kwenye vita hivi mji mtakatifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulinajisiwa na jeshi la Yaziid, na watu wake waadilifu waliuawa kiholela). ‘Tandika mto chini kwa ajili ya Abu Abdul-Rahman (Abdullah Ibn Umar);’ Abdullah Ibn Mutii aliiwaambia wasaidizi wake. Lakini Ibn Umar alimwambia; Sikuja hapa ili niketi chini. Nimekuja ili nisimulie hadith. Nilimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: Yeyote anayeonesha msimamo wa wazi wa kutomtii (Khalifa ambaye anamwia utii wake) atakutana na Mwenyezi Mungu mnamo Siku ya Hukumu bila udhuru wowote. Na yeyote anayekufa bila kumtii (Khalifa) anakufa akiwa kafiri.”<sup>69</sup>

Kwa kusimulia hadith hii, Ibn Umar alikuwa anajaribu kumzuia Ibn Mutii asimuasi Yaziid, akamshawishi kutoa kiapo cha utii na uaminifu kwa Khalifa fisadi. Hii inaonesha kwamba Ibn Umar yeye mwenyewe alikuwa anafikiria kwamba angekutana na kifo cha kikafiri kama hakutoa kiapo cha

<sup>69</sup> Muslim, *Sahih Muslim* Sehemu ya 12, uk. 40.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

utii kwa Yaziid. Lakini Yaziid alikuwa ndiye muuaji wa Imam Husein na mchafuzi wa utakatifu wa Madina na mvurugaji wa Kaaba. Lakini Abdullah alikuwa haogopi kufa kifo cha kikafiri alipokataa kutoa kiapo cha utii na uaminifu kwa Ali, yule ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimfanya ndugu katika ‘udugu wa kiroho.’

Ille namna sahaba huyu alivyoyaelewa maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) inashangaza. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye maelezo yake yaliyosimuliwa, alikataza kuasi dhidi ya Khalifa mwadilifu ambaye muasi alikwisha toa kiapo cha utii na uaminifu. Uasi wa aina hiyo, kama mambo yalivyo, hausameheki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini Ibn Umar ali-fikiri kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anawaamuru Waislamu kumtii na kutoa kiapo cha utii kwa mtawala mwovu.

Kutomtii Khalifa wa aina hiyo si tu inasameheka kwa Mwenyezi Mungu lakini pia Anapendezwa na kitendo hicho. Kwa kweli, Uislamu unawaamuru Waislamu kuwapindua watawala wao waovu na hukataza kutoa kiapo cha utii na uaminifu kwao. Qur’ani Tukufu inasema: “**Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.**<sup>70</sup>” Msimamo wa Abdullah kwa matukio haya unaondoa shaka kwamba kuingizwa kwake kwenye Jopo la Uchaguzi la wajumbe sita ilikuwa ni mafanikio zaidi kwa Uthman na matatizo zaidi kwa Ali.

### **HIVI, UISLAMU UNAKATAZA UPINZANI?**

5. Khalifa huyu anayekaribia kufariki aliwaelekeza Waislamu kumuua yejote mionganoni mwa wajumbe wa Jopo la uchaguzi ambaye hatakubaliana na walio wengi. Kama wajumbe wangegawanyika sawa kwa sawa kundi la Abdul-Rahman ndilo lifuatwe. Wengine watatu pia wangeuawa kama hawangefanya uamuzi wowote katika kipindi cha siku

<sup>70</sup> Qur’ani Tukufu (58:32).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

tatu baada ya maziko yake, na kuwapa uhuru Waislamu wachague Khalifa wenye. Hali hii inashangaza, kwani Uislamu hauruhusu kumuua muumini kwa sababu amekataa kukubaliana na walio wengi au na Abdul-Rahman au na Khalifa. Uislamu unatakasa maisha ya waumini wote. Na mtu anayemuua muumini analaaniwa milele daima. Qur'ani tukufu inasma:

**“Na mwenye kumuua muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahanamu humo atadumu; na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa.”<sup>71</sup>**

Kama kumuua muumini yejote ni kosa kubwa, kumuua mmojawapo wa wajumbe sita ni kosa kubwa zaidi, kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) (kwa mujibu wa taarifa ya Umar) aliwafikiria wao ni wanaotokana na watu wa Peponi.

Kwa melekezo yake, Khalifa wa pili alidokeza pendekazo la kumuawa Ali kama angepingana na walio wengi mionganii mwa wajumbe sita au Abdul-Rahman. Lakini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Mwenyezi Mungu mpende yejote anayempenda Ali na mchukie yejote anayemchukia ye.” Hivyo, chuki dhidi ya Ali, licha ya kumuwa, peke yake ni kuchokoza hasira za Mwenyezi Mungu.

Ni vigumu kuelewa ni vipi Umar alipendekeza kuuawa masahaba mashuhuri au mtu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kutokukubaliana naye tu au na Abdul-Rahman. Waislamu walikuwa na desturi ya kutokukubaliana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) naye hakuwaadhibu. Umar mwenye kama akihitilafiana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na alimzuia asiandike wasia na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwaadhibu. Hivi matakwa ya Umar au Abdul-Rahman yalikuwa yametakasika zaidi kuliko ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?

Labda Khalifa alifikiria kwamba kukubalika kwa uteuzi wake alikopokea

<sup>71</sup> Qur'ani Tukufu; 4:93

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kutoka kwa Waislamu mwanzoni mwa utawala wake ndio alikuwa amepe-wa mamlaka yasiyo na masharti na mipaka kufanya lolote alilofikiria ni kwa maslahi ya Waislamu. Juu ya hili, alitoa hatua kali ambazo zingechukuliwa kwa wajumbe sita. Lakini ni dhahiri kwamba kitendo hiki kilikuwa kosa.

Khalifa aliyeuleliwa na Khalifa mwingine, na ambaye uteuzi wake ulikubaliwa na Waislamu, angeweza kuwa na haki ya kuteua mrithi wake au kudhibiti uhuru wa waliomchagua au kuwanyima baadhi ya haki zao. Lakini kukubalika huko hakumpatii yeye haki ya kumuua sahaba mashuhuri, ambaye alitangazwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni mmojawapo wa watu wa Peponi, kwa sababu tu ya kutofautiana naye kuhusu maoni yake. Waislamu hawana haki ya kumpa mamlaka yeye kutenda yale ambayo yameharamishwa kwake na kwao pia. Waislamu hawana haki ama kwa pamoja wala kama mtu binafsi, ya kumuua mtu ambaye uhai wake umetakaswa na Mwenyezi Mungu. Kuchaguliwa kwa Khalifa kamwe si uhuru wa kufanya atakavyo. Kwa usahihi zaidi ukhalifa unashurutishwa kuambatana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na vitu vyote hivyo vime-haramisha kumuua muumini.

### ONYO LISILOTILIWA MAANANI.

6. Ndoto mbili zilizotokea wakati wa kipindi cha Mkutano wa Uchaguzi:

Ndoto ya Khalifa aliyekuwa mahututi ambaye aliona katika ndoto yake mtu anayeingia bustanini na akachukua matunda yote yaliyoiva na mabichi, akayaweka matunda hayo chini yake.

Ndoto ya Abdul-Rahman ambamo aliona ngamia mzuri wa kupendeza anaingia kwenye mbuga ya majani mabichi. Ngamia huyo alipita majani hayo bila kula hata kidogo. Ngamia wa pili na wa tatu walifuata na wali-

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

fanya kama alivyofanya ngamia wa kwanza. Halafu aliingia ngamia wa nne ambaye alikula majani hayo kwa ulafi.

Waotaji wote wa ndoto hizo walielewa kutoka kwenye ubashiri wao kwamba Khalifa anayekuja hatakuwa mwadilifu kuhusu hazina ya umma. Watu hao wawili wangeshawishiwa na hizo ndoto zao za kushangaza kumchagua mtu mwenye uadilifu mkubwa kwa kazi ya ukhalifa, ambaye hangejiruhusu kuchukua kile kisichokuwa chake. Lakini waotaji hao wawili wa ndoto hizo, hawakutilia maanani onyo hilo. Walichukua hatua ambazo zilimuengua mtu aliye mwadilifu sana miongoni mwa masahaba na wakamchagua mtu mwenye sera za kutia hasara kwenye hazina ya umma.

Historia imeandika matamko mawili yaliyofanywa na Umar kuhusu Ali na Uthman. Kuhusu Ali alisema: “Wewe ni mtu mashuhuri aliyeje! Kama utapewa uongozi, utauongoza umma kwenye njia iliyonyooka.” Kuhusu Uthman alisema; “Natarajia Maquraishi watakupatia wewe ukhalifa kwa sababu wanakupenda wewe. Halafu utawabeba watu wa nyumba yako kwenye shingo za Waarabu kwa kuwapa hazina ya umma. Halafu kundi la mbwa mwitu la Waarabu kutoka sehemu mbali mbali litakusanyika na kukuua wewe.”<sup>72</sup>

Kama tukiuamini utabiri huu tunashangaa ni vipi huyu Khalifa mahututi alimpendelea Uthman badala ya Ali. Kwa kuwa aliamini au alituhumu kwamba Uthman angefuata sera za kusababisha hasara kwenye hazina ya umma, angemuengua kutoka kwenye Jopo la Uchaguzi. Kwa bahati mbaya, huyu Khalifa wa pili si tu kwamba alimjulisha yeye, lakini maelekezo yake kwa wajumbe wa jopo la uchaguzi yalikuwa na dokezo la kumpendelea Uthman na kwa hiyo ushindi ulimwelekea yeye.

Hivyo Khalifa alifanya kila jinsi alivyoweza kutangaza na kumfagilia njia ya ushindi yule ambaye aliyemtuhumu na kumtweza yule aliyemwamini.

<sup>72</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, kwenye fasili zake za *Nahjul Balaghah*.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Uaminifu wa Ali kuhusu hazina ya umma ulionekana dhahiri kwa Umar na masahaba wengine. Hakuwa na tamaa ya makuu na utajiri wa mali haukumvutia yeye. Tofauti na masahaba wengine kama Talha, Zubeir, Abdul-Rahman, Uthmna na masahaba wengine ambao waliohodhi mamilioni ya dirham, Ali aliishi maisha ya wastani. Katika kipindi chote cha uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na makhalifa wawili wa mwanzo, Ali alifahamika kuishi maisha ya kiucha-Mungu na kiuwanachuo.

Onyo ambalo Umar na Abdul-Rahman walilipokea kuitia ndoto zao za ajabu lingewashawishi kumteua Ali badala ya Uthman, kwa uongozi. Kwa bahati mbaya walitekeleza vinginevyo.

**MASHARTI YASIYO NA MAANA**

7. Masharti ya Abdul-Rahman ambayo yalimtaka yule ambaye angekuwa Khalifa wa Tatu kufuata maagizo ya Makhalifa wawili wa mwanzo, yalikuwa nyongeza isiyo na uhalali. Wajibu wa kila Khalifa ni kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hawajibiki kufuata nyayo za aliyemrithi isipokuwa yule anayemrithi awe ameteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Inapokuwa Khalifa mpya ni mjuzi zaidi wa yule aliyemrithi na anaona baadhi ya matendo yake kuwa yenye makosa au taratibu zake zimekosewa, atawajibika kutokukubaliana naye.

Kuweka miongozo ya Makhalifa wawili wa mwanzo katika uwiano sawa na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtume Wake Mtukufu (s.a.w.w.) ni kosa kubwa. Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni chenye kweli tupu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amepewa kinga ya kutokutenda dhambi katika maelekezaji yake ya kidini. Kwa upande mwingine, makhalifa wawili wa mwanzo walikuwa kama masahaba wema kwa ujumla wa masahaba wote, hawakuwa na kinga ya kutenda makosa. Kuweka matendo yao na maneno yao katika usawa mmoja na Qur'ani Tukufu na

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kweli huo ni uasi katika dini.

Ukhalifa unaweza kutegemezwa kwenye uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kutegemea Wahyi wa Mwenyezi Mungu. Pia unaweza kutegemea Wahyi wa Mwenyezi Mungu. Pia unaweza kutegemezwa kwenye uchaguzi wa kuchaguliwa na watu wengi au watu wachache ambaao ni mashuhuri au kuteuliwa na mrithi wa au aliyechaguliwa au aliyeteuliwa na mrithi wa aliyeteuliwa.

Maneno na matendo ya Khalifa aliyechaguliwa (au aliyeteuliwa na mrithi wa aliyechaguliwa) hayawezi kuwa sharia ya Kiislamu iliyotakatifu. Kabla ya kuchaguliwa kwake, angekuwa kama Waislamu wengine wema, ambao hawana kinga ya kufanya makosa. Ataendelea kuwa kivyo baada ya kuchaguliwa. Kuchaguliwa kwake hakubadilishi tabia yake; wala kumfanya yeze kuwa na ujuzi mkubwa endapo alikuwa na ujuzi mdogo.

Kwa kiasi cha juu sana, anaweza kuwa *mujitahid* (mwanachuo anayeweza kuunda maoni yake kwa kujitegemea kuhusu sharia ya Kiislamu). Hapana mwanachuo mwingine wa Kiislamu anatakiwa kumfuata yeye, na inaruhusiwa kwa maamuma kumfuata mwanachuo na si yeye.

Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) (kwa kutegemea Wahyi wa Mwenyezi Mungu) angemteua Khalifa, Waislamu wote wanetakiwa kumfuata mteule. Kumkataa kwao mteule wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ingekuwa sawa na kumkataa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Makhalifa wawili wa mwanzo hawakuteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Khalifa wa kwanza alichaguliwa kwa wingi wa kura za masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na Khalifa wa pili aliteuliwa na Khalifa wa kwanza. Hapana yeote kati ya hao anaweza kufikiriwa kuwa zaidi ya mujitahidi, ambaye hana kinga ya kukosea.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Khalifa anayewafauata wao hatakiwi kufuata nyayo zao.

Hii inaonesha kutokuthibitika na upuuzi wa sharti la Abdul-Rahman ambalo alilipachika kwa yule ambaye angekuwa Khalifda wa tatu. Kichekesho hicho kilifika kwenye kilele pale ambapo Abdul-Rahman alijaribu kukamilisha mwambatano wa Ali na njia ya Makhalfa wawili ambao walikuwa na desturi ya kukimbilia kwa Ali kama mamlaka katika sharia ya Kiislamu.

Zaidi ya hayo, haingewezezana kwa mtawala yejote kufuata miongozo ya makhalfa wawili wa mwanzo. Khalifa wa pili hakukubaliana na Khalifa wa kwanza katika mambo mengi, mionganii mwao ilikuwa mbinu ya kugawa hazina ya umma wa Kiislamu. Abu Bakr alifuata mbinu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na aligawa fedha kwa Waislamu bila upendeleo. Umar aliwapanga masahaba kwa makundi na aliyapendelea baadhi ya makundi zaidi ya mengine.

Na kwa kutofautiana kwa Makhalfa hao wawili wao kwa wao, ikawa hakuna uwezekano wa Khalifa yejote kukubaliana na makhalfa hao wawili hata kama angetaka kufanya hivyo.

Kwa hili, tunafikiri kwamba tamko la Abdul-Rahman si tu kwamba lilikuwa nyongeza katika dini na bidaa kwenye Uislamu, lakini pia ni jambo ambalo halingeteklezeka.

Abdul-Rahman kwa kweli mambo yake yalikuwa ya kifalme akamteua mfalme. Khalifa wa kwanza akamteua Khalifa wa pili na hakumtaka afuate nyayo zake. Alimtarajia kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu tu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wala Khalifa wa pili hakuwelekeza Abdul-Rahman kukamilisha mwambatano wa Khalifa anayefuata nyayo zake.

Sidhani kwamba Abdul-Rahman alikuwa hatambui ubatili wa sharti lake alilolidhihirisha. Alikuwa sahaba mashuhuri na hakuwa mjinga kiasi hicho.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Vinginevyo, Khalifa wa pili hangempa mamlaka muhimu kiasi hicho. Ukweli ni kwamba aliongeza sharti lake lisilo halali kwa sababu tu ya kumwengua Ali. Ilikuwa vigumu yeye kumpendelea Uthman na si Ali bila ya kisingizio. Wala si Uthman ama sahaba mwingine yeyote alikuwa na kila alichokuwa nacho Ali chenyе sifa bainifu katika ujuzi, jitihada katika Uislamu, na udugu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuwa mwanamume wa kwanza kuwa Mwislamu. Licha ya sifa zote hizi bainifu Abdul-Rahman alinuia kumpa uongozi Uthman badala ya Ali japo alikuwa na sifa zisizweza kulinganishwa na za mtu mwingine. Uthman ni shemeji yake Abdul-Rahman na kumpa uongozi ni mpango wenye manufaa.

Uthman anatarajiwa kulipa fadhila kwake kwa kumteua kuwa mrithi wake. Kwa upande mwingine Ali, si mtu wa mipango. Uongozi wake utafunga mlango kwa Maquraishi wote wenye tamaa ya makuu. Watoto wake wanatarajiwa kumrithi yeye. Wao ni wajukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kwa ushahidi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wao ni viongozi wa vijana wa Peponi.

Lakini inawezekana Abdul-Rahman ampendelee Uthman zaidi kuzidi Ali bila kuhatarisha hadhi yake kama sahaba mtenda haki na mwadilifu? Alihitaji udhuru, na alivumbua sharti lake kama udhuru. Alimpa Ali uongozi, halafu kwa Uthman, akiwawekea sharti la wao kuambatana na mwenendo wa Makhalifa wawili wa mwanzo, akitambua kwamba Ali angekataa sharti kama hilo lisilo na uhalali. Lakini siri hiyo haikufichwa sawa sawa. Haraka sana Ali alimshutumu, akasema: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, umempa Uthman ukhalifa kwa sababu tu unatarajia baadaye ataurudisha kwako....”

## UHALALISHO KWA KUTUMIA HADITH.

Inawezekana kusemekana kwamba sharti la Abdul-Rahman linahalalishwa na matamko mawili yanayohusishwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Hadith ya kwanza ifuatayo: “Fuateni mfano wa watu wawili baada yangu, Abu Bakr na Umar ...”

Lakini yale yaliyomo kwenye hadith yanathibitisha kuwa hakuna ukweli ndani yake kwa haya yafuatayo: Hadith inaonesha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikwishawateua Abu Bakr na Umar kuwa warithi wake, ambapo ni jambo linalojulikana sana katika historia kwamba kati ya watu hawa wawili hapana aliyeulewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Abu Bakr alipokuwa anabishana na watu wa Madina huko Saqifa aliwaambia: “Waarabu hawatakulali uongozi wowote isipokuwa utokane na Maquraishi,” na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Maimam watatokana na Maquraishi.” Kama hadithi iliyosimuliwa ingekuwa ya kweli, angeitumia hiyo kama ushahidi wa dhahiri.

Abu Bakr aliwataka Waislamu huko Saqifa kumchagua ama Abu Ubaidah au Umar. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angewataka Waislamu kufuata mfano wa watu hao wawili baada yake, Abu Bakr na Umar, angemkataza Abu Bakr kuwataka Waislamu wamchague Abu Ubaidah kwa sababu ni yeze tu (Abu Bakr) na Umar waliolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Abdul-Rahman alilaumiwa na kushutumiwa na Ali, Ammar na Al-Miqdad akiwa na nia ya siri katika sharti lake. Kama hadithi hii ingelikuwa ya kweli, angejitetea mwenyewe kwa kuinukuu.

Tena, kama hadith ingekuwa ya kweli, Ali angekubali sharti la Abdul-Rahman. Kwa mujibu wa hadith, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwataka Waislamu kuwafauta Makhalifa wawili. Na Ali alikuwa mtiifu sana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.). Kukataa kwa Ali sharti lililowasilishwa ni uthibitisho kwamba alikuwa haijui hadithi hii. Lakini alikuwa ndiye mjuzi zaidi katika mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Zaidi ya hayo, kushindwa kwa masahaba wote kusimulia hadith hii wakati wa Kongamano la Uchaguzi, inaonesha kwamba hapana sahaba ye yeyote aliyejua hadith hii. Hali hii peke yake inaifanya hadith hii kuwa si ya kuaminika.

Ni ukweli unaojulikana sana katika historia kwamba ukhalifa ulikuwa haki yake ya pekee na kwamba alikataa kutoa kiapo cha utii na uaminifu kwa Abu Bakr na aliendelea na kukataa kwake hadi kifo cha mke wake Fatima. Kama tamko liliosimuliwa likuwa la kweli, Ali wala hangedai haki kama hiyo ama kukataa kutoa kiapo cha utii kwa Abu Bakr.

Hadith ya pili ambayo inaweza kutajwa kwa ajili ya kuthibitisha sharti la Abdul-Rahman ni kama ifuatayo: "Hakika Mwenyezi Mungu anaweka ukweli kwenye ulimi kwa Umar na moyoni mwake ...." kama maneno haya yangetuwa ya kweli ingetuwa lazima kwa Khalifa ye yeyote baada yake kufuata.

Labda Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitamka maneno haya yaliyosimuliwa wakati fulani ambapo Umar alitoa maoni mazuri, na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anashuhudia ukamilifu wa maoni ya Umar kwenye fursa hiyo. Hivyo, tamko husika lisieleweke kama tamko la jumla kama tangazo, kwa sababu zifautazo:

Kama tukiichukua hadith kama tamko la jumla, tutatakiwa kuamini kwamba Umar alikuwa na kinga kamili ya kutenda kosa kwa maneno ama matendo, ama kwenye mambo ya dunia au ya dini. Lakini Waislamu walio wengi hawaamini kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alikuwa na kinga dhidi ya kukosa. Wanaamini kwamba anayo kinga ya kutenda kosa katika maelekezo ya dini tu!

Sababu nyingine ya kukataa hadithi hii ni kwamba Umar alitenda makosa mara kadhaa. Hakuwa mkweli alipokanusha kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ibn Hishamu kwenye kitabu chake cha Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na waandishi wa historia wengine wengi walisimulia

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

kwamba Umar alisema mnamo siku hiyo: "Hakika wapo wanafiki, wanadai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametawafu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, atarudi kama alivyorudi Musa (a.s.) na atakataa mikono na miguu ya watu wanaodai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametawafu."

Al-Bukhari kwenye *Sahih* yake ameandika kwamba Abu Bakr alifika hapo siku hiyo ambapo Umar alikuwa anazungumza na watu. Alimwamuru Umar kukaa chini, lakini Umar alikataa kufanya hivyo. Watu wakamwacha Umar na wakamgeukia Abu Bakr naye aliwaambia: "Yeyote miongoni mwenu aliyekuwa anamuabudu Muhammad lazima aelewe kwamba Muhammad ametawafu. Na yeyote ambaye alikuwa anamuabudu Mwenyezi Mungu aelewe kwamba Yu hai na kamwe hafi. Muweza wa Yote alisema: "Na Muhammad ni Mtume tu; Mitume wa kabla yake walipita." baadaye Umar alisema: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, niliposikia Abu Bakr anakariri Aya hii, miguu yangu ililegea. Nilianguka chini niliposikia Abu Bakr anakariri kwamba Muhammad alikwishatawafu."<sup>73</sup>

Kweli haikuwa na Umar alipompinga Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa anajaribu kuandika wasia wake. Alichokoza hasira ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kwa upinzani wake umma ulinyimwa nyaraka ambayo ilitegemewa kutia nuru njia ya kufuatwa na umma baada yake.<sup>74</sup>

Kwa hakika Umar alikosea sana kwenye fursa hii. Alimkataza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuandika wasia wake, na hiyo ni dhambi kubwa. Alihoji uwezo wa kiakili wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao Qur'ani Tukufu inasema: "**Na Mtume hasemi kwa matamanio yake ya binafsi. Ni Wahyi tu ndio unaopelekwa kwake.**"<sup>75</sup>

Tena Qur'ani inatangaza: "**Enyi mliaoamini, mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake .....**"<sup>76</sup>

<sup>73</sup> Ibn Hishamu, Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sehemu ya 2, uk. 656; na *Sahih Al-Bukhari*, sehemu ya 6, uk. 17.

<sup>74</sup> Al-Bukhari, *Sahih Al-Bukhari*, sehemu ya 1, uk. 39.

<sup>75</sup> Qur'ani Tukufu (53:3-4)

<sup>76</sup> Qur'ani Tukufu (59:7).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Umar hakuwa na ukweli mnamo siku ya Al-Hudaibiyah. Waandishi wa historia wanakubaliana kwa pamoja kwamba Umar alibishana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akakataa kutekelezwa kwa mpango wa amani baina ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Qureishi makafiri. Umar alisema baada ya hapo: "Nitatoa Sadaka, nitafunga saumu, nitaswali na kuwaachia huru watumwa kama malipo ya makosa ambayo niliyafanya siku hiyo.

Khalifa wa pili hakuwa sahihi kuunda Jopo la Uchaguzi. Kukataa kwake kumteua Imam Ali na maelekezo yake kwa wajumbe wa kongamano la uchaguzi la kumteua mtu ambaye angekuwa Khalifa wa tatu lilimpa Uthman mamlaka na ukhalifa ukawekwa mikononi mwa ndugu wa ukoo wa Umayya ambao waligeuza ukhalifa kuwa udikteta na utawala wa kurithiana.

Haya ni machache tu mionganini mwa fursa mbali mbali ambazo Khalifa wa pili aliziwekea msimamo wa kimakosa. Kwenye ulimi wa Umar mara nyingi hapakuwepo na neno sahihi wala ukweli haukuwepo moyoni mwake. Hivyo, hizi hadith mbili haziwezi kuhalalisha sharti lililovumbuliwa na Abdul-Rahman.

### KUJITOLEA KWA KIPEKEE KWA ALI.

Namna ambavyo Ali alijiendesha mwenyewe katika kipindi cha hali ya hatari ya Jopo la Uchaguzi haingelinganishwa katika historia ya Uislamu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ulikuwa mfano wa hali ya juu wa uadilifu, uimara na kushikamana na ukweli. Uongozi wa Dunia ya Waislamu alipewa yeye, na bei yake ilikuwa ni bei hiyo na akakataa uongozi kwa sababu yaliwekwa masharti ambayo yalimtaka aingie kwenye upotofu na kuacha kiasi fulani cha kanuni zake. Hapana jaribio la ukubwa wowote ambalo lingemvutia mtu huyu mkweli. Ukhalifa kwake haukuwa ndio mwisho wa kila kitu; hiyo ilikuwa ni jinsi ya kuanzisha haki na kuyaelewa maadili ambayo alikuwa anafungamana nayo na ambamo ali-

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

weka maisha yake kwani masikio yake yalisikia wito wa Muhammad.

Alikasirishwa na kuundwa kwa Jopo la Uchaguzi na alilionia kama tukio la kisirani lililojaa hatari. Muundo wa Jopo la Uchaguzi ulikuwa na hatima ya kumweka Uthman kwenye mamlaka. Hii ingewaweka ndugu zake wenye tamaa ya makuu na wasio waadilifu kwenye kazi za changamoto, na kuwafanya watafute kazi ya juu kabisa kwa namna yoyote ile.

Baada ya kuona hatari hizi, Imam aliamua kujaribu kuwazuia kwa kuutafuta ukhalifa.

### UTABIRI WA KWELI.

Historia iliandika kwamba Ali alitoa matamko mawili ya ubashiri katika kipindi cha jopo la uchaguzi akitabiri matukio yaliyokuwa yametarajija, kama vile aliquwa anasoma kutoka kwenye kitabu.

At-Tabari alisimulia kwamba Ali alizungumza na ammi yake Abbas baada ya Khalifa wa pili kutoa maelezo yake kuhusu mbinu ya kumteua Khalifa wa Tatu. “Ninajua kwamba watamteua Uthman” alisema, “Na ataleta bidaa na mabadiliko yasiyokubalika. Na endapo nitaishi, nitakukumbusha. Uthman akifa au akiuawa, ukoo wa Umayya utaufanya ukhalifa uzunguke mionganoni mwao. Na endapo nitakuwa bado hai, wataniona mimi ninafika mahali ambapo wao hawataki.”

Pia Ali alizungumza na wajumbe wa jopo la uchaguzi pale walipokuwa wanajaribu kumteua Khalifa mpya: “Sifa zote Anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye kutoka mionganoni mwetu amemchagua Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutoka mionganoni mwetu, na akamtuma kwetu kama Mtume. Sisi ni watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), chanzo cha heshima, usalama wa watu wa duniani, na kimbilio la wale watafutao usalama (dhidi ya upotofu).

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

“Tunayo haki. Endapo tunapewa hiyo haki, tutaichukua; kama tukinyang’anywa tutakaa nyuma hata kama safari itakuwa ndefu. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angetupatia sisi maelekezo, tungetimiza. Kama angetuambia tuchukue hatua yoyote, tungepigania jambo hili hadi tufe. Hapana mtu atakayeitika haraka kuliko mimi kuelekea kwenye wito ulio adilifu au wema kwa ndugu.

“Sikilizeni maneno yangu na mfahamu uwasilisho wangu. Uongozi wenu baada ya Jopo hili la Uchaguzi (endapo mnashindwa kumteua kiongozi mwenye sifa zinazostahili) utakabiliwa na mapambano makali sana. Mikataba itavunjwa na mapanga yatachomolewa hadi hapo mshikamanao wenu utakapofika mwisho. Baadhi yenu mtakuwa Maimam wa mabadiliko ya itikadi, baadhi watakuwa wafuasi wa watu wa ujinga.”<sup>77</sup>

Utabiri huo wote ulifanikiwa. Uthman aliteuliwa. Alileta mabadiliko yasiyokubalika, na hii ilisababisha kifo chake. Kwa kifo chake cha kikatili, umoja wa Kiislamu ulikoma. Imam Ali (a.s.) alichaguliwa baada yake, lakini masahaba mashuhuri walivunja mikataba yao na yeze baada ya kutoa kiapo cha utii kwake. Uongozi ulikabiliwa na mapambano makali. Mapanga yalichomolewa na vita vingi vilipiganwa. Viongozi wa madiliko ya itikadi, upotofu na ujahiliya walijitokeza, na umma walio wengi walifauata.

Akitarajia matukio haya mabaya, Imam alilazimika kuingia kwenye jopo la uchaguzi, akijaribu kila awezavyo kuzuia matukio tarajiwa yasitokee. Hali hii ndio iliyomfanya adharau maoni ya ami yake Abbas ambaye alimshauri asiingie kwenye jopo la uchaguzi.

Kuwa mjumbe wa jopo la uchaguzi ni jambo lililomshushia hadhi yake, lakini alilazimika kuwajibika. Kama hangeingia kwenye jopo la uchaguzi, angewapa wajumbe wengine sababu ya kumwengua au wangeelewa

<sup>77</sup> Ibn Al-Athir, *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 37.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kukataa kwake kuwa ndio ushahidi wa yeye kutokuvutiwa na kugombea uongozi.

Kukataa kwa Imam Ali kuingia kwenye jopo la uchaguzi ni hali ambayo ingemweka Imam kwenye nafasi ambayo hangeweza kujitetea kihistoria. Hii inaweza kutufanya tufikirie kwamba alijinyang'anya uongozi mwenyewe. Ambapo uongozi huo ulikuwa wa kwake. Tunaweza tukafikiria kwamba hakujitahidi vyta kutosha katika kuepusha matukio mabaya ambayo alikuwa anayatarajia.

Zaidi ya haya kukosa kuwepo kwake kwenye jopo la uchaguzi, ni kitendo ambacho kingefikiriwa kuwa ni msimamo wa kukataa wajibu na kwa hiyo kuwatia moyo wajumbe wa jopo hilo kumchagua mtu mwengine. Hivyo, angeshiriki pamoja nao wajibu wa kutenda kosa hilo.

Ulikuwa wajibu wa Ali kuhudhuria jopo hilo la uchaguzi na kuwakumbusha wajumbe wake kuhusu haki yake kwa uongozi na kwamba watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni chanzo cha heshima, usalama wa watu wa duniani dhidi ya upotofu, na kimbilio la yejote anayetaka usalama huo. Na hii ndio ilikuwa maana ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwaamuru umma kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na watu wa Nyumba yake, na akawafananisha na Safina ya Nuhu.

Imam alitimiza wajibu wake kwa kuhudhuria jopo la uchaguzi. Aliwaonya wajumbe hao kuhusu matokeo ya hatari kama wakimchagua mtu asiyefaa. Aliwakumbusha kuhusu haki ya Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa uongozi, haki ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwaambia ndugu zake wapiganie.

Historia inasema kwamba mazungumzo baina ya Ali na wajumbe wa kongamano la uchaguzi yalifanyika na yalikuwa kama ifuatavyo:

**Imam:** "Katika jina la Mwenyezi Mungu; ninawaulizeni: Yupo yejote mionganoni mwenu isipokuwa mimi aliyeitwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

ndugu wa kiroho?”

**Wajumbe:** “Hakuna isipokuwa wewe.”

**Imam:** “Yupo mionganini mwenu isipokuwa mimi ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kuhusu yeye: Yeyote ambaye mimi ni ‘*Mawla*’ wake, Ali ni ‘*Mawla*’ wake?

**Wajumbe:** “Hapana yeyote”

**Imam:** “Hivi yupo yeyote mionganini mwenu ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: Wewe kwangu ni kama alivyokuwa Harun kwa Musa (a.s.), lakini hapatakuwepo na Mtume baada yangu?”

**Wajumbe:** “Hakuna.”

**Imam:** Hivi yupo mionganini mwenu isipokuwa mimi aliyekabidhiwa Sura ya Bara’ah, na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema kuhusu mtu huyo: hapana yeyote atakayewasilisha kwa niaba yangu isipokuwa mimi mwenyewe au mtu kutoka kwangu?”

**Wajumbe:** “Hakuna.”<sup>78</sup>

Imam aliwaambia yote hayo, na walikuwa wanatambua kuhusu ukweli wa yale aliyoyasema. Lakini maslahi yao binafsi yalipingana na yale waliyajua kuhusu yeye.

## NIA NA MATOKEO

Imam alijitahidi kwa kutumia mantiki kuwazuia wajumbe wa jopo la uchaguzi wasifanye uamuzi usiofaa, ambao utawaelekeza Waislamu kwenye machafuko ya wendawazimu, ambayo yangeweza kutawala umma

<sup>78</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, fasili yza nahjul Balagha, Juz. 2, uk. 198-199.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kwa vizazi vingi vijayyo. Kwa bahati mbaya, wajumbe walishindwa kunyanya na kufika kiwango ambacho huhitajiwa katika hali ya hatari. Hususan wao walikuwa na tamaa ya makuu na hawakutaka kusahau maslahi yao. Endapo Ali angepata mamlaka ya uongozi, matumaini yao binafsi ya kufika kwenye uongozi siku za usoni yangefifia. Kama uongozi ungerudi kwenye Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ungedumu humo kwa kipindi kirefu. Kwa upande mwingine, kumpa uongozi Uthman, mlango wa kwenda kwenye uongozi ungebaki wazi kwa watu kama Abdul-Rahman ambaye alikuwa na matumaini kwamba Uthman mwenye umri mkubwa angekufa kabla yake na kwa hiyo angemtaja yeche kuwa mrithi.

Wajumbe wa Jopo la uchaguzi walikuwa tayari kisaikolojia kumzuia Ali asipate ukhalifa, japokuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema mengi kuhusu yeye. Kwa nini? Makhalifa wawili wa kwanza pamoja na uadilifu wao, walifanya hivyo. Masahaba wengine walitarajiwa kufanya vivyo hivyo.

Kwa kuwa kukwepesha uongozi kutoka kwa Ali wakati wa kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni jambo ambalo halikutegemewa, kukwepesha uongozi huo kwa Ali baada ya Makhalifa wawili pia ni jambo ambalo halikutegemewa. Khalifa wa pili hakuona kuwa ni kukiuka utaratibu kumpa ukhalifa Uthman. Labda alifikiri kuwa ni tendo jema ambalo lin-gelipwa kwa upendeleo kwake.

Wasomaji wanaweza kukumbuka kwamba Uthman aliandika wasia wa Abu Bakr ambamo alimtaja Umar kuwa mrithi wake. Wakati anatamka imla ya wasia wake, Abu Bakr alipoteza fahamu kabla ya kutamka jina la Umar. Akiogopa kwamba labda Khalifa angezirai na kufa moja kwa moja, Uthman aliandika jina la Umar bila kungoja kauli ya Khalifa. Abu Bakr alipata fahamu, akamtaka Uthman asome yale aliyoandika. Uthman ali-fanya hivyo, na aliposoma jina la Umar, Abu Bakr alishangaa na kufurahi. Kama mambo yalivyo, Umar kamwe hakusahau lile alilomfanyia Uthman.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### TABAKA JIPYA.

Kwa kuwa matukio yaliyotangulia Mkutano wa Uchaguzi yalileta kuundwa kwa matabaka mapya ya kijamii; Maqraishi, masahaba waliopendelewa, na Bani Umayya, kuundwa kwa jopo la uchaguzi kuliongeza tabaka jingine jipy. Talha, Zubeir, Saad na Abdul-Rahman wakawa watu wa tabaka la juu zaidi mionganoni mwa masahaba. Umar aliwapandisha cheo kwa ajili ya kuwa na sifa za kustahili kuwa Khalifa kwa kuwaingiza kwenye jopo la uchaguzi. Tukio hili liliwasha tamaa ya kupata uongozi.

Tukio hili liliwafanya wahisi kwamba wao wapo sawa na Ali na washindani wake. Hali hii ilisababisha matukio mengi ya hatari. Ilisababisha Talha na Zubeir kujaribu kuharakisha kifo cha Uthman baada ya kutoa kiapo cha utii na imani kwake. Walikula njama dhidi yake na kila mmoja wao alikuwa kwenye kinyang'anyiro cha kumrithi yeye. Hali hii ilisababisha kifo cha Uthman katika hali ya vurugu kubwa ambapo ilisitisha mshikamano wa Kiislamu. Tamaa ya makuu ile ile iliwhamasisha masahaba hawa wawili wazuri kuuwekea changamoto uongozi wa Ali baadaye kwa kuvunja makubaliano naye ambapo waliapa kuwa waaminifu na watiifu kwake.

### FURSA ILIYOPOTEA.

Kupitia na kuundwa kwa jopo la uchaguzi, Waislamu na Khalifa wa pili walipoteza fursa ya mwisho ya kurekebisha hali na kuepusha misiba isiyohesabika ambayo ingelitokea kwa umma.

Khalifa wa pili alijiandikia yeye mwenyewe na umma wake kurasa tukufu zing'arazo katika historia. Wakati wa utawala wake na wa yule aliyemtangulia, ukhalifa ulichukua njia ya uadilifu, kwa kutiwa msukumo na mwongozo wa Qur'ani Tukufu na miongozo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini lengo la ujumbe wa Mbinguni ilikuwa si kuendeleza serikali

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

iliyoadilifu kwa miaka kumi na mbili tu na baadaye kutolewa katika njia ya haki, udugu, na demokrasia ya kweli.

Uongozi ulikwepeshwa kutoka kwa Ali na kwenda kwa Abu Bakr, halafu kwa Umar, na wote wawili walikuwa watendaji waadilifu. Kama Ali angechukua uongozi baada ya Umar, kuingia kwake kwenye mamlaka ingekuwa hajachelewa sana, umma lilikuwa bado na nguvu, likitawaliwa na moyo wa udugu na kuiweka dini yake juu ya mambo yake ya kidunia. Ilikuwa inawezakana kwa Imam Ali kwa kuwa na sifa zake kubwa, kuen-delea kuliweka umma kwenye njia iliyonyooka na kuongezea kurasa zing'arazo kwenye rekodi yake nzuri. Ingewezekana yeye kuzuia mfarakano usitokee.

Ushawishi wa Bani Umayya ulianza kukua wakati wa kipindi cha Umar, lakini ushawishi huo ulikuwa bado haujapanuka vya kutosha na kus-ababisha hatari kubwa kwa ukhalifa. Mfano wa utawala wa jimbo wa Muawiya haukuwa na nguvu ya kutosha kuwa changamoto kwa mamlaka ya serikali kuu. Kama Ali angemrithi Umar, angeweza kuwa na nafasi ya kung'oa mmea wa Bani Umayyah huko Damascus (kumwondoa Muawiya) kabla mizizi yake haijakwenda kwenye kina kirefu zaidi na kue-nea kwenye ardhi ya Syria.

Masahaba waliopendelewa hawangekuwa na uwezo wa kutoa changamoto kwa uongozi wa Imam. Wala Talha na Zubeir hawangekuwa na mamlaka ya kutosha kuwa tishio kwake. Walikuwa wawili tu kati ya makundi ya baadhi ya masahaba wema.

Kama Umar angempa Ali uongozi, angeliepusha umma kwenye matukio yote hayo ya maangamizi, na angepata mwendelezo wa mshikamano wa umma pamoja na mwendelezo wa ukhalifa adilifu kwa vizazi vingi vya siku za usoni.

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

Endapo Umar angefanya hivyo, angekuwa ameirudisha haki ya watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa na uongozi wa Kislamu na angekuwa amewalinda watu hawa waadilifu mno dhidi ya uovu wa Bani Umayyah. Kwa kufanya hivyo, angekuwa ameleta furaha kwenye roho Takatifu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Kwa kutumia hekima yake kubwa, Umar alitarajiwa kufuata mkondo huu wa uadilifu. Kwa bahati mbaya, mwambatano wa kiukoo wa Maquraishi ulizidi busara za sahaba huyu mashuhuri. Hali hii ilisababisha msiba wa Mkutano wa Uchaguzi.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

# SURA YA ISHIRINI NA MOJA UTAWALA WA UTHMAN.

Jopo la uchaguzi lilitoa matokeo na kuhitimisha kazi yake kama ilivy-otarajiwa. Uthman akapewa mamlaka ya kuwa Khalifa wa tatu. Akiwa katika daraja la sahaba, Uthman hakuwa pungufu ya wale wawili waliomtangulia: Abu Bakr na Umar. Alikuwa mionganoni mwa watu wanne baina ya watu kumi waliokubali Uislamu mwanzoni (katika watu 40 Waislamu wa mwanzo). Uislamu wake ulikuwa wa mwanzo zaidi ya ule wa Umar, na kabla ya kusilimu hakuwa na vurugu kama Umar katika kuupinga Uislamu. Alikuwa na sifa bainifu ambayo hapana hata mmojawapo kati ya wale waliomtangulia aliyekuwa nayo:

Uthmna alikuwa mkwe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), mara mbili. Alimuoa Rukia, mmojawapo wa mabinti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Tunda la ndoa hii ni mtoto aliyeitwa Abdullah ambaye alifariki akiwa na umri wa miaka sita baada ya kifo cha mama yake. Baada ya Rukia, Uthman alimuoa dada yake Umm Kuluthumu.<sup>79</sup> Pia huyu hakuishi naye muda mrefu. Alifariki wakati wa uhai wa baba yake Mtukufu.

## HAKUWA MPIGANAJI.

Uthman hakushiriki kwenye vita vyta Badr. Alikuwa Madina akimuuguza mke wake Rukia ambaye alikufa kabla baba yake Mtukufu hajarudi kuto-

<sup>79</sup> Hii ni kwa mtazamo wa mwandishi. Lakini kwa mujibu wa utafiti wa kina wa watafiti wetu adhimu ni kwamba mabinti hao wawili hawakuwa watoto wa kuzaa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, bali ni kama vyanzo vingi vya kitafiti vilivyoolekeza kwamba walikuwa ni watoto wa kulea wa Mtume au watoto wa dada yake na Khadija waliokuwa chini ya malezi yake, na hili la pili ndilo chaguo safi toka katika kilele bora cha utafiti na uhakika, na hivyo hititmishe ni kwamba Mtume hakuwa mkwe halisi wa Uthman. – Mhariri.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

ka kwenye uwanja wa vita. Uthman alishiriki vita vya Uhud na vinginevyo. Historia haikuandika chochote kuhusu kushiriki kwake kwenye mapigano kwenye vita vyovyote vile. Kama masahaba walio wengi, na yeze alimkimbia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wakati wa Vita vya Uhud. Alirudi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) baada ya vita kwisha, na alikuwa mmojawapo wa masahaba waliosamehewa na Muweza wa Yote kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu:

﴿ إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَّقَىٰ أَجْمَعَانِ إِنَّمَا أَسْتَرَّ لَهُمُ الشَّيْطَنُ بَعْضُ مَا كَسَبُواۚ ۝ وَلَقَدْ عَفَ اللَّهُ عَنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ۝ ﴾

**“Hakika wale waliorudi nyuma miogoni mwenu siku yalipopambana majeshi mawili. Shetani ndiye aliywatelezesa kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyofanya; na Mwenyezi Mungu amekwishawasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mpole.” (Qur’ani 3:155).**

Uthman hakuwa shujaa, lakini alikuwa mtu wa kutoa misaada. Alishiriki kikamilifu katika kuruzuku jeshi la Tabuk. Taarifa inasema kwamba alimpelekea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) dinari elfu moja (wakati wa kuchapishwa kitabu hiki ilikuwa sawa na dola elfu kumi) ili zitumike kuimarisha misheni ya jeshi. Alitoa misaada mingine pia.

Uthman aliingia madarakani mwishoni mwa mwaka wa ishirini na tatu baada ya Hijiriya (644 A.D). Utawala wake ulianza akiwa na umri wa zaidi ya miaka sabini na aliendelea kutawala kwa miaka kumi na mbili.

Katika kipindi cha miaka sita ya mwanzo wa utawala wake, mambo ya uendeshaji wake yalikuwa sawa. Waislamu walipata ushindi katika sehemu nyingi wakati wa kipindi hiki. Walikuwa bado wapo katika hali ya kivita na falme mbili mashuhuri za wakati huo: Ajemi na Byzantine. Kwenye

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

falme ya Ajemi zile sehemu ambazo zilikuwa hazijatekwa na utawala wa Umar, zilichukuliwa na utawala wa Kislamu chini ya uongozi wa Uthman. Afrika ya Kaskazini pia ilichukuliwa kutoka Falme ya Rumi na kuwa sehemu ya Nchi ya Kiislamu. Khalifa wa tatu aliondoa amri ya kutoikutumia njia za bahari kwa shughuli za kivita. Kundi muhimu la Kiislamu la vipando vya baharini liliundwa kwenye Bahari ya Kati (Mediteranian Sea).

Miaka sita ya mwisho wa utawala wa khalifa wa tatu ilijaa matukio mabaya. Mapambano ya matabaka ya wanaolipwa ruzuku kuzidi wengine na wale waliokuwa wanalipwa fedha kidogo, yalianza kupanuka haraka hadi yalipolipuka kwa mapinduzi na majeruhi wake wa kwanza alikuwa Khalifa wa tatu. Matukio yaliyotokea katika kipindi cha miaka sita ya mwisho wa utawala wa Uthman yalitengenezwa kabla ya kipindi hiki. Fikira za kutengeneza matukio haya ziliasiwi mwanzoni mwa utawala wake na wakati wa kipindi vya utawala wa walio mtangulia.

### MTU KIUNGANISHI.

Uthman wala hakuwa na busara ama dhamira ya wale waliomtangulia. Ama hakuwa na msimamo wao wa kutokuwa na tamaa ya utajiri wa mali. Kwa hakika shaksia yake ilikuwa na pande mbili zinazopingana. Kwa upande moja, alikuwa Muislam wa mwanzoni. Aliandamana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa muda mrefu, akapata heshima ya kuo mabinti wawili wa Mtume, na alikuwa mtoaji sadaka mzuri katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa upande mwingine yeye alikuwa mtu wa ukoo wa Umayyah. Alikuwa anawapenda sana watu wa ukoo wake japokuwa walikuwa na rekodi mbaya kwa uadui wao dhidi ya imani ya Uislamu na Mtume wake (s.a.w.w.). Pande hizi za utu wake ziliwafanya masahaba mashuhuri wabashirie uwezo wa Khalifa wa tatu kuwa kama daraja ambamo ukhalifa utapita kutoka kwenye utawala adilifu wa masahaba wa awali wa Muhammad na kuingia kwenye utawala wa kidikteta na kidhalimu wa watu wa ukoo wa Bani Umayyah.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Msomaji anaweza kukumbuka kwamba Umar alipotoa maelekezo yake kuhusu uteuzi wa mrithi wake, Ali alimwambia ammi yake, Al-Abbas: “Najua kwamba watampa ukhalifa Uthman na endapo anauawa au anakufa, watu wa ukoo wa Bani Umayyah watafanya ukhalifa uzunguke miongoni mwao na endapo mimi nitakuwa hai, wataniona nipo mahali wasipopapenda.”

Inashangaza kwamba Maquraishi walikataa kumpa Imam Ali uongozi, wakihofia kwamba uongozi labda unaweza ukabaki kwenye Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu ya sifa yao ya kuzingatia dini, sifa ambayo hailinganishwi na yoyote, bado Maquraishi walichagua kufanya Ukhilifa uwe kwenye nyumba ya Bani Umayyah ambao walijulikana kwa chuki kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na dini yake.

### UPINZANI ULIANZA MAPEMA.

Labda hii inaweza kuwa mojawapo ya sababu ambazo ziliwafanya masahaba wawili ambao ni mashuhuri; Ammar Ibn Yasir na Al-Miqdad Ibn Al-Aswad, waanze upinzani dhidi ya Uthman mwanzoni mwa utawala wake. Kwa sauti kubwa walikataa kuingia kwake madarakani japokuwa walijua kuhusu uadilifu wake.

Historia imeandika kwamba Ammar alitoka nje akiwa anapiga kelele baada ya kuchaguliwa kwa Uthman: “Wewe mtangazaji wa kifo, jitokeze mbele na utangaze kifo cha Uislamu. Haki imekoma, na uovu umetokeza. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kama nikiona wasaidizi nitapigana na Maquraishi. Kwa jina la Mwenyezi Mungu kama nikimuona mtu mimi nitakuwa wa pili wake.”<sup>80</sup>

<sup>80</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, Fasili zake za *Nahjul Balagha*, Juz. 2, uk. 411-412.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Alimwendea Imam Ali na akamtaka aanze vita dhidi ya Maquraishi. Lakini Imam alimkumbusha yeye juu ya upungufu wa wanaomuunga mkono. Alimwambia yeye na wengine: Nisingependa kuhatarisha uhai wenu, au niwabebesheni mzigo ambao unazidi uwezo wenu.”

Al-Miqdadi alitokeza nje mnamo siku iliyofuata baada ya kuchaguliwa kwa Uthman. Alipokuwa anatembea, alikutana na Abdul-Rahman Ibn Awf, mfagiliaji wa mfalme mtarajiwambaye ndiye aliyesimamia kuteuliwa kwa Uthman. Makabiliano ya masahaba wawili yalitokea kama ifuatavyo:

**Al-Miqdad:** “Ewe Abdul-Rahman, Mwenyezi Mungu na akujaalie hapa duniani na Akhera kama ultaka kumridhisha Mwenyezi Mungu kwa haya uliyoyafanya. Na Akuongezee utajiri kama umedhamiria kutafuta maslahi ya kidunia kwa kufanya kama ulivyofanya.”

**Abdul-Rahman:** “Mwenyezi Mungu na akuhurumie; nisikilize.”

**Al-Miqdad:** “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, sitasikiliza.” Miqdadi akaondosha mkono wake kutoka kwenye mkono wa Abdul-Rahmna na akaondoka.

Masahaba hawa wawili walipambana kwa mara nyingine mahali pengine:

**Al-Miqdad:** “Wallahi, kamwe sijapata kuona mfano wowote wa yale waliyofanyiwa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).”

**Abdul-Rahman:** “Ewe Miqdad, kwa nini unajihuisha na haya?

**Al-Miqdad:** Wallahi! Ninawapenda wao kwa mapenzi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ninashangazwa na Maquraishi ambao wanadai kuwa bora kuzidi watu wengine kwa sababu ya

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

uhusiano wao kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), halafu wana-jidirikisha kuchukua mamlaka ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutoka kwa watu wa Nyumba yake.

**Abdul-Rahman:** “Wallahi, nimejaribu kufanya kile ambacho ni kizuri kwa maslahi ya watu.”

**Al-Miqdadi:** “Wallahi, umemwacha mtu ambaye ndio mwenye uwezo wa kuuongoza umma huu kwenye njia iliyonyooka na kudumisha uadilifu na kutenda haki. Kwa jina la Mwenyezi Mungu kama ningepata watu wa kuniunga mkono dhidi ya Maquraishi, nitapigana nao kama nilivyopigana nao kule Badr na Uhud.”

**Abdul-Rahman:** “Mama yako na aachwe mkiwa kwa kufariki kwako. Naasiwepo mtu wa kuyasikia maneno hayo kutoka kwako. Nina hofu kwamba wewe umekuwa mtu mbadilishaji wa itikadi na unayeendeleza mfarakano.”

**Al-Miqdad:** “Mtu anayewaita watu wafuate ukweli na haki si mbadilishaji wa itikadi. Lakini mtu anayewaswaga watu waelekee uwongo na anapenda ubinafsi badala ya ukweli ndiye mtu mbadilishaji na mpenda faraka ....”<sup>81</sup>

Si Ammar wala Al-Miqdad, wao walikuwa hawana tamaa ya makuu ya kisiasa, na wala hapana yeyote kati yao alikuwa anajaribu kujitahidi kupta rasilimali. Masahaba hawa walisisiwa sana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ibn Majah amesimulia kwenye *Sunan* yake kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: Mwenyezi Mungu ameniamuru mimi niwapende watu

<sup>81</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, kwenye Fasili zake za *Nahjul Balagha*, Juz. 2, uk. 411-412.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wane, na akanitaarifu kwamba Yeye anawapenda watu hao.” Alipouliza watu hao ni akina nani, akasema: “Ali ni mmojawapo (akarudia usemi huo mara tatu) Abu Dharr, Salman na Al-Miqdad.”<sup>82</sup>

Al-Tirmidhi amesimulia kwenye Sunan yake kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Kila Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipewa Masahaba wenyе sifa bainifu lakini mimi nilipewa kumi na nne.” Halafu akahesabu Ammar na Miqdad mionganoni mwa hao kumi na nne.”<sup>83</sup>

Al-Tirmidhi pia ameandika kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema pale ambapo Ammar Ibn Yasir aliomba ruhusa kuingia kwenye nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Mwambieni aingie. Karibu ewe mwema, uliyetakaswa.”<sup>84</sup>

Pia ameandika kwamba Aisha alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Pale ambapo Ammar amepewa fursa kuchagua mambo mawili, huchagua kile ambacho ni kiadilifu zaidi ya kingine.”<sup>85</sup>

Al-Tirmidhi ameandika pia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Ammar: “Ewe Ammar uwe na furaha, kundi la watu waovu ndilo kitakalo kuua.”<sup>86</sup>

<sup>82</sup> Ibn Majah, *Sunan yake* sehemu ya 1, uk. 53 (hadith Na.149).

<sup>83</sup> Al-Tirmidh, *Sunan yake*, sehemu ya 5, uk. 329 (Hadith Na. 149).

<sup>84</sup> Al-Tirmidh, *Sunan yake*, sehemu ya 5, uk. 332.

<sup>85</sup> Al-Tirmidh, *Sunan yake*, sehemu ya 5, uk. 332-333.

<sup>86</sup> Al-Tirmidh, *Sunan yake*, sehemu ya 5, uk. 332-333.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BANI UMAYYAH.

Yale ambayo masahaba hawa wema waliona katika hisia zao sasa yakianza kuwa kweli. Ishara za hali ya baadaye zilianza kuonekana haraka haraka. Watu wa ukoo wa Bani Umayyah walikutana nyumbani kwa Uthman baada ya kuchaguliwa. Abu Sufyani mzee wao, ambaye alikwishakuwa kipofu kwa sababu ya uzee aliwaliza: Wapo amba si wa ukoo wa Bani Umayyah miongoni mwenu?” Walipomhakikishia kwamba hapakuwepo na yejote, alisema: “Wana wa Umayya, uzungusheni (ukhalifa) miongoni mwenu kama watoto wanavyozungusha mpira wa miguu. Kwa jina la yule ambaye Abu Sufyani anaapa, wala hapatakuwepo na Pepo au Jahanamu au ufufuo au Siku ya Hukumu.”<sup>87</sup>

Kama mambo yalivyo, Khalifa alimkemea, lakini karipio halikubadilisha msimamo wake Abu Sufyani. Alimuomba mtu amsindikize kwenye kaburi la Hamza, ami yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na fahari ya mashahidi. Aliposimama juu ya kaburi alisema, akimwambia Hamza: “Ewe Abu Imarah (jina la siri la Hamza) jambo ambalo tulipania sasa limekuwa mchezo uliomo mikononi mwa vijana wetu.” Halafu akalipiga teke kaburi kwa mguu wake.”<sup>88</sup>

Usemi wa Abu Sufyani ulikuwa na maana kwamba ukoo wa Bani Umayyah na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na familia yake walipigana kwa sababu ya mamlaka. Sababu mamlaka ilifika mikononi mwa Bani Umayyah na watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walinyang’anywa mamlaka hayo.

<sup>87</sup> Ibn Abul Al-Hadeed, kwenye Fasil zake za *Nahjul Balaghah*, Juz. 2, uk. 411.

<sup>88</sup> Ubd Al-Fattah, Abd Al-Maqsood, *Al-Imam Ali*, Sehemu ya 1, uk. 284

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Haikuchukua muda mrefu kabla maneno haya hayajatafsiriwa kuwa kweli. Watu wa ukoo wa Bani Umayyah walitumia upole wa Khalifa wa tatu na upendo wake mkubwa sana kwa ukoo wake. Katika kipindi cha miaka michache ya mwanzo wa utawala wake, Bani Umayyah walivishika vyanzo viwili nya mamlaka. mamlaka ya majimbo muhimu ya serikali ya Kiislamu na hazina zao.

Mamlaka makuu na utajiri wa serikali ya Kiislamu vilikuwa kwenye majimbo matatu; Syria, Iraq na Misri. Katika kipindi cha miaka michache ya mwanzo wa utawala wa Uthman, maeneo haya mapana yalikuwa chini ya utawala wa Bani Umayyah.

### MUAWIYA NA SYRIA.

Tumesema katika Sura ya 19 kwamba Umar alimteua Muawiya kuwa gavana wa Damascus, halafu akaongeza Jordan kwenye mamlaka yake baada ya kifo cha Yaziid (kaka yake Muawiya). Umar pia alimteua Umair Ibn Saad (mtu wa Madina) kuwa gavana wa Homs, na Qinnasrine na Abdul-Rahman Ibn Alqamah kuwa gavana wa Palestina. Umar alipokufa, hawa watu wawili walikuwa bado wamo kwenye kazi zao. Lakini Abdul-Rahman Ibn Alqamah alifariki mnamo mwanzoni mwa utawala wa Uthman na Umar alijiuzulu kwa sababu ya maradhi. Uthman aliongeza Palestina, Homs na Qinnasrine kwenye mamlaka ya Muawiya.<sup>89</sup> Hivyo katika kipindi cha miaka miwili tangu ulipoanza utawala wa Uthman, Muawiyah akawa gavana wa ile inayoitwa leo Syria Kubwa ‘Greater Syria.’

Ushawishi wa Muawiya ulianza wakati wa kipindi cha Umar. Lakini, ulibakia kuwa mdogo na ambao ulikuwa unaangaliwa sana na Umar. Ukubwa wa eneo lake ulikuwa zaidi ya mara mbili ya wakati wa utawala

<sup>89</sup> Ibn Al-Athir kwenye *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 57.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wa Uthman na ushawishi wake ukawa kamili na bila uangalizi wowote. Katika kipindi cha miaka michache, Syria ikawa serikali inayojiamulia mambo yake ndani ya serikali ya Kiislamu, na Muawiya akawa mtu mwenye mamlaka na uwezo mkubwa wa dunia ya Waislamu. Katika kipindi cha miaka michache alikuwa na uwezo wa kuwa na jeshi kubwa kwenye uwanja wa vita likiwa na wapiganaji laki moja. Inafaa kufahamu kwamba Muawiya, hakuwa mtu mwadilifu zaidi ya baba yake Abu Sufyani.

### IBN ABU SARH AKIWA MISRI.

Umar alikufa wakati ambapo Amr Ibn Al-Aas alikuwa gavana wa Misri. Uthman alimfukuza mnamo miaka miwili ya mwanzo wa utawala wake. Badala yake akamteua kaka yake wa kuchangia kunyonya Abdullah Ibn Saad Ibn Abu Sarh, ambaye aliendelea na kazi hiyo hadi mwisho wa utawala wa Uthman. Ibn Abu Sarh alikuwa mmojawapo wa maadui wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikubali kuwa Mwislamu wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), halafu akaritadi. Alikuwa na tabia ya kukejeli Qur'ani Tukufu, akisema: "Nitaleta ufunuo sawa na ule ambao Mwenyezi Mungu ameteremshia Muhammad."

Ibn Hishamu ameandika kwamba Ibn Abu Sarh aliukubali Uislamu na akawa mwandishi wa Wahyi ulioteremshwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Halafu akaikimbia imani hii na akarudi kwa Maquraishi. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoingia Makka aliagiza Ibn Abu Sarh auawe. Akakimbilia nyumbani kwa Uthman ndugu yake wa kunyonya, naye akamficha. Hali ilipotulia, Uthman alimpaleka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), akamwombea msamaha. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alinyamaza kimya kwa muda mzuri tu, halafu akasema: "Ndio." Uthman na ndugu yake wa kunyonya walipoondoka, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema na kuwaambia masahaba waliokuwa wamemzunguuka: "Nilinyamaza kwa kipindi kirefu, nikiratajia kwamba mmoja wenu angemuua mtu huyu." Sahaba wa kutoka Madina aliuliza: "Ewe Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

nini hukunipa mimi ishara?" Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu: "Mtume hau i kwa kutumia ishara."

### IRAQ.

Ilikuwepo miji mikuu miwili ndani ya Iraq: Kufah na Basrah. Umar alimteua Saad Ibn Abi Waqass gavana wa Kufah. Halafu akamfukuza na badala yake akamteuwa Al-Mughiirah Ibn Shubah kushika nafasi hiyo.

Uthman alipoteuliwa kuwa Khalifa, alimfukuza Al-Mughiirah na badala yake alimteua Saad Ibn Abi Waqass kwa kuzingatia mapendekezo ya Umar kabla hajafa.

Saad alikuwa sahaba aliyeheshimiwa sana na alipata nafasi mashuhuri pale Umar alipomteua kuwa mjumbe wa jopo la uchaguzi. Licha ya kuwa na nafasi hii Uthman alimweka kwenye nafasi hii ya ugavana kwa mwaka moja tu. Alimwondoa na badala yake alimteua Waliid Ibn Aqabah, binamu na kaka wa kambo wa Khalifa wa tatu.

Waliid alikuwa muovu kwa ushahidi wa Qur'ani Tukufu. Aliingia kwenye Uislamu baada ya mwaka wa mkataba wa amani wa Hudaibiyah. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka kwenye kabilia la Banul-Mustalaq, kwa kazi ya kukusanya Zaka. Wakitarajia kufika kwake, Banul Mustalaq walipanda farasi kwenda kumpokea. Alipowaona wanakwenda mbele yake, aliogopa na akarudi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla ya kukutana nao. Alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba Banul Mustalaq walitaka kumuua yeye. Wakitegemea taarifra yake Waislamu walifikiria namna ya kuwaadhibu hao Banul Mustalaq. Lakini Mustalaq walikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wakamwambia nia yao ilikuwa kumpokea na kumheshimu Waliid na si kumuua yeye. Wahyi uliteremka kuhusu Waliid na Bani Mustalaq ukiwakataza waumini kuamini taarifa za watu wasio waadilifu kama Waliid, kwa sababu fasiki hafai kuaminiwa. Hivyo tunasoma kwenye *Surat Al-Hujurat* ifuatavyo:

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

“Enyi mliaoamini! Akikujieni fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa tena wenyewe kujuta kwa mnayoyatenda. Na Jueni kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angelikutiini katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni wenyewe kuchukia upotovu na uasi. Hao ndio walioongoka.”<sup>90</sup>

Ni dhahiri kwamba Waliid alikuwa ameweka akili yake ya kabla ya Uislamu katika maisha yake yote. Alikuwa gavana wa Kufah kwa miaka mitano, hadi mashahidi kutoka watu wa Kufah walitoa ushahidi kwamba alikuwa anakunywa kilevi. Alipewa adhabu inayostahili kwa kosa hilo, na Khalifa alitakiwa kumfukuza kazi. Hali ya Waliid ilijulikana vya kutosha kwa Uthman na kwa Waislamu wema, hususan baada ya Qur’ani Tukufu ilipomuita yeeye fasiki.

Imeandikwa kwamba Waliid alipokwenda kushika nafasi badala ya Saad, Saad alimuuliza: “Umekwisha kuwa na busara au sote tumekuwa wapumbavu?” Waliid alijibu: “Ewe Abu Is’haq (jina la siri la Saad), wala hakuna lolote. Ni mamlaka ya Kifalme ambayo baadhi ya watu huchukua kama chakula cha mchana na halafu wengine wanachukua kama chakula cha jioni.” Saad akajibu: “Nyinyi (Bani Umayyah) ni dhahiri kwamba mmeufanya ukhalifa kuwa ufalme.” Pia Abdullah Ibn Mas’ud alimwambia Waliid: “Sijui kama umegeuka kuwa mwema au watu wamekuwa wabaya.”<sup>91</sup>

Kwa kuwa Khalifa alitakiwa kumfukuza kaka yake wa kunyonya, baada ya kashfa alitarajiwa kumbadilisha na kumweka badala yake sahaba kama Saad Ibn Abu Waqass, au Ammar Ibn Yasir au Abdullah Ibn Mas’ud.

<sup>90</sup> Qur’ani Tukufu (49:6-7), Ibn Hishamu aliandika tukio hili kwenye Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sehemu ya 2, uk. 296.

<sup>91</sup> Ibn al-Athiir kwenye *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 40.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Lakini Khalifa hakufanya lolote kati ya haya. Alimbadilisha na Said Ibn Al-Aas, Umayya mwengine. Japokuwa rekodi ya Said haikuwa kama ya Waliid, alikuwa ndiye tu mmoja wa vijana wa Bani Umayyah ambaye uganava wake haukuwatia moyo watu wa Kufah na kuwapa matumanini wala kurekebisha yale yalijotakiwa kurekebishwa. Tutaona baadaye kwamba matukio yalitokea na kubadili hali na kuwa mbaya zaidi wakati wa siku za Said.

### BASRAH.

Alipokufa Umar, Abu Musa Al-Ashari alikuwa gavana wa Basrah. Aliendelea na kazi hiyo kwa miaka mitatu au mitano wakati wa utawala wa Uthman. Ujumbe kutoka Basrah ulikwenda kumwona Khalifa, ukilalimika kuhusu ubadhirifu wa hazina ya umma uliokuwa ukifanyiwa na Abu Musa. Abu Musa hakuwa mionganoni mwa masahaba wema. Ilitokea wakati fulani alishutumiwa na Umar kuhusu kujitajirisha kwa ghamra ya Waislamu, na Umar alimnyang'anya utajiri wake wa zaidi na kuurudisha kwenye hazina ya umma. Bado alimwacha akiendelea na kazi yake ile ile kwa sababu ya kuwa mwaminifu sana kwa Khalifa wa pili.

Khalifa wa tatu alitarajiwa kuchunguza malalamiko ya ujumbe wa Basrah na kumweka mtu mwengine badala yake endapo angeonekana ana hatia kwa uthibitisho wa sahaba aliye mbora zaidi. Lakini Uthman hakufanya hivyo. Badala yake, alisikiliza malalamiko ya ujumbe huo, akamfukuza Abu Musa na badala yake alimteua Abdullah Ibn Amir, kijana mwengine wa ukoo wa Umayya. Hivyo, katika kipindi cha miaka michache ya utawala wa Uthman, majimbo matatu muhimu ya serikali ya Kiislamu yalishikwa na watu wa ukoo wa Bani Umayyah. Wengi wa viongozi wao walikuwa maadui wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na waliolaaniwa naye au na Qur'ani Tukufu.

Athari mbaya ya kuteuliwa kwao kushika nafasi za juu kama hizo zingepunguzwa kwa uangalizi mkubwa wa Khalifa. Ilikuwa rahisi Khalifa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kuwa na washauri waadilifu na wenye akili kutoka miongoni mwa masahaba. Angewapa mamlaka washauri kama hao ya kuchunguza na kusimamia uendeshaji wa majimbo haya. Bahati mbaya, usimamizi haukuwe-po kabisa. Mshauri mkuu wa Ukhilifa alikuwa binamu yake Marwan Ibn Al-Hakam, Bani Umayyah mwingine asiye mwadilifu. Uwezo wa mamlaka aliopewa huyu kijana wa ukoo wa Bani Umayyah haupo kwa waziri mkuu yejote wa wakati wetu. Kwa kweli, Marwan ndiye hasa aliyekuwa Khalifa na Uthman alikuwa kama nembo tu ya ukhalifa.

Hivyo, ukhalifa ulibadilishwa na kuwa ufalme halisi wa ukoo wa Bani Umayyah. Kuuandaa ulimwengu wa Bani Umayyah, maofisa watendaji walitetea ubora wa Maquraishi kuzidi Waarabu wengine na ubora wa ukoo wao kuzidi Maquraishi wa koo zingine. Walilazimisha kimya kamili kuhusu kuwaainisha watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa ujumla, na hususan Ali. Waliwapa taarifa raia wao kuhusu uhusiano wao wa karibu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Historia ya uadui wao kwake na watu wa Nyumba yake haukutakiwa kutamkwa kwa raia hao amba walikuwa Waislamu wapya, na hawajui historia ya Uislamu.

Wakati fulani Muawiya alikutana na Ammar Ibn Yasir huko Madina. Katika mabishano makali, alimwambia Ammar: "Huko Damascus wapo zaidi ya watu laki moja watoto na watumishi wao. Hupokea mishahara yao ya mwaka, na hawamjui Ali na uhusiano wake na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au Ammar na Uislamu wake wa siku za mwanzo, wala Zubeir na ushaba wake.<sup>92</sup> Jundab Ibn Abdullah Al-Azdi wakati fulani alijaribu kuwapa taarifa watu wa Kufah kuhusu sifa bainifu za Imam Ali. Taarifa hiyo ilipomfikia Waliid Ibn Aqabah, gavana wa Kufa, alimfunga jela na hakumfungulia hadi hapo watu mashuhuri walipoingilia kati na wakam-wombea msamaha ili aachiwe huru.<sup>93</sup>

<sup>92</sup> Abdul-Fathah Abd Al-Maqsood kwenye *Al-Imam Ali Ibn Abu Talib*, sehemu ya 2, uk. 120.

<sup>93</sup> Ibn Abu Al-Hadeed kwenye fasili zake za *Nahjul-Balaghah*, Juz. 2, uk. 412.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### KHALIFA WA TATU NA WAWILI WALIO MTANGULIA

Unaweza kukumbuka kwamba Abdul-Rahman Ibn Awf aliwapa Ali na Uthman ukhalifa, na kuweka sharti kwamba Khalifa wa tatu alitakiwa afuatae nyayo za makhalifa wawili wa mwanzo. Ali alipoteza ukhalifa kwa sababu alikataa sharti hilo. Uthman alipata ukhalifa kwa sababu alikubali sharti la kufuata nyayo za makhalifa wawili wa mwanzo. Natuangalie kama alitimiza ahadi yake kwa Abdul-Rahman na kwa Waislamu wote.

Hapana mmojawapo baina ya hao makhalifa wawili wa mwanzo waliteua ndugu zao wowote kushika kazi yoyote kwenye majimbo ya Kiislamu au miji mikuu. Kinyume chake, Uthman aliwaweka ndugu zake kwenye kazi za ugavana katika majimbo yote muhimu. Kwa kufanya hivi alikuwa anao ulinganifu wowote katika utendaji wake na makhalifa wawili wa mwanzo? Khalifa wa tatu hakuonekana kuamini kwamba utendaji wake haukupatana na jinsi walivyofanya wale makhalifa wawili waliomtangulia. Alithibitisha uteuzi wa ndugu zake kwa ukweli kwamba Umar alimteua Muawiya na watu wengine kama Muawiyah, kama vile Amr Ibn Aas na Maghiirah Ibn Shubah kuwa gavana wa Damascus, Misri na Kufah. Umar hakuteua masahaba bora sana wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kazi hizi. Khalifa wa tatu angesema pia kwamba Umar alimkabidhi mamlaka ya ukusanyaji wa Zaka Waliid Ibn Aqabah huko Jazirah. Labda pia Umar alimteua Abdullah Ibn Sarh kwa kazi ndogo. Khalifa wa tatu alikuwa sahihi aliposema hivi. Lakini ukweli ulibaki kwamba Umar hakumteua ndugu yake yeyote kushika kazi yoyote kubwa au ndogo. Uthman aliteua ndugu zake kushika kazi kubwa na aliwapa mamlaka bila kuwawekea usimamizi wa kufaa.

Ni halali kusema kwamba Uthman hakuwa anafanya kinyume na walivyofanya makhalifa wawili wa mwanzo kwa kuwateua ndugu zake na kuwapa kazi kubwa kwani mvuto wa Bani Umayyah ulianza kukua na kuonekana wazi wakati wa utawala wa Umar. Ilikuwa ni kawaida kwa

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

mvuto huo kuongezeka wakati wa utawala wa Uthman, kwa kipengele cha muda na kwamba anatoka kwenye kundi la ukoo wa Umayya.

Kama Umar angekuwa hataki kuona mvuto wa ukoo wa Bani Umayyah ukikua kiasi hicho hangewapa watu wa ukoo wa Bani Umayyah kazi mbali mbali katika serikali yake. Hangeunda jopo la Uchaguzi au angalau hangemjumuisha Uthman kwenye jopo hilo, Umar alitambua kwamba Uthman alikuwa anawapenda sana watu wa ukoo wake. Kwa hiyo, hatuwezi kusema kwa uhakika kwamba mpango wa Uthman wa kuwaendeaza ndugu zake, haukuwiana na sera ya Umar, kwani Umar ndiye aliyeanza kuwaweka watu wa ukoo wa Bani Umayyah kwenye mkondo wa kuelekea kwenye mamlaka na akazidisha mvuto wao kwa njia isiyo dhahiri, walimweka ndugu yao Uthman kwenye kazi kubwa kabisa.

### **SERA LEGELEGE YA HAZINA YA UMMA.**

Kipengele ambacho Khalifa wa Tatu kwa dhahiri alitofautiana na wenzake wawili aliowafuata ni sera legelege ya hazina ya umma. Ni jambo linaloleweka vema kwamba Makhalifa wawili wa mwanzo waliishi maisha rahisi na duni, wao na familia zao. Wakati wowote Umar alipowaa-giza watu wafanye jambo, alitarajia ndugu zake kuwa mfano kwa Waislamu wengine katika kufuata agizo hilo. Khalifa wa tatu kinyume chake aliishi maisha ya anasa na wakati wote alikuwa anawamwagia ndugu zake zawadi kutoka kwenye hazina ya umma. Aliwapendelea ndugu zake kwa kuwapa misaada mikubwa ambayo hawakuwa wazingativu wa mafundisho ya Kiislamu kuliko Waislamu wengine.

### **KUHESHIMU HUKUMU YA UHAMISHO YA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.).**

Al-Baladhuri ameandika kwamba Uthman alimpa mjomba wake Al-Hakam Ibn Abu Al-Aas dinari laki tatu (sawa na dola za Kimarekani laki

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

tatu wakati huo wa kuandika kitabu hiki) baada ya kumrudisha Madina.<sup>94</sup>

Mtu huyu alikuwa mmojawapo wa maadui wabaya sana wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla hajawa Mwislamu. Baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuteka Makka, Al-Hakam alikwenda Madina akitangaza Uislamu kinafiki na kwa sababu tu ya kuokoa maisha yake. Bado aliende-lea kumbughudhi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikuwa na desturi ya kumfedhehesha yeze kwa kuiga mwendo wake. Wakati mmoja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuona anachungulia chumbani kwake kuitia kwenye mpasuko wa mlango. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitoka nje akiwa amekasirika na alipomtambua, akasema: "Hivi yupo mtu wa kunishutumu kama nikimuadhibu huyu mdudu aliyelaaniwa?" Halafu akamwadhibu kwa kumhamisha yeze na familia yake na kumpeleka Ta'if, akawakataza yeze na watoto wake kuishi Madina.

Kitendo cha kumruhusu Al-Hakam na watoto wake kurudi Madina, Uthman alikuwa anapingana wazi kabisa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Makhalfa wawili wa mwanzo, ambao hawakumruhusu Al-Hakam kurudi Madina japokuwa Uthman alifanya upatanishi kwa ajili yake.

Uthman alimpa kaka yake wa kunyonya, Abdullah Ibn Saad Ibn Abu Sarh moja ya tano (1/5) ya ngawira iliyotekwa na msafara wa kwanza wa kijeshi ambao uliongozwa na Abdullah huko Afrika ya Kaskazini. Marwan Ibn Al-Hakam alinunua moja ya tano ya ngawira (1/5) iliyotekwa na msafara wa pili huko Afrika ya Kaskazini kwa bei ya dinari laki tano (sawa na dola za Kimarekani milioni tano za wakati huo wa kuandika kitabu hiki). Halafu Khalifa alimruhusu achukue ngawira yote.<sup>95</sup>

Khalid Ibn Abdullah Ibn Usaid (mtu mwengine wa Bani Umayyah) alipokea dinari laki tatu kutoka kwenye hazina ya umma alipomtembelea,

<sup>94</sup> Al-Baladhuri, *Ansab Al-Ashraf* sehemu ya 4, uk. 28.

<sup>95</sup> Ibn al-Athiir, kwenye *Al-Kamil* sehemu ya 3, uk. 49.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

akiandamana na ujumbe. Khalifa aliagiza kila mtu aliyekuwa kwenye ujumbe huo alipwe dinari laki moja.

Pale Abdullah Ibn Arqam, mtunza hazina wa umma alipokataa kulipa kiasi hicho kikubwa cha fedha, Khalifa alimhoji kwa majivuno: “Wewe ni nani kuingilia kati agizo langu? Wewe ni mweka hazina wangu tu.” Lakini Abdullah alijibu vikali akasema: “Sikuamini kwamba mimi nilikuwa mweka hazina wako. Mweka hazina wako ni mmojawapo wa watumishi wako. Mimi ni mweka hazina wa Waislamu.” Halafu akaenda akaziangika funguo za hazina kwenye mimbari ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hapo msikitini na akajiuzulu kazi.

Khalifa aliagiza Abdullah Ibn Arqam alipewa dinari laki tatu baada ya kujuzulu kazi; lakini kwa kumuonea huruma, Abdullah alikataa msaada huo wa fedha.<sup>96</sup>

Pia Uthman alimpa Said Ibn Al-Aus dinari laki moja. Na alipowaoza mabinti zake watatu au wanen kwa wanamume kutoka kabilia la Qureishi, kila mmojawao alimpa dinari laki moja. Alimpa binamu yake Al-Harith Ibn Al-Hakam (aliyeadhibiwa kwa kupelekwa uhamishoni na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)) dinari laki tatu. Alimteua kama mkusanyaji wa Zaka wa Qudah. Alipokusanya Zaka, Khalifa alimruhusu achukue na kufanya mali yake.<sup>97</sup>

Hatupaswi kusahau kwamba Abu Sufyani, mzee wa ukoo wa Bani Umayyah, pia alipokea kutoka kwa Khalifa dinari laki mbili, ambapo mzee huyo alipigana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa miaka ishirini na moja na alitangaza kukubali Uislamu kwa sababu tu ya kuponya maisha yake baada ya yeye na watu wengine wa Makka waliposhindwa kabisa.

<sup>96</sup> Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubraa* sehemu ya 1, uk. 193.

<sup>97</sup> Dkt. Taha Husein, kwenye *Al-Fitnat Kubra* yake sehemuu ya 2, uk. 193.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Alishangilia sana Waislamu waliposhindwa na makafiri wa Hawazin huko Hunain, na akasema; “Wataendelea kurudi nyuma hadi wafike baharini.” (Ibn Hishamu aliandika haya kwenye kitabu chake cha Wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Sehemu ya 2, uk. 443).

Khalifa wa tatu si tu aliwamwagia ndugu zake fedha za hazina ya umma, lakini pia aliwapa maeneo makubwa ya ardhi ambayo yalikuwa mali ya umma.

Fadak, kiunga cha miti ya matunda (ambayo ilikujakuwa mali ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu ilipatikana kwa Waislamu bila vita), pia Uthman alikigawa kwa baadhi ya ndugu zake. Fadak ilitakiwa kurithiwa na Fatima Binti yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), chote au sehemu, lakini Abu Bakr aliitaifisha kwa sababu ya hadith ambayo alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba kile kinachoachwa na Mitume kingekuwa sadaka. Hata hivyo, Uthman alimpa Fadak Marwan Ibn Al-Hakam, mtu aliyepewa adhabu ya uhamisho na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)! (*Sunan Abu Dawood* sehemu ya 2, uk. 127).

Uthman hakufuata sera ya wenzake wawili waliomtangulia kuhusu hazina ya umma. Alikuwa akidhani kwamba alikuwa na haki ya kutumia hazina ya Waislamu jinsi alivyotaka mwenyewe. Yeye alikuwa Imam wa Waislamu, na alikuwa na haki ya kufanya atakavyo kuhusu matumizi ya hazina yao. Hii ilikuwa kinyume cha sera sahihi yenye shuruti iliyofuatwa na Khalifa wa pili ambaye alikuwa na tabia ya kutaka mahesabu kamili kutoka kwa wale aliowateua kuhusu matumizi ya hazina ya umma na kuuliza endapo mtu ye yote alijitajirisha mionganoni mwao: “Ulipataje rasilimali hii?” Na alikuwa na desturi ya kurudisha chochote cha ziada katika utajiri wao kwenye hazina ya Kiislamu.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### UMAR NA ABU HURAIRAH.

Umar alimteua Abu Hurairah kukusanya kodi za Al-Bahrain. Alipotambua kwamba Abu Hurairah alitajirika alimwambia: "Nilikupeleka Al-Bahrain ambapo ulikuwa huna hata viatu, hukuwa na uwezo wa kununua viatu vya kustiri miguu yako. Nimepewa taarifa kwamba umeuza farasi kwa dinari elfu moja na mia sita."

**Abu Huraira:** "Nilikuwa na farasi ambao waliongezeka kwa kuzaana."

**Umar:** "Nitazuia mshahara wako na kiasi kile ulichokuwa unapata katika mgawo wa chakula, au uniletee kile ambacho ni ziada ya utajiri wako."

**Abu Hurairah:** "Huna haki ya kufanya hivyo."

**Umar:** "Ndio, Wallahi ninayo, na nitakuumiza mgongo wako." Halafu akampiga kwa mjeledi wake hadi mgongo ukatoka damu na akamuamuru amletee fedha ya ziada.

Abu Hurairah alipopeleka kiasi kilichotakiwa, alisema: "Ninayo matumanini kwamba Mwenyezi Mungu atanipa fidia ya hii." Umar akasema: "Hiyo itakuwa kweli endapo ulipata mali hii kihalali na kulipa kwa hiari kabisa. Wallahi mama yako hakukuzaa ili upate kazi ya ukusanyaji wa kodi ya mapato kutoka Hajar, Al-Yamamah, na sehemu za mbali za Al-Bahrain, na ukusanye fedha yote iwe mali yako, na isiwe mali ya Mwenyezi Mungu au Waislamu. Mama yako alikuzaa ili uwe mchungaji wa punda." Halafu akamfuka kazi.<sup>98</sup>

Ipo dunia ya tofauti baina ya sera hii yenyewe masharti na ile ya Uthman ambaye alikuwa na desturi ya kuwapa ndugu zake mamia ya malaki na wakati mwagine mamilioni ya dinari, bila yeye kuona ubaya wa kufanya hivyo.

<sup>98</sup> Ibn Abu Al-Hadiid, kwenye fasili yake za *Nahjul Balaghah*, Juz. 3, uk. 104

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

### **MISAADA MINGINE KWA WATU WENGINE.**

Ukarimu wa Khalifa haukuishia kwa ndugu zake. Ukarimu huo ulienezwa kwa watu wengine ambao alikuwa anawalipa kiasi kikubwa kama zawadi kwa ajili ya uaminifu wao kwake au kama kitulizo kwa baadhi ya wapinzani wenye uwezo. Alimpa Zubeir dinari laki sita, na Talha Ibn Ubaidullah alimpa dinari laki mbili.<sup>99</sup>

Masahaba hawa wawili walikuwa wajumbe wa jopo la uchaguzi ambalo ndilo lilimfikisha Uthman kwenye Ukhalfa.

Hapana yeoyote kati ya masahaba hawa wawili aliyejua anahitaji msaada wa fedha. Wote wawili walikuwa matajiri wenye miliki na biashara kubwa. Walikuwa na mashamba makubwa mengi na fedha taslim.

Inafaa kuona kwamba historia haisemi kwamba ukarimu wa Khalifa ulielekezwa kwa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao Qur'ani Tukufu iliyatengenea, angalau moja sita (1/6) ya moja ya tano (1/5) ya ngawira.

### **SERA YA MAGAVANA WA MAJIMBO.**

Magavana wa majimbo walifanya yale walijotarajiwa kwa kufuata sera inayofanana na ile ya Khalifa katika kushughulikia hazina ya Waislamu. Imesimuliwa kwamba Waliid Ibn Aqabah alichukua mkopo kutoka kwenye hazina ya Kufah alipokuwa gavana wa jiji hilo. Wakati wa kulipa ulipowadia, mweka hazina Abdullah Ibn Mas'ud alimwambia aliye deni hilo lakinii Waliid hakulipa. Mweka hazina alipodai malipo, gavana alimwandikia Khalifa akilalamika kuhusu mweka hazina. Khalifa alimwandikia mweka

<sup>99</sup> Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra* sehemu ya 1, uk. 77.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

hazina akimwambia amwache Waliid alivyo na deni lake na akamwambia kwamba yeze alikuwa mweka hazina tu wa Khalifa. Alipopata taarifa hii, Ibn Mas'ud alijuuzulu kazi kwa hasira.<sup>100</sup>

Waislamu wa Kufah walikuwa na bahati kuwa na mtu kama Abdullah Ibn Mas'ud ambaye alikuwa na ujasiri wa kumkabili Waliid na kumtaka aliye deni. Waislamu wa Syria hawakuwa na bahati hiyo. Muawiyah alikuwa mtawala dikteta wa Syria ambaye mamlaka yake hayakuwa na mipaka. Alikuwa akiishi kama mfalme, alikuwa anashughulikia hazina ya umma ya Syria kama vile ilikuwa ya kwake binafsi, bila usimamizi wowote. Alitumia hazina ya umma kwa kununua utii na kuungwa mkono na wate-mi wa makabila ya Syria na watu mashuhuri wenye mvuto. Alikuwa ana-jitayarisha kumrithi, Uthman, na alikuwa na muda wa kutosha wa mata-yarisho kama haya.

Kwa kweli, alianza matayarisho yake kuhusu kufanikisha lengo lake wakati wa utawala wa Umar. Ubadhirifu na israfu ulidhihiri kwa Umar mwenyewe. Khalifa wa Pili alipokwenda mpakani mwa Syria, alikasirishwa na maisha yake ya anasa ya hali ya juu. Lakini Muawiyah alimridhisha Khalifa kuhusu ukamilifu wa sera yake, akitumia ujasiri na Falme ya Rumi, kama kisingizio cha kutetea matumizi mabaya ya hazina ya umma.

Ni jambo la kushangaza kwamba Khalifa alimtaka Abu Hurairah kutoa maelezo ya kina ya matumizi ya dinari elfu moja na mia sita, lakini alishindwa kumuuliza Muawiyah ni jinsi gani aliweza kumudu kuendesha maisha yake ya anasa.

Miongoni mwa magavana, si Muawiyah tu aliye kuwa akitumia fedha kwa maslahi yake binafsi. Maafisa walioteuliwa na Uthman walifuata mbini hiyo hiyo kulingana na mamlaka yao na kutokana na usimamizi. Wote walikuwa wanafanya kazi kwa lengo la kubadilisha Ukhilifa kuwa utawala

<sup>100</sup> Al-Baladhuri, kwenye *Ansab Al-Ashraf*, seheku ya 4, uk. 31.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wa kidikteta na ulimwengu wa Waislamu kuwa ufalme wa Bani Umayyah.

Sera hii isiyo na tahadhari ilikuwa na matokeo mengi mabaya: Kukua kwa utajiri wa tabaka la watu matajiri kwenye jamii ya Kiislamu. Wengi wa watu binafsi wenye kubahatika ambao walipokea zawadi kuto-ka kwa Khalifa na maafisa wake aliowateua waliwekeza fedha zote au kiasi fulani katika kununua mashamba na biashara. Mpango huu uliwapa-tia faida kubwa sana. Masahaba wengi waliokuwa wanalipwa mishahara mikubwa wakati wa utawala wa Umar walitajirika sana kwa kuwekeza ziada ya mishahara yao kwenye mashamba na biashara. Utajiri wa masahaba hawa ulitarajiwa kukua kufautana na kupita kwa muda. Uthman alipowaruhusu masahaba kuishi nje ya Madina (kusitisha sharti lililowek-wa na Umar kwa masahaba), wengi wa masahaba hawa matajiri waliona njia mpya za kuongeza utajiri wao. Walinunua majumba, viunga vyta miti ya matunda na ardhi huko Iraq na majimbo mengine. Khalifa wa tatu pia aligawa ardhi ya umma huko Hijaz kwa ndugu zake wengi, marafiki na wanaomuunga mkono.

Mapatano ya kibiashara na mabadilishano ya milki kubwa baina ya wami-likuwa waliokuwa wanaishi Iraq na wenzao walioko Hijaz na Yemen yaliendelea, na Khalifa aliyatilia mkazo mapatano haya ya biashara.<sup>101</sup> Hivyo, mapatano mengi yalifanyika na mitaji ya wafanya biashara hawa iliongezeka haraka.

Masahaba wengi na watu wengi waliibuka kuwa mamilionea. Rasilimali ya Zubeir ilifika dinari milioni 40<sup>102</sup> na kwamba rasilimali ya Talha ilifika dinari milioni 30<sup>103</sup> na utajiri wa Abdul-Rahman Ibn Auf ulifika dinari milioni tatu. <sup>104</sup>

<sup>101</sup> Ibn al-Athiir, kwenye *Al-Kamil*, Sehemu ya 3, uk. 52.

<sup>102</sup> Ibn Saad, kwenye *Al-Tabaqat* yake, sehemu ya 3, uk. 110.

<sup>103</sup> Ibn Saad, kwenye *Al-Tabaqat* yake, sehemu ya 3, uk. 222.

<sup>104</sup> Ibn Saad, kwenye *Al-Tabaqat* yake, sehemu ya 3, uk. 126

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Matokeo mengine ya jinsi Khalifa wa Tatu alivyosimiamia hazina ya umma yalikuwa ni ongezeko la shinikizo kwa walipa kodi wa nchi zilizotekwa. Ukarimu wa Khalifa na maafisa wake aliowateua kwa kazi ya kusimamia hazina ya umma na zawadi zao kwa watu binafsi ulihitaji fedha taslim ambazo hazingepetikana isipokuwa kwa njia ya kutoza kodi kubwa zaidi kwenye zile nchi zilizotekwa. Kitengo hiki hakikutajwa wazi wazi katika historia yetu, kwa sababu maumma yaliyotekwa hayakuwa na mammalaka au sauti ya kisiasa.

Mazungumzo baina ya Khalifa na Amr Ibn Al-Aus (ambaye aliwahi kuwa gavana wa Misri na nafasi yake ikachukuliwa na Abdullah Ibn Abu Sarh) yaonesha ongezeko la shinikizo kwenye nchi zilizotekwa. Khalifa alimwambia Amr: Ngamia wanatoa maziwa mengi zaidi baada ya kuondoka wewe.” (Alimanisha kwamba fedha nyingi zaidi zilikuwa zinaingia kutoka Misri baada ya kufukuzwa kwake). Na Amr alijibu: “Ndio, lakini watoto wao wameangamia!” (alimanisha kwamba kwa kutoza kodi zaidi kutoka kwa watu wa Misri, Wamisri walikuwa wanafanywa maskini).<sup>105</sup>

## KUONGEZEKA KWA UPINZANI.

Upinzani wa awali dhidi ya Khalifa wa tatu ulianzishwa mwanzoni mwa utawala wake na Ammar Ibn Yasir na Al-Miqdad Ibn Al-Asnad, ambao walikuwa masahaba mashuhuri na walikuwa hawana tamaa ya kisiasa na kutajirika. Upinzani huo ulitulizwa mnamo miaka michache ya mwanzo wa utawala wa Khalifa wa tatu, kwa sababu ya kukosa watu wa kuunga mkono na kwa sababu kile walichotarajia kutokea hakikutokea mwanzoni mwa kipindi cha utawala wake.

Hata hivyo, matukio yaliyotokea baadaye yalitoa mchango wa kukua haraka kwa upinzani. Nia ya upinzani ilikuwa ama ya kidini au kisasa na mara nyingine ilikuwa sababu zote mbili.

<sup>105</sup> *Al-Fitnat Al-Kubra*, Sehemu ya 1.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Abdul-Rahman Ibn Awf, mtu ambaye alimteua Uthman na kumweka kwenye mamlaka, alikuwa mmojawapo wa wakosoaji wa mwanzo dhidi ya Khalifa. Hakufurahishwa kuona Khalifa aliyemteua anafuata sera kinyume na ile ya Makhalifa wawili wa mwanzo, japokuwa aliahidi kufanya hivyo wakati wa kuteuliwa. Bila shaka masahaba wengi walim-laumu Abdul-Rahman kwa kumteua Uthman na kumnyang'anya Ali ukhalifa. Walimuona yeye ndiye mwenye kuhusika na sera ya Khalifa katika usi-mamizi wa hazina ya umma na kulazimisha mamlaka ya Bani Umayyah kwa Waislamu.

Abdul-Rahman alibadili moyo wake kuhusu mtu aliyemteua na kugeuka nyuzi 180 kutoka kwenye msimamo wa muunga mkono mkubwa kabisa wa Khalifa na kuwa adui yake na mkosoaji wake.

Mkondo aliouchukua Uthman labda ulimuonesha Abdul-Rahman kwamba ukhalifa ungeendelea kumilikiwa na Bani Umayyah baada ya Uthman. Ndugu wa Khalifa walikuwa na uwezo na mamlaka makubwa sana na walikuwa wanaweza kuweka Ukhalfia kwenye ukoo wao. Wakiwa na mvuto usio na mpaka kwenye akili ya Khalifa, waliweza kumridhisha ili ampe mmoja wao Ukhalfia. Hivyo, Abdul-Rahman kwa kuchelewa kabisa aling'amua kwamba matumaini yake ya kuwa mrithi wa Uthman yalikuwa si ya kweli.

Tunaweza kukumbuka kwamba Ali alimwambia Abdul-Rahman baada ya kumteua Uthman: "Wallahi, ulimpa uongozi ili tu baadaye aurudishe kwako. Mwenyezi Mungu naakutaabisheni wewe na yeye kwa kuchukiana wenywewe kwa wenywewe kwa mfululizo!"

Endapo Abdul-Rahman angekuwa na kumbukumbu nzuri angekumbuka onyo hilo ambalo alilipata kwenye ndoto yake wakati wa kipindi cha siku za Jopo la Uchaguzi. Aliota ndoto ya mbuga ya majani mabichi ambamo ngamia mzuri aliingia na akapita humo bila kula hata jani moja. Ngamia huyo alifuatiwa na ngamia wengine wawili, mmoja baada ya mwingine, na

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

walifuata tabia yake. Halafu alipita ngamia wa nne na alikula kila kitu ali-chowenza. Abdul-Rahman alifasiri ndoto yake kwa kufikiria kwamba ngamia wa nne angekuwa Khalifa wa tatu ambaye hangefuata maadili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na makhalifa wawili wa kwanza katika kusi-mamia hazina ya umma.

Kwa sababu ya ndoto hii, Abdul-Rahman hakutaka kuwa Khalifa wa tatu, asije kuwa ngamia wa nne. Kama Abdul-Rahman angekumbuka ubashiri angetambua kwamba hakuzingatia onyo lililokuwemo kwenye ndoto hiyo. Angetambua kwamba alimteua mtu ambaye asingemchagua na akamwacha mtu ambaye angemchagua. Kama angemteua Ali angeliепusha umma kwenye matukio yote ya msiba ambayo yalitokea baadaye.

Unaweza kukumbuka kwamba Umar pia aliona kwenye ndoto zake kwamba mtu aliingia kwenye bustani ya matunda na aliokota kila tunda lililo bichi na lililoiva na kuyawenza chini ya miliki yake. Huu ubashiri wa aina mbili ulifanana na mwitiko wa kila aliyeota ndoto hizi mbili. Wote wawili walimchagua mwokotaji na mlaji mlafi.

### WAJUMBE WENGINE WAWILI WA JOPO LA UCHAGUZI.

Talha na Zubeir ambao pia walikuwa wajumbe wa Jopo la Uchaguzi, wal-ijiunga na upinzani. Zubeir hakuwa na vurugu sana katika upinzani wake kuliko Talha.

Ni vigumu kuamini kwamba masahaba wawili hawa walimpinga Uthman kwa sababu ya ufuajji wa hazina ya umma. Kama mambo yalivyo, Khalifa aliwapa ndugu zake kiasi kikubwa cha fedha, lakini masahaba hao wawili nao walipata mafungu yao makubwa ya ukarimu wake. Mgawo wa Zubeir ulikuwa dinari laki sita na Talha alipokea dinari laki mbili. Hawakuweza kuzuia msaada wa Khalifa kwa ndugu zake ambapo walihalalisha msaada wa kwao.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Inaonekana kwamba watu hawa wote wawili walikuwa wagombea wa kumrithi Uthman. Umar alipowapa nafasi ya ujumbe wa kuwa kwenye Jopo la Uchaguzi, kwa hakika alikuwa amewapa sifa ya kustahili kuwa katika uongozi. Utajiri mkubwa wa masahaba hao wawili uliongezea umaarufu mbele ya macho yao na macho ya Waislamu wengi. Talha ali-pata watu wanaomunga mkono wengi sana huko Basrah na hivyo hivyo ilikuwa kwa Zubeir huko Kufa. Kama Abdul-Rahman, masahaba hao wawili waliogopeshwa na ukuaji wa haraka wa mamlaka ya ukoo wa Bani Umayyah ambayo yaliwawezesha kuwa washindani na sahaba yejote katika kugombea uongozi.

Ilikuwa inawasumbua wao kudhani kwamba Uthman angemteua Muawiyah au mtu mwengine wa ukoo wa Bani Umayyah kurithi ukhalifa. Mabadiliko ya hali ya mambo yaliashiria kwamba Bani Umayyah wangeubakisha ukhalifa kwenye ukoo wao, hivyo kuziba njia ya Maquraishi wengine wasipate kazi hiyo kubwa. Masahaba hao wawili walitambua kwamba kimya kingetoa mchango kwa ushindi wa Bani Umayyah katika kufanikisha lengo lao. Kwa sababu hii, waliamua kumpinga Khalifa na kujaribu kukomesha utawala wake kabla hajamchagua mtu kutoka ukoo wa Bani Umayyah kuwa mrithi wake. Hali hii ingemwezesha mmojawapo wa masahaba hao wawili kumrithi Khalifa.

## AISHA

Aisha, mke wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia aliungana na upinzani. Akawa mkosoaji wa dhahiri wa Uthman, akimshutumu yeye kwa kuchukua mwelekeo tofauti na ule wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mara kwa mara alionesha nguo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), akisema kwamba nguo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa bado haijachakaa, lakini Uthman alikwisha yaharibu maadili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikuwa na desturi ya kumwita Uthman ‘Naathal’ (Myahudi mwenye ndevu nyingi). Waandishi wa historia wameandika kwamba alikuwa na

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

tabia ya kusema: "Muueni Naathal kwa sababu ametelekeza imani."<sup>106</sup>

Inaonesha kwamba nia yake ilikuwa ni ya kisiasa tu wala si ya kidini. Hakukasirishwa na ukiukwaji wa sharia ya Kiislamu wa Uthman, kwa sababu yeye mwenyewe alijiruhusu kukiuka amri kubwa zaidi ya Mwenyezi Mungu. Aisha alimpinga Ali ambaye alishikamana sana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na maadili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikuwa mpinzani mwenye vurugu zaidi wa ndugu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuliko katika upinzani kwa Uthman. Aisha alimkosoa Uthman kwa sababu aliwaumiza baadhi ya masahaba na alifuja hazina ya Waislamu, bado alianzisha vita ambayo vilisababisha vifo vya Waislamu maelfu. Kuua Waislamu ni dhambi kubwa zaidi kuliko kuwajeruhi au kupora kiasi fulani cha fedha zao.

Nia yake katika kumpinga Uthman ilifanana na ile ya Talha na Zubeir. Aisha alitaka binamu yake Talha au shemeji yake Zubeir amrithi Uthman. Ukuaji wa mvuto wa Talha katika upinzani dhidi ya Khalifa ulimfurahisha sana Aisha.

At-Tabari aliandika kwamba Aisha alimwambia Ibn Abbas: "Wewe ni mtu wa kuelewa, mwenye busara na uwezo wa kujieleza. Kwa jila na Mwenyezi Mungu ninakuomba usiwazuie watu kwenda kumuunga mkono Talha. Hali ya Uthman imedhihiri. Watu kutoka miji mikuu mbalimbali wamekusanyika kwa tukio kubwa ambalo litatokea hivi karibuni. Nimepata taarifa kwamba Talha tayari anadhibiti nyumba zenye hazina ya umma na funguo zote anazo yeye. Nadhani, Mwenyezi Mungu, akipenda atafuata njia ya binamu yake Abu Bakr." Ibn Abbas alimjibu kwa ukali, akasema: "Mama, kama jambo lolote litamtokea Uthman, watu watakim-bilia kwa mtu wetu (Ali)." Aisha, kama mambo yalivyo, yeye

<sup>106</sup> Al-Tabari, Historia ya Mitume na Wafalme, kuhusu matukio ya mwaka 36, uk.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

hakukubaliana naye, lakini alimwambia: “Ewe Ibn Abbas, mimi sitaki kukufanya uadui wewe au kubishana na wewe.”<sup>107</sup>

Aisha alikuwa anatazama matukio kwa macho ya Talha na Zubeir. Matumaini yake kwamba mmoja kati ya hao wawili angefika kwenye ukhalifa kuitia ushirikiano na Uthman yalikuwa yanafifia pole pole kwa kulinganishwa na ukuaji haraka wa uwezo na mamlaka ya Bani Umayyah na Uthman kuendelea kuwa Khalifa. Ilidhihiri kwa Aisha na masahaba hao wawili kwamba Khalifa angefuata ushauri wa watu kama Marwan na Muawiyah tu, na kwamba washauri hawa wangemshauri kuchagua mrithi kutoka ukoo wa Bani Umayyah.

Aisha na masahaba hawa wawili walifikiri kwamba kimya chao kingewasidia Bani Umayyah katika kufanikisha lengo lao. Kwa sababu hii masahaba hawa wawili wakapiga ukelele dhidi ya Khalifa, na Aisha aliwataka Waislamu wamuuwe.

### AMR IBN AL-'AS.

Amr Ibn Al-'s alijiunga na upinzani. Mwanasiasa huyu hakuwa na tamaa ya kuwa Khalifa. Yeye hakuwa mionganoni mwa masahaba wa siku za mwanzo au mjumbe wa Jopo la Uchaguzi, wala hakuwa na mvuto unaohitajika kumfanya yeye atamani kufika kwenye kazi ya ukhalifa. Upinzani wake ulikuwa msukumo wa nia ya kutaka kulipa kisasi. Al-'s alikuwa gavana wa Misri wakati wa utawala wa Umar. Alitaka kuendelea kwenye kazi ya ugavana, lakini Uthman alimfukuza na badala yake akamteua Abdullah Ibn Saad Ibn Abu Sarh. Alirudi Madina, akangojea fursa ya kumrukia Khalifa. Aisha na watu wengine walipoanza kampeni yao dhidi ya Uthman, Amr akawa mchochezi aliyefahamika sana. Alitumia akili yake na utashi wake katika kuwachochea watu dhidi ya Khalifa.<sup>108</sup>

<sup>107</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, *Fasili za Nahjul Balaghah*, Juz. 2, uk. 506.

<sup>108</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil* sehemu ya 3, uk. 82.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Uthman alipouawa, Amr aliungana na waliokuwa wanataka kulipa kisasi cha damu ya Uthman kwa sababu Muawiya alimuahidi ugavana wa Misri.

### UPINZANI KUTOKA KWA MASAhaba WASIOKUWA MAQURAISHI.

Masahaba kutoka kabilia la Maquraishi hasa zaidi waliskumwa na tamaa ya kisiasa katika upinzani wao kwa Uthman. Upinzani uliotokana na msukumo wa kidini ilitoka kwa masahaba mashuhuri wasio Qureishi. Aliyefahamika sana mionganoni mwao katika historia ya wakati huo alikuwa:

#### ABU DHARR.

Khalifa wa Tatu alipompa binamu yake Marwan dinari milioni tano, na Zayd Ibn Thabit dinari laki moja, na Harith, kaka yake Marwan, dinari laki tatu, Abu Dharr alipiga kelele mara nyingi akikariri aya ya Qur'ani ifuatayo: “**Wape habari ya adhabu kali kwa wale wanaokusanya na kuhodhi dhahabu na shaba na hawazitumii katika njia ya Mwenyezi Mungu.**”

Uthman aliwatura wajumbe wake kwa Abu Dharr wamkataze asikariri maneno hayo ya Qur'ani. Abu Dharr alikataa, akasema: “Uthman anataka kunizua mimi nisikariri Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kuwakanya wale wanaoacha kutii amri ya Mwenyezi Mungu? Wallahi inapendeza zaidi kwangu mimi na vizuri zaidi kwangu mimi kumridhisha Mwenyezi Mungu kwa kumkasirisha Uthman kuliko kumkasirisha Mwenyezi Mungu kwa kumridhisha Uthman.”<sup>109</sup> Msimamo huu ulimkasirisha Uthman.

<sup>109</sup> Ibn Abu Al-Hadeed, Fasili za Nahjul Balaghah, Juz. 1, uk. 240.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Haikuwa vigumu kwa Uthman kutatua tatizo la Abu Dharr na wakosoaji wengine wote, Abu Dharr mwenyewe alimwambia Uthman ufumbuzi wa tatizo hilo. Siku moja alimwambia ‘Fuata njia ya makhalifa wawili walioikutangulia na hakuna mtu atakaye kukosoa wewe.’ Lakini Khalifa hakuwa na mawazo ya aina hii. Alitaka kufumbua tatizo hilo kwa kumwadhibu yejote aliyezea kukmpata. Kwa dhahiri, hakuweza kutambua kwamba kulitibia

tatizo hili la ukosoaji wenye ukweli ndani yake, kwa kutumia nguvu kungeweza kuletea matatizo makubwa zaidi.

### ABU DHARR UHAMISHONI.

Ilikuwa vigumu Khalifa kuwaadhibu wakosoaji Maquraishi. Tayari walik-wishakuwa na uwezo wa mamlaka makubwa mno yeye kuweza kuwaadhibu. Abu Dharr na wengine kama yeye, japokuwa walikuwa na sifa nzuri za Kiislamu, wala hawakuwa na uwezo, ama matajiri. Khalifa alichagua adhabu ya aina ambayo ilikuwa haistahili na haitekelezeki kwao. Alichagua adhabu ya kumpeleka uhamishoni Abu Dharr, ambayo imeainishwa na Qur’ani kwa ajili ya watu walioko vitani dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.), na wenye kufanya ufisadi juu ya ardhi. Abu Dharr hakuwa mionganoni mwa hawa. Yeye kwa usahihi zaidi aliquwa sahaba mwadilifu, ambaye matamano yake yalikuwa kukataza maovu na kuamrisha mema. Hakutoa changamoto dhidi ya mamlaka ya serikali (Khalifa), wala hakushawishi watu wamuasi yeye.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikosolewa na mnafiki ambaye alimwambia: “Lazima ufanye haki katika kugawa ngawira mionganoni mwa Waislamu.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakumhamisha, wala hakumwadhibu. Alimwambia tu yeye: Laana ikuangukie. Kama mimi sikutenda haki nani atakaye fanya hivyo?”

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Abu Bakr aliwaambia watu waliomchagua: “Mnitii mimi almuradi mimi nina mtii Mwenyezi Mungu. Kama nisipomtii Yeye, hamtawajibika nyinyi kunitii mimi.”

Umar alikuwa na desturi ya kusema: “Mnapoona mimi nimepotoka, jari-buni kunirejesha kwenye njia iliyonyooka.”

### ABU DHARR NA MUAWIYA.

Uthman hakuchukua msimamo wa wale waliomtangulia yeye. Alimhamisha Abu Dharr kwenda Syria, akamweka chini ya mamlaka ya Muawiyah, ambaye kwa hakika alikuwa serikali ndani ya serikali. Alipoona israfu ya Muawiya na ufujaji wake wa hazina ya umma, Abu Dharr aliinua sauti dhidi yake. Muawiya alipojenga Ikulu yake maarufu iliyopewa jina la *Al-Khadra*, Abu Dharr alimwambia: “Kama fedha iliyojenga jumba hili inatoka kwenye hazina ya Waislamu, ni wizi. Kama inatoka mfukoni mwako, ni ufujaji.”

Abu Dharr alikuwa na desturi ya kupiga kelele mlangoni kwa Muawiyah, akisema: “Ewe Mwenyezi Mungu, walaani wale wanaoamrishwa mema na kisha wao wenyewe hawatendi mema. Na uwalaani wale wanokataza maovu na wao wenyewe hutenda maovu.

### UHAMISHO WA KUDUMU.

Hali hii ilimkera Muawiyah. Alilalamika kwa Khalifa kuhusu Abu Dharr. Khalifa alimuita arudi Madina na alisafirishwa kwenda Madina kwa njia ya kikatili sana.<sup>110</sup> Abu Dharr alipofika Madina, Khalifa alimuona bado anang’ang’ania kwenye msimamo wake wa ukosoaji dhidi ya serikali yake. Kwa sababu hii alimuamuru aondoke Madina. Abu Dharr aliomba

<sup>110</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu ya 3, uk. 56.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

ruhusa arudi Damascus, au aende Misri, au Makka, kwa mujibu wa riwaya zingine. Khalifa hakumruhusu kufanya hivyo. Alimuamuru aende kwenye jangwa la Najd, akimwambia: “Elekea upande huu na usiende mbele zaidi ya Al-Rabathah.”

Khalifa aliwaagiza watu wasiseme na Abu Dharr wala kumuaga. Abu Dharr alipokuwa anaondoka, Marwan alitembea naye kwa lengo la kuwazuia watu wasiseme naye. Hakuna mtu aliyediriki kuwa naye wakati anaondoka isipokuwa Imam Ali, wanae wawili Hasan na Husein, kaka yake Aqil na Ammar Ibn Yasir. Kwa kufanya hivi, walikuwa wamekiuka amri ya Khalifa. Hali hii iliongeza kuzidi kuzorota kwa uhusiano wa Imam na Khalifa. Maneno ya mwisho ya Imam kwa Abu Dharr yalikuwa yafuatayo:

“Ewe Abu Dharr, uliwapinga watawala kwa sababu hawakumtii Mwenyezi Mungu. Weka matumani yako Kwake. Watawala walikuogopa wewe kwa ajili ya maslahi yao binafsi, na wewe ulihofia wangeitia hatarini dini yako. Waachie mikononi mwao yale wanayotaka kuyalinda na kimbia uchukue yale ambayo unataka kuyalinda. Watawala hawa wanataka kuwa navyo vile vitu ambavyo wewe ulijaribu kuwanyang’anya. Utatambua ni nani mwenye hatima ya furaha na wakuonewa wivu. Kama mbingu na dunia zikifunga milango juu ya mtumishi mwadilifu wa Mwenyez Mungu, Yeye atampa mlango wa kutoke. Uache ukweli uwe ndio rafiki yako na uwongo uwe ndio tu adui yako. Endapo ungekuwa umekubalia hiyo njia yao, wao wangekupenda; na endapo ungegawana ngawira na wao wangekuamini.”<sup>111</sup>

Baadhi ya waandishi wa historia wanassema Abu Dharr aliondoka Madina kwenda Rabathah kwa hiyari, lakini inaonesha kwamba hakuna uwezekano wa Abu Dharr kuchagua kuwa bedui wa kuishi jangwani badala ya kuishi kwenye jiji la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, upo

<sup>111</sup> *Nahjul-Balaghah*, sehemu ya 2, uk. 12-13.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

uhakika kwamba alihamishwa na kupelekwa Damascus kabla hajakwenda Rabathah, halafu akarudishwa Madina. Hakushauriwa kuhusu uhamisho wake wala kurudi kwake.

Abu Dharr aliweka makazi yake Rabathah, wakati wote alishi maisha ya taabu na ufakiri usiovumilika hadi alipoaga dunia. Alipokufa, hapakuwepo na watu wa kutosha kumzika. Endapo isingekuwa Abdullah Ibn Mas'ud na wenzake wachache (pamoja na Malik Al-Ashtar) kupita njia hiyo, Abu Dharr asingeziwa.

Uhamisho wa Abu Dharr kwenda Rabathah ulikuwa ni kosa kubwa la kisia-sa kwa upande wa Khalifa. Waislamu wema walishrushwa na ushamisho wa sahaba huyu mashuhuri, kwani yeze alikuwa na msimamo usiotetereka katika jitihada zake za kuwa mkweli. Alikuwa kipenzi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kuhusu yeze: "Hapana yezote chini ya mbingu na juu ya ardhi ambaye ni mkweli zaidi ya Abu Dharr." Waislamu waadilifu waliskitishwa sana kwa yale yaliyomtokea Abu Dharr kama walivyosikitishwa kwa yale yaliyowatoka wale walieuufu vifo vya kishahidi amba walikuwa mashuhuri kwa kuwa wakweli, amba roho zao zilijazwa kujitolea katika kuyafikia maadili ya kiwango cha juu ambayo waliishi na kufa nayo.

### **ABDULLAH IBN MAS'UD.**

Abdullah Ibn Mas'ud sahaba mwengine mashuhuri ambaye sio Qureishi, pia aliungana na upinzani. Kama Abu Dharr, Abdullah hakuwa na tamaa ya kisiasa au utajiri wa kidunia. Mtu huyu alikuwa mweka hazina wa jimbo la Kufa na alijiuzulu kazi kwa hasira Khalifa alipomwandikia: "...Wewe ni mweka hazina wetu tu, mwache Waliid (gavana wa Kufa wa ukoo wa Bani Umayyah) alivyo na deni lake alilokopa kutoka hazina." Riwaya inasema kwamba Abdullah Ibn Mas'ud alikuwa akitoa hotuba ya kila wiki ambapo alijumuisha maneno yafuatayo: "Hakika Kitabu cha Mwenyezi Mungu

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

ndicho chenyeye ukweli hasa, na mwongozo mzuri zaidi ni mwongozo wa Muhammad. Na tendo baya zaidi kuzidi yote ni lile lisiloendana na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume Wake (s.a.w.w.). Kwani kila tendo la aina hiyo ni bidaa na kila bidaa ni uzushi na kila uzushi mwisho wake ni Jahannamu.”<sup>112</sup>

Waliid alimpa taarifa Khalifa kuhusu hotuba za Ibn Mas’ud zilizojaa vijembe na khalifa alimuuta. Ibn Mas’ud alipoingia kwenye Msikiti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Uthman alisema na kuwaambia jamaa: “Mtu aliyeingia msikitini hivi punde ni mdudu mdogo aliemuovu ambaye hus-ababisha mtu kutapika na hutoa kinyesi juu ya chakula anamotembea.” Ibn Mas’ud akasema: “Mimi sipo hivyo, lakini mimi nilikuwa sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye Vita vya Badr, Uhud, Hudaybiyah; Khandak na Hunain.” Uthman alimuagiza mmojawapo wa watumishi amtupe nje ya Msikiti. Mtumishi alimbeba juu kwenye mabega yake nje ya Msikiti kwa nguvu.<sup>113</sup>

Baadhi ya mbavu za Abdullah zilivunjika. Halafu Khalifa akamnyima mshahara. Abdulah aliishi kwa kipindi cha miaka mitatu baada ya hapo, akiendeleza upinzani wake kwa Uthman. Alipokufa aliasia kwamba Uthman asisalie maiti yake, na Ammar Ibn Yasir alikuwa ndiye wasii wake. Ammar alimzika Abdullah bila kumwambia Khalifa kuhusu kifo chake.

### **NA AMMAR IBN YASIR.**

Ammar alikuwa mtu aliyeingia kwenye upinzani mwanzoni kabisa. Aliwataka Waislamu wapigane na jamii ya Maquraishi kwa sababu ilim-chagua Uthman kwa uongozi na ikamwacha Ali. Kama alivyoona Ali, Ammar aliona katika mwenendo wa Uthman kuwa kama daraja ambamo ukhalifa ungepita kutoka kwa masahaba wema wa Muhammad kwenda

<sup>112</sup> Dr. Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra* sehemu ya 1, uk. 160.

<sup>113</sup> Dr. Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra* sehemu ya 1, uk. 160-161.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

kwa ukoo wa Bani Umayyah. Mfuatano wa matukio ulikuwa na hatima ya kuthibitisha tu kwa Ammar na wenzake yale waliyoyatarajia. Yaliyomtokea Abu Dharr na Abdullah Ibn Mas'ud yalimfanya Ammar awe makini zaidi kwenye upinzani wake dhidi ya Uthman. Ibn Yasir hakuwa mtu wa aina ya wale wanaonyamaza kimya anapoona jambo linalokinzana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Upinzani wa aina hiyo ulitarajiwa kumweka Ammar kwenye hatari ya kupewa adhabu kali sana kutoka kwa Khalifa. Uthman alitaka kumhamisha kama alivyofanya kwa Abu Dharr, lakini Ali na masahaba wengine walikataa vikali, hali ambayo ilimfanya Khalifa amtishie kumhamisha Ali mwenyewe. Lakini Ali alimwekea pingamizi asifanye hivyo.

Palikuwepo na vito vyenye thamani kubwa kwenye hifadhi ya hazina na Uthman aliwapa zawadi wake zake vito hivyo. Watu wakasema kuhusu tukio hilo, na Uthman alikasirika kuhusu mzungumzo hayo ya watu. Alisema wakati alipokuwa anatoa hotuba: "Tutachukua kile tunachokihitaji kutoka hazina hata kama watu wengine hawatafurahi." Ali alijibu: "Halafu utazuiwa na kukomeshwa." Na Ammar akasema: "Ninamshuhudia Mwenyezi Mungu kwamba mimi ni mtu wa kwanza mionganii mwa watu wasiofurahia tukio hilo." Uthman alijibu kwa hasira: "Wewe unathubutu kuniambia hivyo mimi? Mchukueni."

Alikamatwa na Uthman akaenda pale alipozuiliwa Ammar. Alimpiga Ammar hadi akazirai, na alidumu katika hali hiyo hadi akaikosa Swala ya Adhuhuri, Alasiri na Magharibi. Alipopata fahamu, alichukua udhu, akaswali swala zake, na akasema: "Sifa zote zinamstahiki Yeye Mwenyezi Mungu. Hii si mara yangu ya kwanza kuteswa kwa sababu ya jithada zangu katika njia ya Mwenyezi Mungu."<sup>114</sup>

<sup>114</sup> Dr. Taha Husein, *Al-Fitnat Al-Kubra* sehemu ya 1, uk. 167.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Imesimuliwa kwamba kundi la masahaba (mionganini mwao akiwemo Talha, Zubeir, Al-Miqdad na Ammar) lilimwandikia Uthman barua ambamo likosoa idadi fulani ya matendo ya Uthman, lilimshutumu yeye kwa kuisaliti dini yake na kumwonya kwamba kundi hilo lingepigana naye. Ammar aliwasilisha barua hiyo kwa Uthman. Uthman aliposoma sehemu ya barua hiyo, alimuuliza Ammar: "Ni wewe peke yako ambaye ni jasiri mionganini mwao kunikabili mimi na hii?" Ammar akajibu: "Mimi ni mshauri wako bora mionganini mwao."

Uthman akamwambia: "Mwana wa Sumayah (mama yake na Ammar) umedanganya." Ammar alijibu hasira: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu mimi ni mwana wa Sumayyah na Yasir" Uthman akawaagiza watumishi kumlaza Ammar chini na kumshika miguu na mikono yake. Halafu Uthman akampiga mateke tumboni. Maumivu hayo yalisababisha apate maradhi ya henia. Ammar alikuwa mzee na dhaifu, akazirai.

Ammar alikuwa ndiye msemaji sana na kwa sauti kubwa sana dhidi ya Uthman. Upinzani wake kwa Uthman ulidhiiri kuwa mkubwa kwa sababu ya sifa yake njema sana na kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyoyasema kuhusu yeye.

### UPINZANI KUTOKA NJE YA MADINA.

Utarawala wa kidikteta wa Maquraishi katika jamii ya Kiislamu ulianza mwanzoni mwa utarawala wa Khalifa wa kwanza. Kwenye hoja yake kuhusu uongozi wa Maquraishi huko kwenye mkuutano wa Saqifa, Abu Bakr alisema kwa kuwaambia wazalendo wa Madina kwamba Waarabu hawangekubali uongozi wa mtu asiyé Qureishi. Kwani Qureishi ilikuwa jamii ya daraja la juu sana mionganini mwa Waarabu na jamii ya Jiji linaloheshimiwa sana.

Baada ya kuambiwa haya, watu wa Madina walikubali uongozi kuchukuliwa na Maquereishi. Hivyo masahaba wengi wa Makka na Madina wali-

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

iona hali hiyo kama ubora wa kikabila. Kwa hoja hii mamlaka ya juu ya Maquraishi yalianzishwa, japokuwa Imani ya Uislamu, dini ya usawa, inakataza aina yoyote ya ukabila.

Ukabila huu ulikua wakati wa utawala wa Khalifa wa Pili na kufika kwenye kilele chake wakati wa kipindi cha utawala wa Khalifa wa Tatu. Fikira ya ubora wa Maquraishi ilikua wakati wa utawala wa Uthman na kufika mbali zaidi hadi kuiona dunia ya Waislamu kuwa Ufalme wa Maquraishi. Hatima ya hali hii ilikuwa ionekane kutokuwapendeza watu wenyewe kuelimika ambao walitambua kwamba Uislamu ni dini ya usawa na udugu. Ujumbe wa Uislamu unalengo la kumnyanyua kila Mwislamu na kuwapa hadhi wote waomuamini Mwenyezi Mungu badala ya kuwapa hadhi wachache kwa ghamrama ya mamilioni wengine.

Waislamu waadilifu walisumbuliwa na dai la Maquraishi la ubora wao kwa jina la dini, ambapo Bani Umayyah ambao walichukua nembo ya uongozi mionganini mwa Maquraishi hawakuwa waadilifu hata kidogo mionganini mwa Waislamu.

Cheche ya upinzani nje ya Madina ilianza Kufah. Watu wake walio wengi walikuwa wanatoka Yemen. Riwaya zinasema kuwa baadhi ya viongozi wa Jiji hilo, walipomtembelea gavana, walizungumzia kuhusu viunga vyaya miti ya matunda vya Kufa. Mazungumzo baina yao na Kamanda Mkuu wa Polisi wa Jiji Abdul-Rahman Ibn Khumeis yalifanyika kama ifuatavyo:

**Ibn Khumeis:** “Ningependa viunga vyote vingemilikiwa na gavana, na nyinyi watu wa Kufa, mmemiliki viunga vizuri kuliko viunga hivi.”

**Maliki Al-Ashtar:** “Mtake gavana amiliki viunga vizuri zaidi ya viunga hivi lakini hatutaki amiliki rasilimali zetu.”

**Ibn Khumeis:** Ni vipi utashi wangu ulikuumiza na kufanya wewe ukunje uso mbele yangu? Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kama gavana akitaka

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

hivyo, atachukua viunga hivi.”

**Al-Ashtar:** “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kama akitaka hivyo, hatapata kitu.”

Said alisema kwa hasira: “Viunga vyote hivi vya matunda ni mali ya Maqraishi.”

**Al-Ashtar:** “Unataka kufanya kile tulichokipata kwa mikuki yetu na kile ambacho Mwenyezi Mungu ametupatia, kuwa kiunga chako na watu wako?”

Na watu wengine wakazungumza wakimuunga mkono Al-Ashtar.

**Al-Ashtar:** “Yupo mtu yejote hapa? Mtu huyu asiruhusiwe kufanikisha alichosema.”

Watu walimrukia Ibn Khumeis, wakamkanyaga sana hadi akazirai. Halafu wakamvuta. Hatimaye uso wake ulimwagiwa maji hadi akapata fahamu.

Ibn Khumeis alimwambia Said: “Watu uliowachagua wameniu.”

**Said:** “Hakuna mtu atakaye kuwa na mimi jioni hii baada ya tukio hili.”

Waandishi wengine wa historia wameandika kwamba baadhi ya watu walisema mbele ya Said kuhusu ukarimu wa Talha Ibn Ubaidullah na kwamba maoni ya magavana na watu waliomtembelea yalikwenda kama ifuatavyo:

**Said:** “Mtu mwenye utajiri kama wa Talha na miliki zake lazima awe karimu. Endapo ningemiliki mali kama ya Talha, ningekufanyeni muishi katika mafanikio.”

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Kijana kutoka khabila la Asad akasema: "Ningependa umiliki viunga vyote vilivyomo pande zote mbili za mto wa Euphrates." Usemi huu uliwaudhi baadhi ya watu waliokuwepo hapo na kusababisha wamkemee kwa ghadhabu kijana huyo. Baba yake kijana huyo akasema: "Bado mdogo sana. Msimwadhibu kwa yale aliyoyasema." Wale watu walioudhika wakasema: "Anamtaka Said achukue rasilimali zetu." Walimrukia kijana huyo. Baba yake akataka kumtetea. Watu hao walimpiga baba na mwanae hata kupoteza fahamu. Watu wa khabila la Asad wakapata taarifa ya tukio hili na walikwenda wakizunguka Ikulu. Said aliwapa maelezo ya kuridhisha wakaondoka.<sup>115</sup>

Maelezo yote ya pande mbili ya tukio hili yanakubaliana kwamba Al-Ashtar na wengine waliokuwa hapo walikaa mbali na gavana na wakasema maneno ya upinzani dhidi ya Said na Khalifa bila hofu. Ni kwenye tukio hili ndipo upinzani ulipojitokeza Kufah. Ama taarifa ya kwanza au ya pili ndio ilikuwa ya kweli, tukio hili linaonesha kwamba katika kipindi hicho watu walichoshwa na mwenendo wa Maquraishi, viongozi wake, madai yao makubwa ya ghilba yao iliyokithiri.

Tukio hili kwa hakika ndilo lililovunja nguvu ya Maquraishi. Mfuatano wa matukio ulikuwa na mwelekeo kwenye mlipuko wa kisiasa usio epukika. Abdullah Ibn Mas'ud alitoa hotuba ambazo zilikosoa sera za Uthman na maafisa wake, zilisaidia kuwafanya watu wa Kufah waelewe tatizo la rushwa serikalini. Uhamisho wa Abu Dharr pia ulikuwa kipengele kilichotia chachu kwenye upinzani. Tumekwishesema kwamba Al-Ashtar na wengine kutoka Kufa walikuwa pamoja na Ibn Mas'ud wakati wa maziko ya sahaba huyu aliyeonewa. Yale yaliyomtokea Abdullah Ibn Mas'ud baadaye ni kipengele kingine pia. Watu wa Kufa walikuwa wanamheshimu sana sahaba huyu mashuhuri ambaye alitupwa nje ya Msikiti Mtukufu kwa nguvu kwa amri ya Khalifa.

<sup>115</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, Juz. 3, uk. 71-72.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Watu wa Kufa walimfahamu Ammar Ibn Yasir na sifa yake inayong'ara katika Uislamu. Alikuwa gavana wa jiji lao wakati wa utawala wa Umar. Walikuwa wanamheshimu sana huyu sahaba mashuhuri. Yale yaliyomtokea wakati wa utawala wa Khalifa wa tatu pia yalikuwa ni kipengele kilichoongezeka na ambacho kilifanyiza mlipuko wa upinzani kutoka kwa watu waadilifu wa Kufa kuwa jambo la kutegemewa. Moto ulikuwa karibu uwake na ulipata cheche yake kwenye tukio lililomhusu Said.

Upinzani wa Kufa ulipata adhabu ile ile aliyopewa Abu Dharr. Uhamisho ikawa adhabu ya kawaida kwa anayeikosoa serikali; na Damascus ikawa kituo cha wakosoaji waliohamishwa. Wakiwa huko walipata adhabu zao kutoka kwa Muawiyah, mtu mwenye mamlaka makubwa kwa serikali ya Kiislamu.

Watu wa Kufa waliohamishwa waliwekwa kwenye kanisa la Mariamu. Muawiyah alikutana nao, aliongea nao na aliwafundisha. Mada ya mafunzo yake ilikuwa ni sifa maalumu ya Maquraishi katika historia ya Uislamu na kabla ya historia ya Uislamu. Alijaribu kuthibitisha ubora wa Maquraishi kwa ukweli kwamba jamii zingine zote zilipata kuvamiwa isipokuwa Maquraishi ambao walilindwa na Mwenyezi Mungu. Pia alisema kwamba Mwenyezi Mungu alifanya ukhaifa uwe mikononi mwa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wenye asili ya Qureishi. Hivyo, wao ndio wenye sifa za kustahili uongozi. Halafu akawaambia kwamba Mwenyezi Mungu aliwalinda Maquraishi ambapo bado hawajawa waumini." Mnafikiri kwamba Mwenyezi Mungu hatalindwa wakati ambapo ni wafuasi wa dini Yake."<sup>116</sup>

Aliwaambia kwamba Abu Sufyani (baba yake Muawiya) alikuwa mtu mwenye kuheshimiwa sana na mtoto wa mtu aliyekuwa anaheshimiwa sana mionganoni mwa Maquraishi isipokuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), halafu akaongeza: "Nadhani kwamba endapo Abu Sufyani angekuwa baba

<sup>116</sup> Ibn al-Athiir, Al-Kamil, Juz. 3, uk. 70.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

wa watu wote, watu wote wangkuwa na hekima.”<sup>117</sup>

Said Ibn Sa’sa’ah Ibn Souhan alimuonesha jinsi mfano ule usivystahiki kwa mtu huyo aliyetajwa, kwa kusema: “Adamu alikuwa bora zaidi kuliko Abu Sufyani. Mwenyezi Mungu alimuumba kwa mkono Wake, akapuliza pumzi ndani mwake kutoka kwenye roho Yake na akawaamuru malaika wamsjudie yeye. Alikuwa baba wa binadamu wote. Bado tunaona miongoni mwao wema na waovu, wapumbavu na wenye busara.”

Mantiki ya Muawiyah ilijaa upotoshaji wa ukweli. Alisema kwamba baba yake Abu Sufyani alikuwa mtu bora zaidi baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) (pamoja na Abu Bakr na Umar).

Alisahau kwamba ulinzi wa Mwenyezi Mungu uliofanywa kwa Maquraishi hakuwa kwa ajili ya Abu Sufyani, wanawe na wengineo kuto-ka kabila la Qureishi. Kwa usahihi zaidi, ulinzi huo ulikuwa kwa ajili ya ile Nyumba Tukufu na kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), mbora aliyetokana na uzao wa Ibrahim. Pia hilo lilikuwa ni jibu la dua ya Ibrahim, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye Qur’ani Tukufu inatuambia:

**“Na aliposema Ibrahim: ‘Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye hu uwe mji wa amani na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.’ Akasema: ‘Na mwenye kuku-furu pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.”<sup>118</sup>**

Muawiya hakufahamu kwamba ukhalifa kwenye uzao wa Ibrahim, pamoja na Maquraishi ulifanywa kwa utezi wa Mwenyezi Mungu. Utezi huo hakuwfikia madhalimu mionganoni mwao. Tunasoma kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu:

<sup>117</sup> Ibn al-Athiir, Al-Kamil Juz. 3, uk. 71.

<sup>118</sup> Qur’ani Tukufu (2:126).

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

**“Na Mola wako Mlezi alipomjaribu Ibrahim kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza, akamwambia; ‘Hakika nitakufanya uwe Imam wa watu.’ Ibrahim akasema: “Je, na katika vizazi changu pia? Muweza wa Yote akasema: ‘Ahadi yangu haitawafikia wenyewe kudhulumu.<sup>119</sup>**

Historia inatuambia kwamba Muawiya aliwaachia huru wale waliopewa adhabu ya kuhamishwa na waliporudi Kufa waliendelea na upinzani wao. Kwa hiyo walihamishwa tena na kupelekwa Humus. Waliwekwa chini ya mamlaka ya Abdul-Rahman Ibn Khalid Ibn Al-Walid. Adhabu hii ilikuwa kali zaidi ya kukasirisha kuliko ile ya Muawiya. Walimuonesha kutubia, na akawaachia huru. Al-Ashtar alikwenda kwa Khalifa, na Khalifa akamruhusu aende popote anapotaka. Alirudi tena Humus. Upinzani ulipozidi kuongezeka huko Kufah, Al-Ashtar alirudi na kujiunga na upinzani. Yeye na Yaziid Ibn Qaisw waliongoza umati wa watu kwenda sehemu iitwayo Al-Jarah kumzuia Said Ibn Al-Auss asiingie tena Kufa. Said alirudi Madina na watu wa Kufah walimtaka Uthman amweke Abu Musa (a.s.) kuwa gavana wa Kufa badala ya Said.

Tunaweza kutambua uchungu ambao watu waliopewa adhabu ya kuhamishwa walihisi tunaposoma ujumbe kutoka kwa Malik Al-Ashtar kwenda kwa Uthman kama jibu la barua aliyando khalifa kwa watu wa Kufah akiwakemea wapinzani:

“Kutoka kwa Malik Ibn Al-Harth kwenda kwa Khalifa mwenye mtihani na mtenda dhambi ambaye anapotaka kutoka kwenye maadili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kukipatia kisogo Kitabu cha Qur’ani Tukufu.

“Tumesoma ujumbe wako. Lazima ujizue wewe na maafisa wako msifanye udhalimu, uchokozi na kuwapa adhabu ya uhamisho watu wetu waadilifu. Hali hii itatufanya turidhike na kukutii wewe. Ulidai kwamba sisi ndio wakosefu. Huu ni ubunifu ambao ulisababisha wewe kuangamia

---

**119 Qur’ani Tukufu (2:124).**

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

(kiroho) na ulikufanya wewe ufikirie upendeleo ni haki na batili kuwa usawa. Kuhusu tunachotaka sisi, tunataka ubadilike na utubu, na umwombe Mwenyezi Mungu msamaha Wake kwa kuwatia hatarini watu wetu wema, unatutoa kwenye majumba yetu na kututawala kutumia vijana wetu. Tunataka umteue Abdallah Ibn Qais, Abu Musa (a.s.), kuwa gavana wa Jiji letu. Tunakuomba uwaweke watu wako wawili hawa, Waliid na Said mbali na sisi.”<sup>120</sup>

Khalifa alijibu kwa kumteua Abu Musa kuwa gavana wa Kufa. Upinzani dhidi ya sera ya Khalifa ulienea sehemu zingine nyingi kuvuka mipaka ya Kufa. Ulienea hadi Basra huko Iraq na pia Misri. Waandishi wa historia wanatuambia kwamba Muhammad Ibn Abu Bakr na Muhammad Ibn Abu Hudhaifah walikwenda Misri na kuwachochea watu waasi dhidi ya Uthman. Kwa kuwepo kwa Abdullah bin Saad Ibn Abu Sarh huko Misri kama gavana, hawa Muhammad wawili hawakuhitaji kupeleka Misri ushahidi wa nyongeza unaohusu uovu serikalini. Imesimuliwa kwamba mtu mmoja wa Misri alikwenda Madina, akalalamika kwa Khalifa kuhusu gavana. Mlalamikaji aliporudi Misri, gavana huyo akamuua.

Imesimuliwa kwamba kundi la masahaba waliokuwa Madina waliwaandikia barua masahaba wenao waliokuwa majimbo mbali mbali, wakisema: “Kama mnataka kufanya Jihad, njooni kwetu. Dini ya Muhammad inanajisiwa na Khalifa wetu. Kwa sababu hii, watu wamemgeuka na kuasi.”<sup>121</sup>

## SASA WATU WAKAMKUMBUKA ALI.

Kuendelea kurudi nyuma kwa matukio ya kisiasa kuliwafanya Waislamu wasio Maquraishi kutambua ukubwa wa msimamo wa kimakosa wa Maquraishi kwa Ali. Sasa waliweza kuona kwa uwazi kabisa ukubwa wa

<sup>120</sup> Al-Baladhuri, *Ansabul Ashraf*, sehemu 4, uk. 46.

<sup>121</sup> Ibn al-Athiir, Al-Kamil, Juz. 3, uk. 73 na 83.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

kosa ambalo lilifanywa na wajumbe wa Jopo la Uchaguzi walipoche pua ukhalifa kutoka kwa Ali na kumpa Uthman. Kwa kufanya hivyo, waliuswaga umma na kuingia kwenye kilele cha hatari ambayo ilikuwa hijapata kutokeea. Watu wenye busara walielewa dhahiri kwamba umma usingeingia kwenye kilele cha mgogoro kama Ali angekuwa Khalifa. Hivyo, watu walianza kufikiria kwamba uongozi wa Ali ulikuwa ndio ufumbuzi wa tatizo la umma.

Watu walizungumzia habari za Ali bila kuficha na kwa sauti za kusikika na Uthman alianza kuona kwamba kuwepo kwa Ali na yeye Madina ni hali iliyofanya matatizo kuwa makubwa zaidi. Uthman alimwomba Ali aondoke Madina aende kwenye kiunga chake huko Yunbu, ili watu labda wangemsahau; lakini mgogoro ulipozidi kuwa mkubwa, alimwambia arudi Madina ili aweze kuwa kama ngao yake dhidi ya hatari. Halafu Ibn Abbas alikwenda kwake akiwa na ujumbe kutoka kwa Uthman, ambao ulimtaka aondoke aende Yunbu, akitegemea kwamba watu wangeacha kutamka jina lake. Imam akasema: “Ewe Ibn Abbas, Uthman anataka kunifanya mimi kama ngamia, kwenda na kurudi ndoo za maji zikiwa zimejaa. Aliniambia niende Yunbu, halafu akaniambia nirudi. Sasa ananiambia niondoke kwenya Yunbu tena. Wallahi nimemtetea hadi nikaogopa kwamba huenda ninatenda dhambi.”<sup>122</sup>

Ali aling’amua kwamba Uthman mwenyewe alikuwa ni tatizo kubwa zaidi kuliko lile ambalo Uthman alikuwa anakabiliwa nalo. Mambo yote yalikuwa chini ya uwezo wa Uthman kwa kubadilisha sera yake kama ufumbuzi wa kutatua matatizo yake yote yaani, jinsi ya kushughulikia hazina ya umma, kuwafukuza kazi ndugu zake, na kumwondo Marwan asiwe karibu naye. Hatua hizi zingemrejeshea uaminifu wa watu kwake na kuridhika kwao.

<sup>122</sup> *Nahjul Balaghah*, sehemu ya 2 uk. 233.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Kwa upande mwingine, Ali hakuwa na njia za kutatua tatizo lake na tatizo la umma lililopo kwa Uthman mwenyewe. Ali alikuwa anaona kupitia nuru ya Mwenyezi Mungu kwamba kuendelea kudumu kwa umma na hatima yake ni hali ambayo ingeamuliwa kwa kiwango kikubwa na jambo amba-lo lingempata Uthman. Uthman alikwishaanzisha sera ambayo ingewawezesha ukoo wa Bani Umayyah kutawala dunia ya Waislamu kwa vizazi vingi vifuatavyo. Bado watu wa ukoo wa Bani Umayyah walifa-hamika kwa wao kutokuwa waaminifu kwa Uislamu. Walisilimu hapo tu ambapo waliona wameshindwa kabisa.

Ali aliwatambua vizuri sana kama watu wazima na watoto. Ni yeye ndiye aliyevunja nguvu yao na kuwadhalilisha hadi wakakubali imani ya Uislamu kwa shingo upande. Alijua kwamba kama wangepata mamlaka wangekula hazina ya umma, wangewafanya watumwa watumishi wa Mwenyezi Mungu na kunajisi dini Yake.

Uthman alikuwa na mambo matatu ya kuchagua: (1). Kujiuzulu; (2). kung'ang'ania sera yake na kukataa kujiuzulu, au (3) abadili kabisa sera yake. Njia mbili za kwanza zilikuwa uovu na ya tatu haikutarajiwa. Kama angeamua kuendelea na sera yake, angeuawa. Mauaji yake yangekuwa tukio baya na la kuogofya. Angekuwa Kiongozi wa kwanza kuuawa na Waislamu. Watu wa ukoo wa Bani Umayyah, ndugu zake khalifa, tayari walikwishakuwa na uwezo wa kutosha kuwawezesha kuwapa changamoto Waislamu wema kwa kuanzisha vita, kulipa kisasi cha kifo chake, kuki-tumia kifo hicho kama njia ya kunyakua mamlaka.

Kama Uthman angelazimishwa kujiuzulu na watu wamchague mtu wa kumrithi, watu wa ukoo wa Bani Umayyah, wakiwa na uwezo mkubwa, hawangekubali kushindwa. Wangeweza kudai kwamba Uthman alikuwa Khalifa halali na kwamba kumlazimisha kujiuzulu hakungeondoa uhalali wa uongozi wake. Kwa sababu hii, wangefikiria malengo waliyoyataka. Na ingekuwa rahisi zaidi wao kufanikisha lengo lao kama angeuawa.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Njia ya tatu haikutegemewa. Hapakuwepo katika tabia ya Uthman kuonesha uwezekano wa mabadiliko yanayotakiwa. Hata kama angetaka kubadilisha sera yake ya fedha na kuwafukuza ndugu zake waovu, Marwan angemshawishi asifanye hivyo, na alikuwa hana ushupavu ambaao ungempa kinga ili aepuke ushawishi wake.

Ali alitambua yote haya. Bado alijaribu kila iwezekanavyo kufikiria njia ya tatu ili kuepuwa uovu wa njia mbili za kwanza. Waandishi wa historia wanatutaarifu kwamba kundi la masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambaao walikuwa wanaishi Madina, waliwaandikia barua masahaba waliokuwa kwenye mipaka ya serikali ya Waislamu, wakisema: “Njooni rudini Madina. Jihad ipo hapa.” Watu walikuwa wanamsema Uthman kwa ubaya na hakuna sahaba aliyemtetea isipokuwa Zayd Ibn Thabit, Abu Usaid Al-Sa’idy, Kaab Ibn Malik na Hasan Ibn Thabit. Hawa walikuwa waaminifu kwa Khalifa kwa sababu walipokea zawadi zake za ukarimu.

### IMAM ANAPATANISHA.

Masahaba walikutana na wakazungumza na Ali ili awe mpatanishi baina yao na Uthman. Alikutana na Khalifa na akazungumza naye, akasema: “Watu walioko nyuma yangu waliniomba niwe mpatanishi baina yako na wao. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, sijui ni kwambie nini. Wala siwezi kuonesha mambo ambayo wewe huyajui. Umemuona, umesikia na uliambatana naye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ukapata sifa ya kuwa mkwe wake. Wewe pia unategemewa kufanya mema kama alivyofanya Ibn Abu Quhafan (Abu Bakr) na Ibn Al-Khatib (Umar). Wewe uko karibu zaidi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuliko wote wawili na umepata kwa sababu ya ndoa kile ambacho wao hawakukipata. Wala hawakukutangulia kwa lolote. Wallahi ninakuomba ujihurumie wewe mwenywewe. Huna maradhi ya upofu wala ujinga. Njia iliyonyooka inaonekana wazi na dhahiri na mipaka ya dini haibadiliki.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

“Ewe Uthman, kumbuka kwamba mtumishi wa Mwenyezi Mungu aliye bora mbele ya Mwenyezi Mungu ni Kiongozi anaye tenda haki ambaye ameongozwa kwenye ukweli na yeye huongoza kuelekea kwenye ukweli. Hivyo, anathitisha maadili yajulikanayo na huondosha na kuacha bidaa. Aliye mbaya kuliko wote ni Imam aliye dhalimu ambaye si mnyoofu na huongoza kuelekea kwenye upotovu. Hivyo, huondosha maadlili yajulikanayo sana na kuhuisha bidaa iliyoachwa.

“Nimemsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: Kiongozi asiyetenda haki, mnamo Siku ya Hukumu ataletwa akiwa hana msaidizi wala mtetezi. Atatupwa Jahanamu ..... Ninakuonya kuhusu ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na machungu na adhabu Yake. Hakika adhabu Yake ni chungu na ni kali. Ninakuonya usijekuwa Kiongozi aliyeuawa wa umma huu. Inasemekana kwamba Kiongozi atajauawa na kifo chake kitafungua mlango wa umma kuanza mauaji na vita hadi Siku ya Hukumu. Atachafua mambo ya umma na kuwatupa Waislamu kwenye mifarakano, hivyo kwamba hawataweza kuona ukweli kwa sababu ya urefu wa udanganyifu ...”<sup>123</sup>

Maneno ya Imam hayakumfurahisha Khalifa. Mazungumzo baina ya watu wawili yalifanyika ifuatavyo:

**Uthman:** “Umar aliteua na kuwaweka kwenye ofisi watu kama hao ambao mimi nimewateua na kuwaweka kwenye ofisi.”

**Ali:** “Umar aliwateua watu kama hao lakini alikuwa anawakemea. Alipogundua ukiukwaji mdogo umefanywa na yejote mionganoni mwao, alimuita na kumwadhibu vikali. Wewe umedhoofu kwa sababu unawahurumia sana ndugu zako.”

<sup>123</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, Sehemu ya 3 uk. wa 76.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

**Uthman:** “Watu hawa ni ndugu zako pia.”

**Ali:** “Ndio, ni ndugu zangu, lakini hawana uadilifu.”

**Uthman:** “Hujui kwamba Umar alimteua Muawiyah na akamwacha akaendelea na kazi yake hadi mwisho wa utawala wake?”

**Ali:** “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, ninakuuliza. Hujui kwamba Muawiyah alikuwa akimuogopa Umar zaidi ya Yarfah, mtumishi wa Umar.”

**Uthman:** “Ndio.”

**Ali:** “Muawiyah hufanya uamuzi bila kupata ushauri wako, halafu huwaambia watu: ‘Hii ni amri ya Uthman.’ Wewe unajua na hubadilishi kitu chochote. Wala humwambii aache hayo anayofanya.”<sup>124</sup>

Hivyo Ali, tofauti na mtu mwingine yejote hakutumia matatizo ya vurugu za Khalifa ambaye alimuona kuwa mpotoaji wa haki yake ya uongozi kwa manufaa yake. Alijitokeza na kuushinda udhaifu huo na akawa mlinzi wake mkubwa akawa anajaribu kurekebisha hali ya mshindani wake kwa sababu hatima yake ilikuwa na uhusianao wa hatima ya umma wote. Lakini Uthman aliuchukulia ushauri wa Ali kuwa uchochezi. Alikwenda kwenye mimbari akatoa hotuba kali akiwatishia wapinzani kwamba angewaadhibu vikali. Alikuwa anategemewa kufanya hivyo tu, almuradi Marwan alikuwa mshauri wake mkuu. Hivyo, moto wa upinzani ulielea kuwa mkali.

## MAKAZI YA KHALIFA YAZINGIRWA.

Ujumbe uliopelekwa na masahaba waishio Madina kwenye majimbo mbali mbali ilitetea matokeo yaliyotarajiwa. Makundi kutoka Misri, Kufa, na

<sup>124</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk. 76.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Basra yalikwenda Madina na kumtaka Khalifa kuwafukuza ndugu zake waliomo kwenye kazi za utawala au ye ye ajiuzulu. Vinginevyo, walikuwa tayari kumuua. Khalifa alipotambua uzito wa hali, alikwenda kwa Ali na akamwomba afanye usuluhishi baina yake na washindani wake.

Ali alimuuliza: "Masharti yako ya mapatano yakoje?" Khalifa alijibu: "Wewe umepewa mamlaka kamili ya kuahidi kwao chochote utakachoona kinawafaa." "Mimi nitatekeleza lolote utakalo pendekaze" Ali alimkubusha kwamba aliwahi kuzungumza naye mara nyingi kuhusu hatua fulani za kurekebisha na kwamba Khalifa mara kwa mara aliahidi kutekeleza hatua hizo. Halafu, ahadi hazikutekelezwa na Khalifa, ambaye alikuwa kwenye mvuto wa Marwan, Muawiyah, Ibn Amr na Abdullah Ibn Saad Ibn Abu Sarh. Uthman akajibu: "Sitawati wao, nitakutii wewe."

Akiwa amefuatana na watu thelethini wa kabile la Quraishi na wengine kutoka Madina, Imam alikwenda kukutana na kundi la Misri. Aliwapa maelezo ya kuridhisha na akawaambia wasikimbile matumizi ya nguvu na aliwaahidi kwa niaba ya Khalifa kutimiza madai yao ya kuwafukuza ndugu zake na kubadili sera yake kuhusu ugawaji wa hazina ya umma. Alipokwenda kwa Khalifa alimshauri aende msikitini na atoe ahadi hadharani ya kufanya mabadiliko.


## KUTUBIA NA KUJIRUDI.

Khalifa alitiikia na kukubali ushauri mzuri. Alikwenda kwenye mimbari na akahutubia jamii, akasema: "Mimi ni wa kwanza anayetakiwa kumtii Mwenyezi Mungu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu anisamehe kwa yale ambayo nimeyafanya. Nitatubu Kwake. Mtu kama mimi anatarajiwa kubadilika na kutubu. Nitakapoteremka chini viongozi wenu waje ili wafanye uamuzi kuhusu mimi. Wallahi endapo haki itaniteremsha daraja na kuwa mtumwa nitafanya kama afanyakyo mtumwa, na nitakuwa mnyenyeketu kama mtumwa.


**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Si rahisi kukwepa hasira ya Mwenyezi Mungu isipokuwa kumwendea Yeye. Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, nitawapeni myatakayo hadi mtosheke na nitamweka Marwani na ndugu zangu mbali na mimi. Nitakuwa na nyinyi mionganoni mwenu.<sup>125</sup>

Maneno haya yaliwasisimua wasikilizaji. Walilia hadi machozi yalilowesha ndevu zao, na Khalifa naye akalia, na watu wakawa na matumanini mazuri.

Marwan alikuwa anangojea. Mara tu Uthman aliporudi nyumbani kwake, Marwan alimgeuza mawazo akarudi kwenye msimamo wake wa zamani. Marwan alitoka nje akakabiliana na umati wa watu waliokuwa wanasubiri mageuzi. Akawakaripia na akawaambia ...Mmekuja kutunyang'anya mamlaka ambayo yapo mikononoi mwetu. Ondokeni nendeni zenu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mkitupatia changamoto, mtakiona cha mtema kuni ..." 

Ali alipotambua nini kilichotokea alisema: "Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, mimi nikikaa nyumbani kwangu yeye anasema; 'Unaniangusha licha ya uhusiano wangu wa kindugu na wewe na kile ninachostahili kuto-ka kwako.' Nikijaribu kumsaidia na juhudzi zangu zikisababisha matokeo mazuri, Marwan humshauri na humdanganya. Amekuwa kitendea kazi kitii fu mikonini mwa Marwan baada ya kuwa sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."<sup>126</sup>



Alikwenda kwa Uthman na akazungumza naye kwa ukali akasema: "Hungemridhisha Marwan isipokuwa ukengeuke kutoka kwenye dini na busara yako. Umekuwa kama ngamia wa kipando anayeongozwa na mshika hatamu wake na kuelekea popote atakiwapo. Wallahi, ninabashiri kwamba Marwan atakupeleka hatarini, lakini atashindwa kukuokoa. Sitarudi tena kwako baada ya leo. Umeharibu heshima yako na umepoteza

<sup>125</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk. 82.

<sup>126</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk. 82.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

uwezo wa maamuzi.”<sup>128</sup>

Ali aliacha upatanishi baina ya Uthman na waasi. Uthman alipozingirwa nyumbani kwake, alikwenda kwa Ali na akamwambia: “Ninayo haki ya udugu wa Uislamu, uhusiano na wewe na mimi kuwa mkwe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Endapo hapana lolote kati ya mambo haya lililokuwepo na tungkuwa kwenye siku za ujahiliya, ingekuwa aibu kwa wana wa Abu Munaf (babu wa babu wa ukoo wa Hashim na Bani Umayyah) kumruhusu mtu kutoka Taymi (Talha Ibn Ubaidullah) atunyang’anye mamlaka yetu.”

Talha alikuwa anaunga mkono kwa bidii sana waasi. Aliwasaidia na akakubaliana na mpango wao wa kumzingira Uthman. Labda uvamizi wao wa Madina ulikuwa matokeo ya mawasiliano yake na uchochezi wake.

Ali alikwenda kwa Talha na aliwakuta watu wamekusanyika na kumzunguka pande zote. Alimuuliza Talha: “Mambo gani haya unajihusisha nayo?” Talha alijibu: “Umechelewa mno.” (Alimaanisha kwamba mwisho wa Uthman ulikuwa umefika) Ali alikwenda kwenye jumba la hifadhi ya hazina na akataka pafunguliwe. Funguo zilipokosekana alivunja mlango na aligawa baadhi ya vitu vilivyokuwa humo mionganini mwa watu waliokuwa wamemzunguka Talha. Watu hao waliondoka na wakamwacha peke yake, na Uthman alifurahishwa na tukio hilo. Talha alikwenda kwa Uthman na kamwambia: “Ewe Amiri wa waumini, nilitaka kitu fulani na Mwenyezi Mungu amenizua nisikipate.” Uthman alimjibu: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, wewe hukuja kutubu; ni kwamba umeshindwa kabisa. Mwenyezi Mungu akuwajibishe kwa yale uliyoyafanya.”<sup>128</sup>

Ibn Al-Athiir amesimulia kwamba Ibn Abbas alisema: “Nilikwenda kwa Uthman alipozingirwa. (Ilikuwa kabla Uthman hajampeleka Ibn Abbas kama kiongozi wa mahujaji wa Hija ya mwaka huo). Yeye (Uthman) alinishika mkono wangu na akaniongoza kuelekea mlangoni, akaniamuru

<sup>127</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk. 84.

<sup>128</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk.82.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

niyasikilize maneno ya waliozingira nyumba yake. Baadhi yao walikuwa wanasema: Tunangoja nini? Wengine walisema: “Na tungoje. Labda anaweza kubadilika.” Tulipokuwa tumesimama, Talha alikuja na akaulizia kuhusu Ibn Udais (mmojawapo wa viongozi wa waasi wa Misri) Ibn Udais alikwenda kwa Talha, na wakateta jambo. Ibn Udais aliporudi, aliwaagiza wafiasi wake wasimruhusu mtu yejote kuingia au kutoka ndani ya nyumba ya Uthman.

Uthman akamwambia Ibn Abbas: “Hili ni agizo la Talha, Mwenyezi Mungu na amwangalie Talha. Amewachochea watu hawa dhidi yangu. Wallahi, nina matumanini kwamba mgawo wake wa Ukhilifa utakuwa sufuri na kwamba atauawa.” Ibn Abbas akasema: “Nilipotaka kuondoka wao waliniuzia hadi Muhammad Ibn Abu Bakr aliponiombea ruhusa.”<sup>129</sup>

Kuhusu Zubeir, inasemekana kwamba aliondoka Madina kabla Uthman hajauawa. Waandishi wa historia wengine waliandika kwamba alikuwepo Madina wakati alipokufa Uthman. Aisha alikwenda Hija na alipokuwa kwenye shughuli za ibada aliwasihii watu wamkane Uthman.

Uthman alipozingirwa, waasi walikata huduma ya maji. Ali alikwenda na kiriba cha maji na akazungumza na Talha, akasema: “Maji haya apewe Uthman,” Maji hayo alipewa Uthman. Alijaribu mara nyingine kumpelekea maji Uthman na akazungumza na waasi, akasema: “Mnachofanya hakifanani na matendo ya waumini au wasioamini! Msiondoe huduma ya maji kwake. Warumi na Waajemi walimlisha na kumpa maji mfungwa wao.” Lakini waasi walikataa maji yasimfikie Uthman.

Kuzingirwa kwa Khalifa kuliendelea kwa siku arobaini. Waasi walikuwa wanamlazimisha Uthman abadili sera yake au ajiuzulu. Alikataa kujiuzulu, akasema: “Siwezi kuvua shati ambalo Mwenyezi Mungu amenivisha.”

<sup>129</sup> Ibn al-Athiir, *Al-Kamil*, sehemu 3, uk. 87.

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

Labda Uthman alikuwa sahihi kukataa kuijuzulu. Lakini alikosea kusema kwamba ukhalifa ni shati ambalo Mwenyezi Mungu alimvisha, kwani uongozi wake haukutokana na uteuzi wa Mwenyezi Mungu au Mtume Wake (s.a.w.w.). Mtu aliyemvisha shati ni Abdul-Rahman Ibn Auf na nyuma yake Maquraishi; au tunaweza kusema kwamba Khalifa wa pili ndiye aliyemvisha Uthman shati hilo.

Inaonesha kwamba waasi hawakuwa na nia ya kumlazimisha Khalifa ajiuzulu wala hawakuwa tayari kumuua. Walichotaka kutoka kwake ni kubadili sera yake ya kushughulikia hazina ya umma, kuwafukuza katika kazi ya ugavana ndugu zake na Marwan asiendelee kuwa mshauri wake mkuu. Aliahidi kufanya hivyo, lakini kamwe hakutekeleza ahadi yake. Hivyo, walimtaka ajiuzulu na alikataa. Sasa baadhi ya waasi walikimbilia matumizi ya nguvu.

### MUAWIYAH ALIMKATISHA TAMAA KHALIFA.

Inashangaza kwamba Muawiyah na magavana wengine wa ukoo wa Bani Umayyah hawakujaribu kwa dhati kumuokoa Khalifa ambaye ni ndugu yao. Hawakupeleka majeshi kusitisha kuzingirwa kwa Khalifa au kuwazuia wavamizi wasimuue. Bado Khalifa aliomba msaada wao. Imesimuliwa kwamba Muawiyah alipeleka jeshi ambalo lilifika karibu ya Madina lakini wakati huo Khalifa alikwishingirwa. Muawiyah alimurumu Kamanda wa jeshi hilo asifanye lolote hadi atakapopata amri kutoka kwake. Alimwambia: “Usiseme kwamba aliyepo anaona kile ambacho asiyekuwepo hawezi kukiona. Wewe ni asiyekuwepo na mimi ni aliyopo.”

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### WATU WA MADINA PIA WALIMKATISHA TAMAA KHALIFA.

Kitu kingine ambacho kinaweza kuonekana kwa urahisi kwenye matukio ya siku hizo yaliyosimuliwa ni kutokuwepo na upinzani wowote kutoka kwa watu wa Madina. Wala hawakuwapinga waasi waliovamia, ama kuwazuia wasimuue Khalifa. Inaonesha kwamba Maquraishi katika wakazi wa Madina (isipokuwa ukoo wa Bani Umayyah) hawakuwa na huruma kwa Uthman. Walikinahi na mwenendo wa Bani Umayyah na kasi kubwa ya ongezeko la ushawishi wao katika ulmwengu wa Waislamu. Maquraishi walio wengi walioko Madina walikuwa pamoja na Aisha, Talha na Zubeir kimsimamo na hisia zao kuhusu Khalifa.

Wakazi wengi wa Madina hawakufurahishwa na sera za Uthman za kuwatkuza watu wa kabile la Quraishi na kuwaweka Bani Umayyah, ukoo ambao mionganii mwa Maquraishi si wafuasi makini wa dini, kwenye shingo za Waislamu. Wazalendo wa Madina kwa dhahiri hawakuwa wanajihisi kuwa wanamuunga mkono Khalifa, kwa sababu wao walikuwa hawapokei mgawo wa ukarimu wake sawa na ule waliokuwa wanapata Maquraishi. Kwa tabia yao, wenyeji wa Madina walikuwa washika dini zaidi kuzidi Maquraishi.

Hivyo wakazi wengi wa Madina walimkatisha tamaa Uthman na hawakumpa ulinzi, ingawa kwa idadi walikuwa wengi zaidi ya waasi wavamizi.

Imam Ali alikuwa sahaba ambaye hakutaka kabisa Uthman auawe na alikuwa mkweli sana katika kujaribu kurekebisha sera ya Khalifa. Si tu kwamba alionesa huruma yake kwa Khalifa kwa maneno tu, alijaribu kumpa ulinzi kwa kutumia silaha. Alihatarisha maisha ya watoto wake wawili; Al-Hasan na Al-Husein ambao kwake walikuwa na thamani zaidi

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kuliko macho yake mawili. Aliwapeleka hao vijana wawili wamlinde Uthman na aliwaagiza wasimame mlangoni kwake wakiwa na silaha ili wawazuie waasi wasiingie nyumbani kwa Uthman.

Hatimaye, waasi walipewa taarifa kwamba majeshi kutokea miji mbali mbali yalikuwa njiani kwenda Madina kumuokoa Uthman. Baadhi ya waasi walihisi kwamba ufumbuzi mmoja tu uliokuwepo hapo ni kumuua Khalifa. Kwa kuwa hawangeweza kuingia mlangoni, walipanda juu ya nyumba kupitia kwenye ukuta na wakamuua ambapo walinzi waliokuwa mlangoni hawakujua kilichotokea ndani!

Hivyo, jambo ambalo Ali alijaribu kulizuia kwa bidii sana lilitokea, na juhudzi zake zote kuzuia jambo hilo lisitokee zilishindwa. Mauaji ya Khalifa yalikuwa tukio bayo sana ambalo matokeo yake yalikuwa yanahatarisha kuendelea kudumu kwa Uislamu na Waislamu. Jambo hili halingetokea kama Khalifa angesikiliza na kuzingatia ushauri wa Ali, kwa kuwafukuza kazi maafisa waovu kutoka kwenye serikali yake na kuitakasa serikali isiwe na ujisadi.

Kama Uthman angesikia ushauri wa Ali kwa kufuata sera ya wenzake wawili waliomtangulia, Abu Bakr na Umar, hangeuawa. Lakini Khalifa huyu wa tatu hakuwa na uwezo wa kudhibiti mambo. Marwan, mtoto wa mtu aliyepewa adhabu ya uhamisho na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alikuwa ndiye mtawala halisi wa ulimwengu wa Waislamu na mshauri mkuu wa Khalifa. Marwan alikuwa na uwezo wa kuendesha na kumwelekeza popote alipotaka.

Hata hivyo, nina shaka kwamba Uthman alikuwa anaweza, hata kama alitaka kufanya hivyo, kumfukuza Muawiyah ambaye alikwishakuwa na uwezo zaidi kumzidi Khalifa. Na tudhani kwamba Uthman alimwambia Muawiyah kuondoka kwenye kazi yake ya ugavana na akakataa kutii. Uthman angejaribu kumlazimisha aondoke ofisini? Na Uthman alikuwa na uwezo wa kutosha kufanya hivyo?

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

### **MAZINGATIO**

Tunapokaribia kuhitimisha maelezo yetu mafupi ya matukio ya siku za Uthman na mwisho wake wa kusikitisha, tunalazimika kukumbuka yafuatayo:

Ukhalifa wa Uthman na matukio yake umethibitisha kwamba uongozi wa ulimwengu wa Uislamu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ungeteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na si kuchaguliwa na masahaba. Alikuwa ni yeze peke yake aliyesaidiwa na ufunuo na Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwajua wenyewe sifa nzuri sana za uongozi mionganini mwa watu wa Nyumba yake na masahaba.

Uongozi haungeachwa kwenye hali ya fursa za uchaguzi wa Waislamu kwa ujumla au wa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au wa udikreta hususan kama ule wa jamii ya Quraishi. Wala haungeachwa kwenye fursa ya uteuzi kutoka kwa Khalifa aliyekwisha kuchaguliwa kwa uwazi au kwa undani. Wala uongozi haungeachwa kwenye uchaguzi wa wajumbe wa Jopo la uchaguzi. Uchaguzi au uteuzi kama huu ungeweza kumweka mtu bora sana au nzuri anayefuatia au mbaya sana kwenye mamlaka ya uongozi. Hii ni hatari kwa mustakabali wa umma unaobeba ujumbe kwa ajili yake wenye na kwa ajili ya ulimwengu wote, hasa zaidi pale ambapo umma bado upo kwenye mwanzo wake wa maendeleo na kukua. Uchaguzi wa aina hii wakati mwingine ungeleta kwenye mamlaka ya uongozi, uongozi dhaifu ambao hauna uwezo wa kubeba ujumbe. Wakati mwingine ungeweza kuleta uongozi imara ambao ungepotosha umma na ujumbe, kwa kukusudia au bila kukusudia, kutoka kwenye njia yao ilionyooka ambayo ilikuwa imeamriwa na mtu wa ujumbe.

Kufuzu kwa uchaguzi wa kwanza uliofanywa na masahaba na uteuzi wa kwanza wa Khalifa aliyechaguliwa ambao ulimweka Abu Bakr na Umar

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

kwenye mamlaka ya uongozi, uliwafanya Waislamu waandishi wa historia na wanachuo kutotilia maanani uharibifu uliosababishwa na kushindwa kwa uchaguzi wa Khalifa wa tatu. Mafanikio ya Makhalifa wawili wa mwanzo yamedumaza akili za Waislamu. Hawakuweza kuona kwamba matukio ya Ukhalifa wa Uthman yalitoa ushahidi wa wazi kwamba uchaguzi si njia iliyio salama ya kufuatwa na umma wenye ujumbe wa mageuzi.

Waislamu wamesahau ukweli ulio dhahiri kwamba madhumuni ya ujumbe wa Kiislamu ilikuwa si kuanzisha serikali adilifu ambayo ingedumu miaka kumi na mbili au thelathini tu. Makusudio ya ujumbe wa Mbinguni yalikuwa na lengo la juu na la muda mrefu zaidi.

Hapo Ghadir Khum, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipotangaza uongozi wa Ali na watu wengine waliotakaswa wa Nyumba yake, alikuwa anafuata njia ya kawaida tu. Hivi ndivyo inavyotakiwa kufanywa na kiongozi yeyste wa serikali anapokaribia kumaliza muhula wake wa kazi.

Hi hii ingekuwa kweli iliyio dhahiri pale ambapo kiongozi wa nchi ni mwenye kubeba ujumbe muhimu sana ambamo humo ndimo chimbuko la Dola inamoundwa na Serikali yake inatakiwa kubeba ujumbe huo na kuupeleka kwenye mataifa ya dunia na pia kwa watu wake.

Upotofu wowote unaotokea kwenye ujumbe kwa ujinga, udhaifu, ukosa ucha-Mungu wa uongozi, unaweza kuingiza ujumbe wote hatarini. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anaingalia hali ya siku za usoni kupitia kwenye nuru ya Mwenyezi Mungu alipopendekeza kwa ajili ya umma, wakati anakaribia kukata roho, kuwa na hati ya maandishi – yenye maelekezo - ambayo kwayo umma haungepotea baada yake.

Alibashiri kwamba baada yake Waislamu wangekabiliwa na hatari nyingi zenye kujaribu imani zao. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu kumteua kiongozi wa umma ambaye anazo sifa za kweli za uongozi ili aweze kuuweka umma

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

huo kwenye njia iliyonyooka.

Kwa bahati mbaya sana, Umar, akisaidiwa na masahaba wengine, walikataa pendekozo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wakidai kwamba alikuwa amezidiwa na maradhi na kusema Kitabu cha Mwenyezi Mungu kingewatosha.

Matukio ya Jopo la uchaguzi ambalo lilimpa Uthman mamlaka, na matukio yaliyotokea wakati wa kipindi cha ukhalifa wake na matokeo yake yameonesha ukubwa wa kosa la Umar. Kitabu cha Mwenyezi Mungu hakikumzuia yeye kuunda Jopo la Uchaguzi ambalo lilimnyang'anya Ali uongozi na kumpa Khalifa Uthman. Kitabu cha Mwenyezi Mungu hakikumzuia Uthman kufanya makosa ya dhati, wala hakikuwazua Waislamu wasitumie nguvu katika kujibu kushindwa kwake kuendesha mambo ya Waislamu na kufuatiwa na vita kadhaa vyta wenye kwa wenye baada ya kifo chake na kusababisha umwagaji damu mkubwa.

Ili Kitabu cha Mwenyezi Mungu kiweze kazi na kuwazuia watu wasichukue njia inayoelekea kwenye upotofu, lazima kiunganishwe na uongozi madhubuti na imara wenye ujuzi mkubwa kufasili Kitabu hicho na pia mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Uongozi wa aina hii hukizewesha Kitabu cha Mwenyezi Mungu kufanya kazi na kuwaelekeza watu kwenye njia ya Qur'an.

Uongozi huu ndio ambaa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitaka kuupata kwa ajili ya umma kwa njia ya kuandika pendekozo lake lenye maelekezo kwa maandishi. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na maana hii alipotangaza mnamo siku hiyo ya Ghadir Khum alipowaambia Waislamu kwamba alikuwa anawachia vitu viwili ambavyo vingewaepusha wasije kutumbukia kwenye uovu na kuacha njia iliyonyooka, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na watu wa Nyumba yake, na kwamba vitu hivi viwili kamwe havitaachana.

**Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume****Sehemu ya pili**

Kukataza kuandikwa pendekezo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lenye maelekezo, kuligharimu umma mshikamano wake wa kisiasa na kiroho na kuusababishia umma pigo lisilorekebishika. Masahaba walipopuuza kuzingatia tangazo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) la hapo Ghadiir Khum na kukataa waraka alioupendekeza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), walisukumwa na ubinafsi wao.

Walikuwa hawapendelei kumpa Ali uongozi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu hawakutaka kuuachia ukhalifa kwenye ukoo wa Hashim. Kumruhusu Ali kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kingekuwa kitendo cha kukubali, angalau kwa njia isiyo wazi, kwamba uongozi wake (Ali) uliamriwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.) ambaye alisadikisha kwamba watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kamwe hawangefarakana na Qur'ani Tukufu. Hii ingeuweka uongozi kwenye kundi hili lenye kuheshimiwa sana.

Masahaba wa Makka wa koo mbali mbali hawakuwa radhi kuacha mata-manio yao. Walitaka kuuweka ukhalifa kuwa kitu cha kushindaniwa kwa kumpa mtu wa Makka asiye wa ukoo wa Hashim. Katika hali hii ukhalifa ungepata hadhi ya kushindaniwa na kuwaruhusu watu wa koo mbalimbali kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kugombea uongozi kwa sababu hukuna aliye bora kuzidi mwenzake mionganoni mwao.

Nadharia hii iliwafanya kazi kwa muda fulani. Masahaba watatu, (Abu Bakr, Umar na Uthman) kutoka kwenye koo tatu za Makka walirithiana kwenye uongozi katika kipindi cha miaka kumi na tatu. Masahaba wenye tamaa, hata hivyo kwa kucheleva waliamka wakati wa utawala wa Uthman walipogundua kwa masikitiko sana, kwamba matumanini yao ya kufika kwenye kazi hiyo kubwa yalikuwa yanafifia. Walikabiliwa na kile ambacho walikuwa wanakiepuka.

Bani Umayyad walikaribia kufanya ukhalifa usiwe kitu cha kushindaniwa kwa sababu walikwishatawala ulimwengu wa Waislamu katika kipindi cha

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

miaka sita ya utawala wa Uthman. Walikaribia kuanzisha utawala wa kinasaba, ambao msingi wake si utakatifu na sifa bora ya Kiislamu kama ile ya watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), lakini msingi ulioegemezwa kwenye mamlaka yaliyopatikana kwa ujisadi, uporaji na umilikaji. Matokeo yake ya kwanza yaliyotegemewa yalikuwa ni kumzuia sahaba yejote mwenye shauku asifike kwenye ofisi hiyo ya Juu. Majeruhi wa kwanza wa maendeleo haya yangekuwa ni ndoto za Talha, Zubeir, Abdul-Rahman na Aisha.

Wakipata msukumo kutokana na woga wa kutawaliwa kwa nguvu na ukoo wa Bani Umayyah watu hawa wenye kutaka makuu walianza kampeni yao dhidi ya Khalifa wa Tatu. Walijaribu kuzuia ndoto ya kuanzisha utawala wa ufalme wa kinasaba na kuwafungulia tena Mlango wa Uongozi watu wa Jopo la Uchaguzi.

Masahaba hawa wenye tamaa walikuwa hawamuogopi Ali, kwani waliamini kwamba wangeweza kuziba njia yake ya kufika kwenye ukhalifa pindi Uthman akifa. Mpinzani wake alikuwa Kureishi na Maquraishi, ndio walikuwa watu wenye kuathiri uteuzi wa kiongozi. Hapana mtu mwingine aliyelijua hili zaidi ya Ali ambaye aliwaambia Bani Hashim wakati wa Mkutano wa Uchaguzi kwamba: “Almuradi watu wenu (Maquraishi) wanapewa utii (katika ule wakupewa ninyi), basi ninyi ham-tapewa uongozi kamwe.”

Hata hivyo, matumaini ya masahaba wenye shauku hayakutokea kuwa kweli. Hawakujumuisha katika mpango wao ukweli kwamba Quraishi wangepoteza udhibiti wa kisiasa kwa kipindi kifupi baada ya kifo cha Uthman, ambapo watu wengine, mbali na Maquraishi ndio wangekuja kuwa wenye athari ya uteuzi wa kiongozi.

\* \* \* \* \*

## **Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume**

## **Sehemu ya pili**

**“Tunazitia hofu nyoyo za waliokufuru katika walivyomshirikisha Mwenyezi Mungu na washirikina ambao hakuwateremshia hoja yoyote. Na makazi yao ni motoni; na ni maovu yaliyoje maskani ya wenye kudhulumu.”**

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

### ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangaa wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba' Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102. Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

114. Iduwa ya Kumayili.
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenyе hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt  
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia
171. Amali za Makka
172. Amali za Madina
173. Uislamu na mfumo wa Jamii ya dini nyingi
174. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
175. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
176. Elimu ya Tiba za Kiislam Matibabu ya Maimamu
177. Falsafa ya Dini

## BACK COVER

Imam Ali (as) hakuwa kiongozi wa Waislamu tu bali wa wanadamu wote. Maisha na mwenendo wa Imam Ali (as) umewavutia watu wote, marafiki

## Imam Ali (a.s) Binamu yake Mtume

## Sehemu ya pili

na maadui, hali ambayo imemfanya kuwa kiongozi wa umma.

Mtukufu Mtume (saw) alimtangaza mwanzoni kabisa mwa Ujumbe wake katika kile kikao mashuhuri kabisa cha “karamu ya jamaa”, aliposema: “Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu, waziri wangu, khalifa wangu na mrithi wangu. Basi msikilizeni na mumtii.” Hili lilikuwa tangazo la mwanzo kabisa alilolitoa Mtukufu Mtume (saw) kwa ajili ya Imam Ali (as) na aliendelea kuwakumbusha Waislamu kuhusu uongozi wa Imam Ali baada yake katika matukio mengi yaliyofuata baadaye, kama vile katika tukio la Ghadir Khum pale aliposema: “*Man kuntu mauwahu fahadha Aliyyun mawlahu* – Yule ambaye mimi kwake ni kiongozi basi na huyu Ali ni kiongozi wake.” Na mwisho ni tukio la “Karatasi” pale Mtukufu Mtume (saw) alipokuwa ni mgonjwa na maradhi yamemzidi akaomba aletewe karatasi, kalamu na wino, mashuhuri kama “hadithi ya karatasi.”

### Kimetolewa na kuchapishwa na:

#### Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: [alitrah@raha.com](mailto:alitrah@raha.com)

Tovuti: [www.ibn-tv.com](http://www.ibn-tv.com)

Katika mtando: [w.w.w.alitrah.info](http://www.alitrah.info)